# UKANDAMIZAJI WA JINSIA YA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI: *NJOZI YAPATA MTENZI* (MBATIAH: 2018) NA *NGUU ZA JADI* (MOMANYI: 2019)

**NA**

**PATRICIA WAENI JANVAN**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2023**

## UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kingine, kwa minajili ya shahada ya uzamili.

Sahihi …………...          Tarehe: 29 Novemba, 2023

**PATRICIA WAENI JANVAN**

**C50/38492/2020**

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi kwa idhini yetu kama wasimamizi.

**Prof. Kineene wa Mutiso**

Sahihi………………          Tarehe: 29 Novemba, 2023

(Msimamizi)

**Dkt. Mary Ndung'u**

Sahihi ………………          Tarehe: 29 Novemba, 2023

(Msimamizi)

# TABARUKU

Kwa babangu mpendwa Javan Anton

Kwa heshima yako, utabaki kuwa shujaa wa maisha yangu. Baba, ulikuwa ngao ya kunipa ujasiri. Ushauri wako utazidi kudumu milele. Mchango wako wa kukimu maisha yangu ulinipa uwezo wa kufikia nyota yangu. Mungu azidi kuilaza roho yako mahali pema.

Kwa Mamangu mpendwa Juliana Janvan

Kwa taadhima yako, mama ulinielewa, uliniombea, ukanihimiza na ukanihudumia kwa njia anuwai nilipokuwa ninasoma. Mungu akuzidishie rehema zake.

Kwa familia Yangu

Mama yangu mpendwa, Mkuu wa Gereza la Wanawake la Bungoma, Mrakibu Mkuu wa Magereza Phyillis Wafula Chida, mume wangu, Sajenti Mike Cullen Wasike, watoto wangu Laureen Amanda na Salma Arianna; uvumilivu na ushauri mlionipa ulinipa shime na ari ya kukamilisha tasnifu hii. Asanteni kwa kuwa marafiki wa karibu nilipowahitaji. Mungu awabariki.

# SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, afya njema na fursa ya kuweza kusoma hadi kiwango hiki. Fadhili na neema zake Rabana zilinijalia nguvu za kukabiliana na changamoto nilizokubana nazo.

Ninatoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu, Prof. Kineene wa Mutiso na Dkt. Mary Ndung'u kwa uvumilivu wenu, uelekezi mwema na ushauri bora. Mlinipa mapendekezo mazuri. Nyinyi ni msingi bora kwangu. Mungu awabariki sana na awajalie neema zake.

Vilevile, ningependa kuwashukuru wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi waliowahinifunza. Wahadhiri hawa ni pamoja na: Dkt. Hannah Chaga Mwaliwa, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Prof Mwenda Mbatiah, Dkt. Basilio Mungania, Dkt. Prisca Jerono, Prof. Rayya Timamy, Prof. Kyallo Wamitila, Dkt. Samson Ongarora Ontiri, Prof. John Habwe na Prof. Evans Mbuthia. Nimepata maarifa mengi kutoka kwa kila mmoja wenu. Mungu awazidishie baraka zake.

Aidha, shukrani za dhati ziwaendee wanafunzi tulioanza safari hii pamoja: Quinter Achieng, Peter Israel, John Shitemi, Lydia Nekesa na Innocent Okworo. Tulisaidiana na kuhimizana. Mungu awabariki sana.

Ningependa kuwashukuru ndugu zangu: Patrick Manthi, Kennedy Nyamai, Agnes Nzavila na Benjamin Sumbi. Pia, ningependa kuwashukuru: Lucky Maruti, Daisy Lukela, Walter Chida, Margaret Akoth, Agneta Atieno, Emmanuel Raila, Juliana Mwelu na Cate Muthoni. Mlinitia moyo na kunihimiza kwa hali na mali nilipokuwa nikishighulikia kazi hii. Asanteni sana.

**IKISIRI**

Katika utafiti huu tumeshughulikia ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* ya Mwenda Mbatiah (2018) na *Nguu za Jadi* ya Clara Momanyi (2019). Malengo ya utafiti huu ni: Kuchunguza makundi ya watu wanaokandamiza jinsia ya kiume, kubainisha athari za ukandamizaji wa jinsia ya kiume na kuchunguza mikakati ambayo wanaume wanatumia katika kupigania ukombozi wao katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019). Zaidi ya hayo, nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ni Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Nadharia hii iliasisiwa na Connel, R. (1987) na kuendelezwa na Bly, R. (1990) na baadaye Izugbara (2005). Nadharia hii humchora mwanaume akiwa mbabe kwa misingi ya rangi nyeupe ya ngozi na ya kibayolojia, humuona mwanaume kama mtekelezaji wa majukumu yote ya familia na jamii yake kulingana na mila, itikadi na matarajio ya jamii na pia, hueleza kuwa katika jamii kuna mwanaume mpya ambaye sio mbabe nyakati zote na hana tabia za mfumo-dume ambazo huashiria kuwepo kwa taasubi ya kiume. Matokeo ya utafiti huu ni pamoja na: Jinsia ya kiume imeonyeshwa kwa pande mbili. Kwanza, kuna wanaume wabinafsi ambao wanatumia ubabe wao kuwakandamiza wanaume ambao sio wababe. Pili, kuna wanaume wapya walioondokana na mfumo-dume, wanawajali wengine na wanandeleza ustawi wao, wanaume wengine na jamii yao. Utafiti huu utakuwa muhimu katika taaluma ya elimu jamii kuwahamasisha kuhusu masuala ya mahusiano mema ya kiuana na usawa wa kijinsia. Aidha, utafiti huu utakuwa muhimu katika kuendeleza taaluma ya Kiswahili hususan fasihi ya Kiswahili hasa katika uandishi wa riwaya ambao huzidi kukua na kubadilika na waandishi chipukizi wa riwaya watanufaika zaidi. Kadhalika, utafiti huu utatumika kuhamasisha jamii kuwa sio wanawake ambao hukandamizwa tu pia wanaume hukandamizwa na kuna haja ya kuangalia upya suala la ukandamizaji wa jinsia zote. Pia, utafiti wetu utatumika na watafiti wa baadaye katika kuendeleza tafiti zao.

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI

| | | |
|---|---|---|
| **Athari za ukandamizaji** | **:** | Matokeo au hali zinazotokana na tabia, mazoea au matendo hasi ya makundi kandamizi na ambayo hubakia kwa muda baada ya kufikwa na udhalimu. |
| **Itikadi** | **:** | Ni mambo ya jamii au asasi yoyote kama vile ya dini, kisiasa ambayo watu hutarajiwa kuyakubali kuwa ya kweli na kuyaheshimu. |
| **Makundi kandamizi ya watu** : | **:** | Mkusanyiko wa watu wanaowadhalimu watu wengine kihisia, kiafya, kimwili na kisaikolojia. |
| **Mikakati ya ukombozi** | **:** | Mbinu mbalimbali zinazotumiwa na watu kuhakikisha uonevu na ukandamizaji wa jinsia umekomeshwa. |
| **Ukandamizaji** | **:** | Ni aina mbalimbali za maonevu ya kimwili, kihisia na kimawazo yanayotendewa binadamu yeyote katika jamii. Maonevu haya yanaweza kujitokeza katika hali kama vile kuibiwa kupigwa, kuuliwa, kunyimwa chakula miongoni mwa mengine ambayo hukiuka haki za kibinadamu. |
| **Uwezo-Mkuu wa Kiume** | **:** | Ni dhana inayoelezea mwanamume hutazamwa akiwa mbabe, shujaa na mkakamavu kwa misingi ya kibayolojia, rangi ya ngozi, mielekeo, imani na matarajio ya jamii husika. Huhusishwa na uwezo wa mwanaume kuwa na mafanikio ya kutekeleza majukumu yake kama vile kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia bila kushindwa. |

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **I. D. A. S** | : | International Day for Abolition of Slavery |
| **L. H. R.C** | : | Legal and Human Rights Centre |
| **M. R. G** | : | Men’s Rights Movement |
| **UN** | : | United Nations |

## YALIYOMO

UNGAMO ........ ii
TABARUKU ........ iii
SHUKRANI ........ iv
IKISIRI ........ v
MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI ..... vi
VIFUPISHO ........ vii
YALIYOMO ........ viii
**SURA YA KWANZA ........ 1**
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Tatizo la Utafiti ........ 2
1.2 Maswali ya Utafiti ........ 3
1.3 Malengo ya Utafiti ........ 3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........ 3
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 5
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 5
1.6.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Ukandamizaji wa Jinsia ya Kiume ........ 5
1.6 2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mikakati ya Ukombozi wa Jinsia ya Kiume ........ 8
1.6.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Uwezo-Mkuu wa Kiume ........ 9
1.7 Msingi wa Nadharia ........ 11
1.8 Mbinu za Utafiti ........ 14
1.8.1 Uteuzi wa Sampuli ........ 15
1.8.2 Ukusanyaji wa Data ........ 15
1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ........ 16
**SURA YA PILI ........ 17**
**MAKUNDI YA WATU WANAOKANDAMIZA JINSIA YA KIUME KATIKA RIWAYA YA *NJOZI YAPATA MTENZI* NA *NGUU ZA JADI* ........ 17**
2.0 Utangulizi ........ 17
2.1 Ubainishaji wa Makundi ya Watu Yanayokandamiza Jinsia ya Kiume ........ 17
2.1.1 Polisi ........ 17
2.1.2 Wezi ........ 19
2.1.3 Nafsi ........ 22
2.1.4 Mzazi wa Kiume ........ 25
2.1.5 Makahaba ........ 28

2.1.6 Jamii ........................................................................................................ 29
2.1.7 Wanarika wa Kiume .......................................................................................... 31
2.1.8 Wanasiasa ........................................................................................................ 32
2.1.9 Hitimisho ........................................................................................................ 34
**SURA YA TATU ................................................................................................ 35**
**ATHARI ZA UKANDAMIZAJI WA JINSIA YA KIUME KATIKA RIWAYA .......... 35**
**YA *NJOZI YAPATA MTENZI* NA *NGUU ZA JADI* ........................................... 35**
3. 0 Utangulizi ........................................................................................................ 35
3.1 Mmomonyoko wa Maadili ................................................................................. 35
3.2 Msongo wa Mawazo ......................................................................................... 37
3.3 Mauaji .............................................................................................................. 40
3.4 Kupata Malezi Yasiyofaa .................................................................................. 42
3.5 Kukosa Kuendelea na Masomo .......................................................................... 46
3.6 Kukosa Chakula, Mavazi Na Malazi .................................................................. 47
3.7 Ugonjwa Wa Afya ya Kiakili ............................................................................. 48
3.8 Kupoteza Imani na Polisi ................................................................................... 50
3. 9 Kupoteza Kazi ................................................................................................. 51
3. 10 Hitimisho ....................................................................................................... 52
**SURA YA NNE ................................................................................................... 53**
**MIKAKATI AMBAYO WANAUME WANATUMIA KATIKA HARAKATI ZA KUPIGANIA UKOMBOZI WAO KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI: *NJOZI YAPATA MTENZI* (2018) NA *NGUU ZA JADI* (2019) ....................................... 53**
4. 0 Utangulizi ........................................................................................................ 53
4. 1 Mkakati wa Kuikimbilia Dini ............................................................................ 53
4. 2 Mkakati wa Kuwajibika ..................................................................................... 55
4. 3 Mkakati wa Kukomesha Utumwa Wa Kisasa ..................................................... 57
4. 4 Mkakati wa Kutafutiwa Makazi ......................................................................... 58
4. 5 Mkakati wa Kufuata Sheria ............................................................................... 59
4.6 Mkakati wa Kuamua kubadilika kutoka Mui na Kuwa Mwema. ............................ 60
4.7 Mkakati wa Wanaume Kuamua Kushirikiana na Wanawake. ................................ 62
4.8 Hitimisho .......................................................................................................... 65

**SURA YA TANO** ........................................................................................................ **66**
**MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, MCHANGO WA UTAFITI NA MAPENDEKEZO** ........................................................................................................ **66**
5. 0 Utangulizi ........................................................................................................ 66
5. 1 Muhtasari wa Matokeo Ya Utafiti ........................................................................ 66
5.2 Mchango wa Utafiti ........................................................................................ 67
5.3 Mapendekezo ........................................................................................................ 68
**MAREJELEO**……………………………………………………………………………**69**

# SURA YA KWANZA

## 1. 0 Utangulizi

Katika utafiti huu tumechunguza ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah, 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019). Mwanaume ni binadamu wa jinsia ya kiume, ambaye aidha amefikia utu uzima au amebalehe, kabla ya hapo huwa anaitwa mtoto wa kiume tu au mvulana, baada ya kuzaa huitwa kwa kawaida baba na akianza kupata wajukuu anajulikana pia kama babu (Burke, K. 1966: 16). Kwa hivyo wanaume huwa na umuhimu mkubwa katika jamii. Hata hivyo, masuala kuhusu jinsia ya kike yamepigiwa debe sana na masuala kuhusu jinsia ya kiume kusahulika katika harakati hiyo. Tumechunguza iwapo ukandamizaji wa jinsia ya kiume ni matokeo ya jamii kuwasahau au la au ni matokeo ya mfumo wa kuumeni.

Mwelekeo huu umetusaidia katika utafiti wetu ili tuchanganue vitendo vya kikatili vinavyokandamiza jinsia ya kiume katika jamii. Maoni ya Bufacchi, V. (2005: 41) ni kuwa vitendo vya kikatili huhusu matumizi ya nguvu ya kimwili, maneno ya kutisha kwa nia au uwezekano wa kusababisha maumivu, madhara, majeraha au uharibifu kwa mtu au mali yoyote. Aidha, Bufacchi, V. (2005) anaeleza kuwa vitendo vya kikatili vikielekezwa kwa mtu mahususi husababisha mtu mwenye akili timamu kupata hofu au mfadhaiko mkubwa wa kihisia, au kuhofia usalama wao au usalama wa wengine. Kwa hivyo, tumechunguza iwapo kitendo chochote cha kudhuru ambacho kimetendwa kinyume na mapenzi ya mtu kinaweza kuzua ukandamizaji wa jinsia ya kiume. Vilevile, tumechunguza iwapo mitazamo binafsi inaweza kuhalalisha maovu yanayoweza kukandamiza jinsia ya kiume ikakosa kuwa na uamuzi wa mambo ya ndani ya familia, jamii na nchi.

Mathalan, katika kila jamii ulimwenguni kuna wanaume ambao wameathiriwa na vitendo vya kikatili. Mfadhaiko mkubwa wa kihisia, huhusisha mateso makubwa ya kiakili au uchungu ambao unaweza, lakini si lazima, kuhitaji matibabu au matibabu mengine ya kitaalamu au ushauri Bufacchi, V. (2005). Kwa hivyo, tumechunguza iwapo vitendo vingi vya kikatili vimefanywa na makundi ya watu wanaotumia mamlaka yao vibaya. Kadhalika, tumebainisha iwapo vitendo vya kikatili vinaweza vikatangazwa kwa ufasaha au vikabakia siri kama vile dhuluma za kimapenzi.

Hali kadhalika, juhudi za kutetea jinsia ya kiume zinaonekana zimeng’oa nanga katika jamii ya Afrika na ulimwengu mzima ambapo ubabedume umekita mizizi. Kama anavyosema Galla, S. (2020), harakati za haki za wanaume (M. R. G), zilianza nyakati za kukabiliana na

wimbi la pili la ufeministi. Anaeleza kuwa kufikia miaka ya 1980 baadhi ya wanaume walikuwa wakizingatia haja ya kutetea haki za wanaume bila kuwa wahafidhina wa kijamii au kupinga ufeministi. Kulingana naye, baadhi ya masuala muhimu ambayo yaliibuka ni pamoja na malezi ya mtoto wa kiume, wajibu wa malezi ya mwanaume na kukabiliana na unyanyasaji wao. Anadokeza kuwa jinsia ya kiume imethaminiwa na jamii kama kiumbe mwenye staha, mwenye uongozi na uwezo wa kuzalisha mali katika jamii. Suala hili, limetupa taswira mwafaka ya kuchunguza iwapo vizuizi kama vile taasubi ya kiume vikiondolewa visa vinavyomdhulumu mwanaume vitapunguzwa.

Katika utafiti huu, tumeongozwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume ambayo iliasisiwa na Connel, R. (1987) na kuendelezwa na Bly, R. (1990) na baadaye Izugbara (2005) kutafitia utafiti huu. Nadharia hii hufungamanishwa na mahusiano na utendaji wa majukumu ya wanaume kulingana na matarajio ya jamii. Mwanamume huchorwa akiwa na sifa kama vile uwezo, uvumilivu, ushujaa, mkimu familia, kiongozi wa jamii na ujasiri. Vilevile, majukumu ya mwanaume yanaweza kuwa magumu na anaweza kushindwa kutimiza majukumu yake. Kutokana na hali hizi, tumebainisha iwapo ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika jamii unaweza kumdunisha mwanaume na kumfanya awe na hofu, wasiwasi, mwenye shaka na akose heshima katika jamii yoyote yenye mtazamo wa ubabedume.

**1.1 Tatizo la Utafiti**

Katika utafiti huu tumechunguza ukandamizaji wa jinsia ya kiume kama unavyodhihirika katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah, 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019). Mahusiano ya jinsia ya kiume na watu wengine kulingana na desturi na mila za jamii husika huweza kudhihirisha hali halisi za kijamii, kisiasa, kitamaduni na kiuchumi zinazomzunguka mwanaume. Hali hizi zimetupa taswira kamili iwapo ukandamizaji wa jinsia ya kiume ni matokeo ya mahusiano hayo au la.

Tofauti na tatizo la utafiti katika utafiti huu, watafiti wengi kama vile Lugano (1989) na Katola (2006) wanaeleza kuwa ubabedume unapelekea ukandamizaji wa jinsia ya kike duniani. Kulingana nao, wanawake ndio tu hukandamizwa. Kwa hivyo, lazima tutie maanani kwamba mwanaume pia ni binadamu ambaye anaweza kudhulumiwa na kunyanyaswa katika uhalisi wa maisha tunayoishi katika wakati tulio nao. Kwa hivyo, tumechunguza iwapo mwanaume anaweza kukandamizwa akiwa mnyonge katika kudumisha nafasi yake kama kiongozi katika jamii.

Utafiti huu umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume iliyoasisiwa na Connel, R. (1987) na kuendelezwa Bly, R. (1990) na baadaye Izugbara (2005). Nadharia hii imetusaidia katika kujibu maswali ya utafiti na kutimiza malengo ya utafiti yanayotuongoza katika uchunguzi wa suala la ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019).

## 1.2 Maswali ya Utafiti

Maswali yafuatayo yameongoza utafiti huu:

(i) Ni makundi yepi ya watu wanaokandamiza jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019)?

(ii) Jinsia ya kiume imeathirika aje kutokana na ukandamizaji katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019)?

(iii) Ni mikakati ipi inayotumiwa na wanaume kujinasua kutokana na ukandamizaji katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019)?

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo:

(i) Kuchunguza makundi ya watu wanaokandamiza jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019).

(ii) Kubainisha athari za ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019).

(iii) Kuchunguza mikakati ambayo wanaume wanatumia katika harakati za kupigania ukombozi wao katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019).

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Sababu ya kuchagua mada hii ni kuwa kazi ya fasihi ya Kiswahili hasa katika uandishi wa riwaya huzidi kukua na kubadilika na waandishi chipukizi wa riwaya watanufaika zaidi. Kadhalika, tafiti za fasihi ya Kiswahili zitaendelea kuwepo katika maisha ya mwanadamu kwa maana anaendelea kuwepo.

Aidha, sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuwa watafiti wa hapo awali, kulingana na uelewa wetu, hawajashughulikia suala la ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya ya

*Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019). Kwa hivyo, suala la ukandamizaji wa jinsia ya kiume limewekwa wazi katika utafiti huu.

Katika utafiti huu, tunachunguza ukandamizaji wa jinsia ya kiume kwa sababu ni suala ambalo limekuwepo katika jamii nyingi. Kwa hivyo, sababu kuu ni kutaka kujua ni kwa nini waandishi hawa Mbatiah, (2018) na Momanyi, (2019) wameamua kuweka wazi udhalimu wa jinsia ya kiume. Hii ni kinyume na watafiti wengi kama Mnenuka, (2011) na Mavisi, (2007) na wengineo ambao kazi zao zimejikita kuwajadili wanawake kama sehemu ya jamii inayoonewa na kukandamizwa kutokana na mitazamo na tajriba ya kuumeni.

Matokeo ya utafiti huu, yameongeza maarifa ya kiakademia yanayohusu changamoto wanazopitia wanaume na vyanzo mbalimbali vya ukandamizaji wao. Vilevile, chemchemi ya maarifa kwa watafiti na umma imekuwa muhimu katika kuelewa taswira mbalimbali ambazo jamii imewapa wanaume. Pia, nafasi mahsusi walizonazo wanaume katika jamii zao kupitia uwasilishi wa waandishi wa riwaya teule zimebainika. Kwa hivyo, utafiti huu utakuwa muhimu ili kuelewa jinsi wanaume wanavyoathiriwa kama wakimu familia na mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi.  Aidha, tafiti hizi zitabadilika kutokana na mahitaji ya kijinsia ya jamii husika kulingana na nyakati za kihistoria za jamii hiyo. Kwa hivyo, utafiti huu ni muhimu ili kulitekeleza hilo.

Kadhalika, utafiti huu utatumika kama chanzo cha jamii kuliangalia na kulichunguza kwa undani suala la jinsia ya kiume, katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wanawake na wanaume pamoja na kazi nyinginezo za fasihi. Kazi hii, itachangia katika taaluma ya elimu jamii kuwahamasisha kuhusu masuala ya mahusiano mema ya kiuana na usawa wa kijinsia.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuendeleza utumikaji wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume katika utafiti wa suala la ukandamizaji wa jinsia ya kiume. Vilevile, kazi hii itasaidia kupiga msasa harakati za kuwakomboa wanaume kutokana na ubabedume, mila, desturi, na njia zingine zozote zinazowadhalilisha kama zinavyojengwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Hata hivyo, bila kuwabadilisha wanaume na wanawake, mabadiliko ya wanaume wa kisasa hayatapatikana kwa ukamilifu wake. Ni muhimu kuwa nafasi mpya na majukumu mapya ya wanawake yaende sambamba na nafasi mpya na majukumu mapya ya wanaume ili ukandamizaji wa jinsia ya kiume upunguzwe.

Sababu ya kuchagua Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume ni kuwa, imejengeka katika misingi kwamba majukumu na mahusino ya wanaume na wanajamii wengine hutokana na itikadi, mila na desturi na matarajio ya jamii. Kadhalika, sababu nyingine ya kuchagua nadharia hii ni kwamba inajishughulisha na masuala ya kijamii. Vilevile, nadharia hii uhakiki nafasi ya mwanaume katika asasi za kijamii, kisiasa, elimu, na kiuchumi miongoni mwa zingine zinavyoingiliana na kusaidia kujenga jamii imara.

Nadharia hii imetusaidia kuelewa jinsi mwanaume anavyokandamizwa kutokana na matarajio yanayotokana na tamaduni za kijamii alimokulia. Hii inamaanisha kwamba mwanaume hutenda kulingana na matakwa ya mfumo wa jamii yake.

### 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Katika utafiti huu tunachunguza riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019). Kwa hivyo, riwaya hizi mbili zimeteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha juhudi mpya ulimweguni za kuvunja imani na mila potovu zinazopelekea ukandamizaji wa wanaume. Riwaya mbili zimechanguliwa kwa sababu ni za hivi karibuni ili kufanikisha malengo ya utafiti.

Aidha, riwaya hizi tulizozichagua zina mawanda mapana ya kutosha kuwakilisha mtazamo wa mwandishi wa kila riwaya kuhusu suala la mwanaume. Riwaya hizo ziliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha nyakati za kuchapishwa. Kigezo hicho ni muhimu kwa maana mambo hubadilika kulingana na nyakati yaani matendo ya wahusika katika jamii.

### 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Katika sehemu hii, tunalenga kuonyesha tafiti na maandishi ya hapo awali kuhusu ukandamizaji. Vilevile, tunanuia kuonyesha udurusu wa hapo awali kuhusu mikakati ambayo wanaume huchukua ili wajikomboe kutokana na ukandamizaji.

#### 1.6.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Ukandamizaji wa Jinsia ya Kiume

Kulingana na Simon J. na Preger S. M. (1991: 306) katika makala yao, "Ukandamizaji wa Wanaume na Uhusiano Wao na Wanawake," wameeleza kuwa wanaume wamekandamizwa katika jamii kupitia: wazazi, wenzao, taasisi mbalimbali na vyombo vya habari. Wanaume wamekuwa na wajibu wa kuongoza familia na kukimu mahitaji yao. Hivyo, wajibu huu umeweza kukandamiza jinsia ya kiume ili kutimiza matarajio ya jamii ambayo yamezidi kuwanyamazisha. Mawazo haya yametusaidia kuweka wazi uwajibikaji wa wanaume kama

vile kutafutia familia riziki na iwapo hawatatekeleza majukumu hayo ipasavyo huenda wakakandamizwa.

Aidha, Scott (2020) katika tasnifu yake, "Mgogoro wa Kisaikolojia katika Riwaya ya *Mkamadume* na *Unaitwa Nani*?" Mada yake ni tofauti na yetu inayohusu ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* na *Nguu za Jadi*. Pili, Utafiti wake ni tofauti na wetu tukizingatia misingi ya nadharia. Yeye ametumia Nadharia ya Upembuzi nasi tunatumia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Utafiti huu wa Scott umekuwa wa manufaa kwetu kwa sababu tumepata picha ya migogoro ambayo ndiyo misingi mikuu iletayo tofauti zinazochagia ukandamizaji wa jinsia ya kiume.

Vilevile, Masibo (2009) katika kazi yake, "Usawiri wa Wahusika Wanaume na Wahusika Wanawake katika Riwaya za Ngugi wa Thiong'o na Alice Walker," ameonyesha mfumo wa kuumeni katika riwaya za Ngugi wa Thiong'o umewakandamiza wahusika wanaume kwa kupewa nafasi kubwa katika jamii. Katika riwaya za Walker, mhusika mwanamke amepewa nafasi chanya katika jamii. Kulingana na Masibo, Walker amemsawiri mhusika mwanaume kama kiumbe anayehitaji kujinasua kutoka asasi potovu za jamii kama vile za kisiasa, kidini na ubabedume ambao umewakandamiza. Utafiti huu wa Masibo umekuwa muhimu kwetu katika kuonyesha vile ubabedume umechangia katika ukandamizaji wa jinsia ya kiume. Hali kadhalika, utafiti huu wake ni tofauti na wetu kwa sababu utafiti wetu unahusu ukandamizaji wa jinsia ya kiume na wa Masibo ambao unahusu usawiri wa wahusika wanaume na wanawake.

Kadhalika, Badru (2020) katika makala yake, "Mfumo dume-Chanzo cha Ufungwa wa Mwanaume-Uhakiki wa Semi kutoka Jamii za Kiafrika," ameeleza kuwa ubabedume umeweza kupelekea ukandamizaji wa jinsia ya kike katika jamii. Utafiti wa Badru ni tofauti na wetu kwa misingi ya kazi ya fasihi. Yeye ameshughulikia semi lakini sisi tumejishughulisha na riwaya na kujihusisha na masuala ya ukandamizaji wa jinsia ya kiume. Hata hivyo, Utafiti wa Badru umetuwezesha kufahamu vile jinsia ya kiume inavyokandamizwa na mfumo dume katika ugawaji wa majukumu ya kijamii.

Vilevile, Mulila (2009) ameangalia, "Usawiri Chanya wa Wahusika Wanawake katika Tamthilia za *Zilizala* na *Chamchela*." Utafiti wa Mulila ni tofauti na wetu kwa misingi ya fasihi. Yeye amejihusisha na tamthilia na sisi riwaya. Hata hivyo, utafiti wa Mulila ni muhimu katika utafiti wetu hasa katika kuonyesha vile jinsia ya kike imepigiwa debe katika kujinasua kutoka mielekeo ya dhuluma na ukandamizaji kuliko jinsia ya kiume kwani

ameeleza mwanamke wakisasa anafahamu haki zake na amepata nguvu ya kujitetea kutokana na dhuluma za wanaume.

Kwa upande mwingine, Suzana, S. (2015) katika tasnifu yake, "Usawiri wa Mwanamke katika Muziki wa Nyimbo za Dansi," amedai wanawake ingawa huonekana kama viumbe hasi, ni wenye nguvu katika mazingira magumu kama vile mlipuko wa magonjwa kuliko wanaume. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa msingi wa fasihi. Yeye amengalia nyimbo na sisi riwaya. Mawazo haya ya Suzana yametusaidia kuonyesha unyonge unaopata jinsia ya kiume inapokabiliwa na changamoto za maisha ambayo humkandamiza mwanaume.

Vilevile, Opunde (2018) katika tasnifu yake ameangalia, "Uchunguzi wa Masuala ya Kijinsia katika Nyimbo za Daudi Kabaka na John Amutabi Nzenze." Yeye ameangalia nyimbo na sisi riwaya. Utafiti wa Opunde ni wa manufaa kwetu kwa sababu tumepata picha ya vile mwanaume katika jamii ametukuzwa kupitia mila na utamaduni kwa kutwika awe shujaa katika jamii na kutambua kutenda majukumu yake kama vile kumlinda mwanamke na jamii kutokana na vikwazo vya kiusalama, kiuchumi, kitabaka na kielimu mambo ambayo huenda yakamkandamiza iwapo hataimbuka mshindi.

Kadhalika, Wasike (2020) katika makala yake ameangalia, "Mwanamke wa Kisasa katika Insha za Kifasihi Magazetini." Yeye ameshughulikia Insha za Kifasihi Magazetini na sisi tumetumia riwaya. Pia utafiti wake ni tofauti na wetu kwa msingi wa nadharia. Yeye ametumia Nadharia ya Upalizi na sisi tumetumia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Utafiti wa Wasike umetusaidia kueleza umuhimu wa mtagusano wa watu wanapong'ang'ania nafasi za kazi katika jamii huenda kukawakandamiza wanaume.

Zaidi ya hayo, Bayyo (2020) katika tasnifu yake, "Usawiri wa Jinsia ya Kiume katika Riwaya Teule za Shafi Adam Shafi," ameeleza suala la majukumu ya jinsia ya kike na jinsia ya kiume limeendelea kuzua mgogoro miongoni mwa watu. Utafiti huu wa Bayyo ni tofauti na wetu kwa misingi ya waandishi. Yeye ameshughulikia riwaya za Shafi Adam Shafi tofauti na sisi tumeshughulikia riwaya teule ya Mwenda Mbatia na Clara Momanyi. Pili, utafiti wake ni tofauti na wetu kwa misingi ya nadharia. Yeye ametumia Nadharia ya Uhalisia tofauti na sisi tumetumia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Utafiti wa Bayyo umetusaidia katika kueleza mifumo mbalimbali inayoleta migogoro katika jamii na vile imechangia katika ukandamizaji wa jinsia ya kiume inapokabiliwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa.

Vilevile, Kibet, J. O. na Mavisi, R. (2021) katika makala yao, "Taswira ya Mwanamke katika kipindi cha Bi. Msafwari Runinga ya Citizen Nchini Kenya." Utafiti wao ni tofauti na wetu kwa msingi wa mbinu. Wao wametafitia mazungumzo katika televisheni kwa kutazama na kusikiliza na sisi tumesoma riwaya na kuweza kuchambua. Utafiti wa Kibet na Mavisi umetupatia picha ya mtazamo wa wanawake na umuhimu wao katika maisha ya jinsia ya kiume.

Kadhalika, Gwachi (2012) ameangalia, "Migogoro ya Kisaikolojia katika Riwaya ya *Mkamandume na Unaitwa nani?*" Mada yake ni tofauti na yetu kwa sababu yetu inahusu ukandamizaji wa jinsia ya kiume naye ameangalia migogoro ya kisaikolojia katika jinsia ya kiume na kike. Utafiti wa Gwachi umetubainishia suala la utabaka ni mwelekeo wa ukandamizaji unaojikita katika misingi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kuwepo na maoni tofauti ya wahusika yanayoleta ukinzano. Madai haya yametusaidia katika kuonyesha jinsi jinsia ya kiume iliyo na ukwasi na umaskini inavyokandamizwa na wenye nacho na wasio nacho

### 1.6. 2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mikakati ya Ukombozi wa Jinsia ya Kiume

Kulingana na Chachage (2002) katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, suala la ukombozi wa jinsia kutoka minyororo ya kitabaka umejitokeza na bila shaka jinsia ya kiume ni miongoni mwa watu walio katika harakati za kuzinduka. Kwa hivyo, katika utafiti wetu tumeweza kuainisha namna jinsia ya kiume inavyosawiriwa katika harakati za kujikomboa katika nyanja zote kama vile utamaduni, siasa na uchumi.

Aidha, Raymond (2016) ameshughulikia, "Usawiri wa Mwanaume katika Methali za Kimeru Nchini Kenya." Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa misingi ya fasihi. Yeye ameshughulikia methali na sisi riwaya. Pili, Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa misingi ya nadharia. Yeye ametumia Nadharia ya Ubabedume na sisi tumetumia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Utafiti wa Raymond umetupa picha mwafaka kuhusu suala la kukamilika kwa jinsia ya kiume na umoja katika jamii ambayo ni nyenzo kuu inayohitajika ili kuzindua jinsia ya kiume kujikomboa kutoka athari za asasi za kijamii katika masuala kazi na utawala.

Vilevile, Kones (2021) ameshughulikia, "Jinsia Inavyowakilishwa katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa katika Kaunti ya Bomet Nchini Kenya." Utafiti wake umekuwa tofauti na wetu kwa misingi ya fasihi. Yeye ameshughulikia nyimbo na sisi riwaya. Utafiti huu umekuwa na umuhimu kwetu tunachunguza maswala ya kuzinduka kwa jinsia ya kiume kutokana na utamaduni uliopitwa na wakati miongoni mwa mambo mengine.

Kadhalika, Rwegira (2017) ameshughulikia, “Ujinsia katika Methali za Wakurya.” Utafiti wa Rwegira ni tofauti na wetu kwa misingi ya mada. Yeye ameangalia mada inayohusu ujinsia katika methali, ilhali mada yetu inahusu ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya *Nguu za Jadi* (2019) na *Njozi Yapata Mtenzi* (2018). Pili, utafiti wake ni tofauti kwa msingi wa fasihi. Yeye ameshughulikia methali na sisi riwaya. Utafiti wa Rwegira umetusaidia kupata picha ya vile mila na desturi kupitia mahusiano ya wanaume na wanawake zimechangia matarajio ya jamii na kuishi bila mkinzano. Mawazo haya ya Rwegira yamekuwa ya manufaa kwetu katika kuonyesha jinsia ya kiume sio kandamizi na inatetea ukombozi wake kutokana na madhalimu.

### 1.6.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Uwezo-Mkuu wa Kiume

Marejeo yanayohusu Uwezo-Mkuu wa Kiume yamechambuliwa ili kubaini jinsi watafiti na wataalamu walivyouchambua usawiri huo kwa mikabala mbalimbali. Katika sehemu hii tumeshughulikia baadhi ya watafiti na watalaamu hao.

Kulingana na Osore (2008) katika tasnifu yake alifanya utafiti kuhusu, “Kinaya katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed.” Anaeleza kuwa wanaume huchukuliwa kuwa, ‘Kichwa cha familia.’ Ili kutimiza haya, walijihusisha na kilimo na uvuvi. Majukumu ya wanawake yalikuwa ya kufagia boma, kupika, kuosha vyombo na nguo na kufuma mikeka. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu unashughulikia maudhui ya kinaya kwa kutumia Nadharia ya Tahakiki Usemi huku utafiti wetu ukitumia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Matokeo ya utafiti wa Osore yalitufaa kuangalia vile hadhi ya wanaume hushushwa hadhi kama kiongozi wa nyumba wanapokosa uwezo wa kiuchumi.

Kadhalika, Kibigo (2019) katika tasnifu yake, “Ubabedume katika Majigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo Miongoni mwa Waisukha Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Kisemantiki,” anakubaliana na Osore (2008). Anaeleza kuwa Uwezo-Mkuu wa Kiume huhusishwa na misingi ya kibaiolojia ya mwanamume, mielekeo, imani, na matarajio ya jamii husika ambayo huzaliwa na kukuzwa na utamaduni wa jamii hiyo. Kupitia maelezo yake tunapata ufahamu kuwa mwanaume hutenda mambo yake na majukumu yake kwa kuzingatia umbile wake na uwezo wake wa kukidhi majukumu kulingana na mkakati unaokubalika na jamii yake. Matokeo ya utafiti wa Kibigo (2019) ni kuwa ingawa kuna tofauti katika maumbile ya jinsia tofauti kama vile nguvu za kimwili na kuwa na misuli huwapa nguvu nyingi kuliko wanawake. Maoni haya yamechangia katika kuendeleza utafiti huu iwapo mwanaume atashindwa kudhihirisha nguvu zake huenda akakandamizwa na watu

wengine kama vile wanawake au wanaume wenzake. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa sababu ametumia nadharia mbili tofauti na sisi ambao tumetumia nadharia moja. Utafiti wake ulishughulikia suala la jinsia ya kiume kama vile wetu ingawa mada zilizoshughulikiwa ni tofauti.

Vilevile, Mutungi (2008) katika tasnifu yake, "Usawiri wa Wahusika wa Kiume Kama Kielelezo cha Udume," anaeleza kuwa Uwezo-Mkuu wa Kiume hutokana na mila, desturi na utamaduni wa jamii zenye mfumo-dume. Anaeleza kuwa mwanaume hupewa nafasi chanya, mamlaka ya kutawala, kulipa mahari, watoto kumili jina lao, kulinda familia na wengine ambao wanatarajiwa kuwaheshimu. Utafiti huu umetusaidia kudhihirisha kuwa kuna baadhi ya wanaume walio na mamlaka au nguvu nyingi wanawakandamiza wanaume wasio wababe. Kadhalika, utafiti huu wa Mutungi (2008) umetusaidia kuonyesha kuna baadhi ya wanaume wanatumia ubabe wao kwa njia chanya kukomesha mila na desturi zilizopitwa na wakati zinazopelekea ukandamizaji wa wanaume. Kazi hii imemsaidia mtafiti kubaini masuala ya kitamaduni ambayo yanauendekeza mfumo dume na kuwanyanyasa wanaume.

Aidha, Izugbara, C. (2019) ameshughulikia, "Wanaume wenye Kutamani Miongoni mwa Vijana Maskini wa Mijini Nchini Kenya." Ameeleza kuwa vijana wa kiume katika mji mkuu wa Nairobi, katika vitongoji vyao, Uwezo-Mkuu wa Kiume, mamlaka na ubabe 'sahihi' unajumuishwa katika suala la jadi la ndoa, ugumu wa kutafuta riziki na kujitegemea. Anaeleza kuwa vijana hao hutamani uwezo wenye sifa ya mtafuta riziki 'mvumilivu', anayejali, mwenye hisia chanya katika uhusiano wowote na jamii yake na kukataa vurugu. Hata hivyo, anaeleza kuwa matarajio ya wavulana maskini wa Nairobi ni magumu; yaliyoundwa katika makutano ya vikwazo vya kimuundo na miradi ya mawakala kwa maisha bora. Matarajio haya yanawekewa mipaka na yanaakisi hali ya lengo la kila siku na kustahimili ukosefu wa usawa. Hali hii huashiria hamu kubwa isiyofikiwa ya mabadiliko chanya ya kijamii na kimaisha.

Kadhalika, mchango wa Glenn, E. N. (2002) katika kitabu chake, Uhuru Usio na Usawa (*Unequal Freedom*) unahusu utambulisho wa wanaume kwa misingi ya rangi ya ngozi. Anaeleza kuwa, wanaume weupe katika Ulaya iliyoendelea kiviwanda na Amerika ya Kaskazini wana thamani kubwa kuliko wanaume wenye rangi ya ngozi nyeusi. Anasema jamii imeidhinisha nafasi yao wenyewe kama bora kuliko wanaume wasiokuwa weupe, walio na rasilimali kidogo au wasio na mali. Suala hili limetupa taswira ya ukandamizaji wa jinsia

ya kiume kwa misingi ya rangi inayoweza kuwaweka katika hatari ya kudhulimiwa na wanajamii wengine.

Zaidi ya hayo, Bly, R. (1990) anadai kuwa, kuna ulemavu wa maisha ya wanaume wanapokuwa katika harakati ya kudumisha Uwezo-Mkuu wa Kiume katika jamii. Anaeleza kwamba, karibu katika tamaduni zote wavulana huchukuliwa kutoka kwa wazazi wao na kuanzishwa kimakusudi kuwa mwanaume na wanaume wazee wa jamii. Kuna wanaume hupata majukumu ambayo yanajumuisha anuwai kamili ya uzoefu wa ndani wa wanaume. Kulingana naye, mzazi wa kiume hawezi mwenyewe kuwa mwanzilishi. Inakuwa "ni hali ya wasiwasi sana; baada ya yote baba na mtoto wa kiume huwa wanampenda mwanamke mmoja". Hata hivyo, katika jamii za "jadi" (kwa kukosa neno bora zaidi) akina baba wana jukumu muhimu la kutekeleza, kama walinzi na waelimishaji wa watoto wao. Bado katika tamaduni za sasa, akina baba wanashindwa hata katika jukumu hili lenye ukomo zaidi. Si kwamba ni kushindwa binafsi bali ni suala la lawama za kibinafsi na mapungufu ya mtu binafsi.

Scanzoni (1979) katika makala yake, "Mikakati ya kubadilisha Majukumu ya Wanaume," anaeleza kuwa Uwezo-Mkuu wa Kiume huelezwa kwa kuangazia hatua tatu ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuleta mabadiliko katika majukumu ya familia ya mwanaume. Hatua ya kwanza aliita uungwana ambapo mwanaume hutenda mambo kwa manufaa ya wengine. Mwanaume anabadili majukumu yake kwa sababu ni haki, adilifu na sahihi. Anaeleza kuwa mwanaume aliye na Uwezo-Mkuu wa Kiume chanya hushiriki katika majukumu ili kuleta ufanisi wake na katika familia yake. Hatua ya pili ni mbinu ya upendeleo au ubinafsi. Katika hatua hii wanaume hubadili majukumu yao kwa sababu watafaidika kutokana na mabadiliko hayo. Hatua ya tatu ni kupitia majadiliano na ushirikiano. Kwenye hatua hii, mwanaume na mwanamke hujadiliana kuhusu mabadiliko katika majukumu yao. Utafiti wa Scanzoni unatofautiana na wetu kwa kuwa, wake unatambua mbinu za kuyabadilisha majukumu ya familia ya mwanaume huku wetu ukihusu ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019). Utafiti wake umetusaidia kuchunguza mikakati ambayo wanaume hutumia katika harakati za kupigania ukombozi wao.

## 1.7 Msingi wa Nadharia

Katika utafiti huu, tumeongozwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume iliyoasisiwa na Connel. R. (1987) na kuendelezwa na Bly, R. (1990) na baadaye Izugbara, C. (2005).

Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume hujikita katika vigezo vitatu: Mwanaume ni mbabe kwa misingi ya kimaumbile, rangi nyeupe ya ngozi na kibayolojia, mwanaume ni mtekelezaji wa majukumu kulingana na mila, itikadi na matarajio ya jamii na mwanaume mpya asiye na udikiteta taasubi ya kiume.

Aidha, kulingana na Bly, R. (1990), Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume hueleza wanaume wenye rangi nyeupe ya ngozi huwa na pesa, thamani kubwa na hushikilia nafasi chanya katika jamii kuliko wanaume wenye rangi nyeusi ya ngozi. Vilevile, nadharia hii inajikita katika maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume. Dhima kuu ya nadharia hii huwania kuhalalisha desturi za jinsia ya kiume, ubabedume na mabadiliko ya mwanaume mpya anayetumia ubabe wake kwa kuwajali wengine.

Vilevile, Bly, R. (1990) anasema kuwa, kichocheo cha vuguvugu la wanaume kilitokana na uhakiki wa jinsia ya kiume na utawala wa wanaume unaoathiri kila sehemu ya jinsia ya kike pamoja na mageuzi ya miaka ya 1960. Huu ulikuwa wakati wa upeo wa mgogoro wa itikadi za kijamii katika nchi za Marekani ambazo zilihitaji kuzingatia upya majukumu ya kijinsia. Mgogoro huu ulihusu nafasi na majukumu ya kijinsia katika jamii.

Kama anavyosema Connel. R. (1987), Nadharia ya Uwezo–Mkuu wa Kiume imejengeka katika misingi kwamba majukumu, mahusiano, matendo, malezi, tabia na kutangamana kwa wanaume na wanajamii wengine hutokana na itikadi, utamaduni, mila na desturi na matarajio ya jamii husika. Kwa hivyo, Nadharia ya uwezo-Mkuu wa Kiume huonyesha ubabe wa wanaume na imebainisha wanaume wamepewa mamlaka zaidi katika jamii. Wanaume wengi wanashikilia nafasi muhimu na kubwa katika asasi mbalimbali kama vile za kiserikali, kisiasa, kidini na kielimu na kiuchumi.

Vilevile, nadharia hii humtazama mwanamume kama mkimu familia, kiongozi, mkakamavu, shujaa, na jasiri asiye na asiyeshindwa na jambo lolote. Hata hivyo, maoni ya Bly, R. (1990) ni kuwa, wanaume ambao hushindwa kudhihirisha sifa hizi zilizowekwa kulingana na matarajio ya jamii, wanatazamwa kama wapotovu na wasio wanaume kamili.

Aidha, Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, hutenganisha majukumu ya wanaume na wanawake kama watendaji wa kijamii. Upambanuzi wa kimuundo ni hitaji la jamii, na mgawanyiko wa kazi ndani ya familia kati ya wanaume na wanawake ni muhimu katika jamii. Wavulana hufundishwa ndani ya familia, vikundi rika, shule, na mashirika na taasisi nyingine za kijamii tabia na tabia zinazochukuliwa kuwa zinafaa kwa wavulana na

wanaume. Wavulana huweka ndani tabia 'zinazofaa' kwa jinsia mahususi. Uwezo-Mkuu wa Kiume huwa ni utambulisho unaowiana na nafasi ya mwanamume katika miundo ya jamii.

Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume hueleza asasi za kijamii hubadilika katika vipindi tofauti vya kihistoria katika muktadha wa kijamii. Vivyo hivyo, ndivyo Uwezo-Mkuu wa Kiume hubadilika. Kwa upande mwingine, Bly, R. (1990) anaeleza kuwa, wimbi la pili la fikra za ufeministi linashughulikia dhana ya Uwezo-Mkuu wa Kiume kama taasisi ambayo imekumbwa na mawimbi na inayumbayumba. Anajiuliza iwapo Uwezo-Mkuu wa Kiume ni tatizo la siasa za kijinsia au ikiwa shida sio ya kijinsia bali ipo katika mipango ya kikatiba inayozalisha ukosefu wa usawa wa kijisia. Anaamini kuwa Uwezo-Mkuu wa Kiume ni suala la mahusiano ya kuheshimiana kati ya mtu binafsi na ya kijamii.

Hata hivyo, Izugbara, C. (2005), anaeleza kuwa wanaume ambao kwa muonekano ni wapole sana ila wanatawaliwa na mfumo dume. Kwa maana hiyo, jamii ina wanaume mchanganyiko wakiwemo wanaume wapya yaani walioondokana na mfumo dume na ambao wanaushikilia. Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume inalenga kuwaonesha wanaume wapya ambao wamebadilika na kuwa katika utendaji mpya ikilinganishwa na mfumo uliotekelezwa na wanaume awali.

Kwa upande mwingine, Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume ina mihimili kadhaa. Mihimili mitano, kama ifuatayo imetufaa katika utafiti huu. Katika mhimili wa kwanza, Connel, R. (1987) anaeleza kwamba fikra za wanajamii humtazama mwanaume kama mwenye hadhi ya juu kuliko mwanamke. Anaendelea kudai kuwa fikra hizi huongozwa na itikadi, mila na desturi za jamii husika na hutambulika katika historia ya jamii yake. Kulingana na Bly, R. (1990), wanaume wa rangi ya ngozi mbalimbali wamepinga desturi na imani zinazojengwa kuhusu wanaume weupe. Anaeleza kuwa wanaume wa rangi ya ngozi nyeusi hutazamwa na jamii kama duni kuliko wanaume wa rangi ya ngozi nyeupe.

Mhimili wa pili wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume unadai kwamba, majukumu ya binadamu yeyote hugawanywa kwa misingi ya kijinsia. Mwanaume huwa na majukumu tofauti na ya mwanamke. Kulingana na Sherman na Wood (1982: 137), mafundisho ya majukumu ya wanawake na wanaume katika misingi ya uana huanzia katika kiwango cha familia. Kwa hivyo, nadharia hii humchora mwanamume kama mkimu jamii anayepaswa kukidhi mahhitaji ya jamii yake ya chakula, mavazi na malazi.

Mhimili wa tatu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume ni kwamba, mwanaume huwa na sifa angama kama vile: ni mbabe, mtafuta riziki, mkimu familia, jasiri, mwenye pesa na

mkakamavu. Sifa angama za mwanamume hutokana na misingi ya kibayolojia ya mwanamume pamoja na mielekeo, imani na matarajio jamii husika Connel, R. (1987:150). Mhimili huu umetusaidia kuelewa maana kuu zinazohusishwa na Uwezo-Mkuu wa Kiume umeegemezwa kwenye itikadi na ishara zinazowaweka wanawake kama dhaifu ikilinganishwa na wanaume.

Mhimili wa nne kwa mujibu wa Wells na Holland (2001) ni kwamba, jamii huundwa na makundi ya watu mbalimbali. Kwa mujibu wa Msanjila na wenzake (2011), wanaeleza kwamba jamii huundwa na matabaka na makundi mbalimbali ya watu. Kwa mfano, kuna matabaka ya watawala na watawaliwa, wakulima na wasio wakulima, wafanyakazi wa kuajiriwa na wasio wa kuajiriwa. Vilevile, kuna waliosoma na wasiosoma, wafanyabiashara na wasio wafanyabiashara na kadhalika. Pia, kuna makundi ya vijana, wazee, wanawake, wanaume, wanafunzi, wanachuo, wanamichezo, wanajeshi, walimu na kadhalika. Kwa hivyo, mhimili huu umetusaida kuelewa mahusiano ya wanaume na wanajamii wengine yanayoweza kuwakandamiza au wasikandamizwe.

Mhimili wa tano Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume unadhihirisha jamii hubadilika kila wakati. Kwa mujibu wa Connel, R. (2005) ni kwamba, tabia, mtazamo na maadili ya wanaume kwa kipindi kirefu hubadilika. Hii ni kwa sababu ya itikadi za kijamii na viwango hubadilika kadiri muda unavyopita na hutofautiana kulingana na muktadha wa kijamii. Pia mtazamo wa jamii kumhusu mwanamume hubadilika. Hii ni kwa sababu miili na akili ya wanaume hubadilika katika kipindi cha maisha ya mwanadamu. Mhimili huu umetusaidia kubainisha iwapo mabadiliko haya hutokea katika asasi za kijamii kama vile elimu, siasa, na kiuchumi. Vilevile, mhimili huu umetusaidia kuzua mwamko mpya wa wanaume kutafakari upya hali yao katika jamii. Hali hii inaonyesha wanaume wamo mbioni kujikomboa kutokana na mifumo ya kitamaduni na mahusiano yao na wanajamii wengine.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Ili kufanikisha malengo ya utafiti ni lazima mtafiti akusanye data zinazowezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Kulingana na Kabir, (2016), mbinu za utafiti ni mwongozo uliopangwa kufuatwa katika kukusanya na kuchambua data ili kujibu maswali ya utafiti husika. Sehemu hii iliainisha mbinu mbalimbali ambazo zilitumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data ili kujibu maswali ya utafiti kama ifuatavyo:

### 1.8.1 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ni utaratibu anaoutumia mtafiti kupata idadi ya watoa taarifa (sampuli) kutoka katika idadi ya watu lengwa wa utafiti (Kabir, 2016). Katika kupata sampuli ya kufanyia utafiti, mtafiti ametumia sampuli ya kimaksudi ambapo mtafiti ameweza kupata data kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

Aidha, Rimando, W. (2015), anaeleza kwamba ni vigumu kwa mtafiti kushughulikia idadi kubwa ya wanajamii inayohusika katika utafiti wake hata kama anavutiwa na idadi hiyo ya vitafitiwa. Hivyo basi, mtafiti hulazimika kuchagua au kuteua idadi maalumu ya watafitiwa/vitafitiwa ya kushughulikia katika utafiti wake. Idadi hiyo maalumu huitwa watafitiwa lengwa/vitafutiwa lengwa. Hivyo basi, vitafitiwa lengwa katika utafiti huu ni riwaya mbili ambazo ni: *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019). Riwaya hizi mbili ziliteuliwa kama sampuli inayowakilisha nyingine kwa sababu zililenga suala la wanaume kikamilifu.

Kadhalika, mtafiti alilenga kutafiti kazi zilizoandikwa miaka ya hivi karibuni yaani mwaka wa 2018 na 2019. Hii ndiyo sababu mtafiti alijikita katika riwaya teule maana zilionekana zinakidhi vigezo vya wanaume kulingana na mada ya utafiti. Mtafiti amezingatia matukio yaliyofanywa na wahusika wa kiume katika hizi riwaya ili kuweza kuchunguza namna waandishi walivyoonyesha ukandamizaji wa wanaume.

### 1.8.2 Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alisoma vitabu, makala na tasnifu mbalimbali zilizoandikwa na wataalamu na watafiti mbalimbali. Upekuzi wa majarida na vitabu mbalimbali maktabani ulimwezesha mtafiti kufichua maoni na mawazo ya watafiti wengine kuhusiana na masuala ya wanaume pamoja na kukadiria nadharia iliyofaa kuongoza utafiti huu. Mtafiti pia, alidondoa na kuainisha makundi mbalimbali ya watu ambao wanakandamiza wanaume kama walivyosawiriwa na mwandishi Mbatiah (2018) na Momanyi (2019) katika kila riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* na *Nguu za Jadi* mtawalia.

Mtafiti alisoma riwaya mbili zilizoteuliwa pamoja na vitabu vya maelezo kuhusu nadharia. Vilevile, upekuzi ulitumika kutafuta makala katika maktaba na kwenye mtandao wa tovuti kuhusu nadharia na ukandamizaji wa wanaume katika fasihi. Kadhalika, udurusu ulitumika katika kutafuta yale yaliyokuwa yameandikwa kuhusu: Ukandamizaji wa mwanaume na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume na wataalamu mbalimbali. Aidha, mtafiti alitumia

uandishi kama kifaa cha kumwezesha kuyanakili yale yote ambayo yameandikwa katika utafiti huu. Baada ya kukusanya data, ilipangwa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti.

### 1.8.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Uchanganuzi wa data iliyotokana na uchambuzi wa riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na *Nguu za Jadi* (2019) pamoja na maandiko yaliyochangia kuimarisha utafiti huu, yalichunguzwa kulingana na malengo ya utafiti. Data hiyo ilichanganuliwa kuainisha makundi ya watu wanaokandamiza jinsia ya kiume kutoka katika kila riwaya. Kwa kiwango kikubwa, kigezo cha kuamulia athari ambazo wanaume hupata kutokana na ukandamizaji zilitegemea tathmini na ukadiriaji wa mtafiti. Awamu ya mwisho ilikuwa ni mikakati ambayo wanaume hutumia kujinasua kutoka ukandamizaji.

Maelezo yametumiwa kuweka bayana na kushadidia yale yaliyojitokeza kwenye riwaya teule. Kila mhimili wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume umetumiwa katika ufafanuzi wa data kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Mkabala wa maelezo unaelezwa na Kabir (2016), kuwa ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo haihusishi mahesabu bali maelezo tu ndio hutolewa huhusiana na data za utafiti zilizokusanywa. Matokeo yaliwasilishwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti kwa namna data zake zilivyokusanywa. Njia hii humwezesha mtafiti kurahisisha uwasilishaji wa matokeo na kwa kutumia muda mfupi katika kukamilisha malengo ya utafiti.

Baada ya data kukusanywa na kuchanganuliwa mtafiti amewasilisha matokeo ya utafiti kwa umma kwa njia ya maelezo na kutolea mifano mwafaka inayoafikiana na mada ili yatumiwe kuelewa na kuendeleza maarifa kuhusiana na mada ya utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAKUNDI YA WATU WANAOKANDAMIZA JINSIA YA KIUME KATIKA RIWAYA YA *NJOZI YAPATA MTENZI* (2018) NA *NGUU ZA JADI* (2019)

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunachunguza makundi ya watu wanaohusika na ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah, 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019). Utambuzi huu umetusaidia kutambua makundi ya watu wanaokandamiza jinsia ya kiume wanapotangamana na wanajamii wengine katika riwaya teule. Tumeongozwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume kwamba jamii huundwa na makundi mbalimbali.

Sura hii inahusu uchanganuzi wa makundi ya watu wanaokandamiza jinsia ya kiume katika riwaya *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah, 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019). Maoni ya Msanjila na wenzake (2011) ni kuwa, jamii imegawanyika katika makundi kadhaa ya watu. Kwa mfano, kuna makundi ya watawala na watawaliwa, wakulima na wasio wakulima, wafanyakazi wa kuajiriwa na wasio wa kuajiriwa. Vilevile, kuna waliosoma na wasiosoma, wafanyabiashara na wasio wafanyabiashara na kadhalika. Pia, kuna makundi ya vijana, wazee, wanawake, wanaume, polisi, wanasiasa, makahaba na madaktari miongoni mwa makundi mengine.

## 2.1 Ubainishaji wa Makundi ya Watu Yanayokandamiza Jinsia ya Kiume

Kwa mujibu wa Simon, J. na Preger, S. M. (1991), wanaume hawakandamizwi tu na wanawake bali hukandamizwa na jamii kwa ujumla kupitia kwa: wazazi, wanaume wenzao, taasisi mbalimbali, vyombo vya habari na wanarika wenzao. Taswira hii inaonyesha kuwa jinsia ya kiume imetanzwa na matatizo, imekandamizwa na makundi ya watu na haijapewa hadhi inayostahili katika jamii kama inavyoonekana kwenye sura hii.

### 2.1.1 Polisi

Polisi ni jina linalotumiwa kurejelea mtumishi wa umma ambaye kazi yake ni kulinda, kupunguza vurugu na kudumisha usalama. (Tafsiri yetu). Hata hivyo, kuna baadhi ya maofisa wa polisi ambao hukosa kutekeleza wajibu wao wa kushika doria, kuwakamata wahalifu na kutochukua hatua kwa waliotenda maovu.

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi,* (Mbatiah 2018: 20), kuna baadhi ya wanaume kama vile Shukri ambao hawapati usaidizi kutoka kwa polisi wanaporipoti visa vya uhalifu vilivyotokea. Inabainika kuwa polisi hao wanafeli kuwajibikia kazi ya kulinda usalama, mali ya watu na kukosa kukabiliana na wahalifu. Maelezo haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Haikuwa mara ya kwanza ya Shukri kutangamana na polisi. Alikuwa ameripoti uhalifu aliotendewa mara kadha. Mwaka jana, nyumba yake ilivunjwa usiku, vyombo vyote vya kielektroniki vikatwaliwa. **Alipiga ripoti kwenye Kituo cha Polisi cha Mtoni. Akaahidiwa kwamba uchunguzi ungefanywa lakini hakuna lolote lililowahi kufanyika.** Polisi hawakusaidia lolote. Kila mara alitoa taarifa kwa polisi, lakini hakuwahi kusikia kwamba wanyang'anyi wamekamatwa. (Mbatiah 2018: 20)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 20), polisi wamemkandamiza Shukri kwa kumnyima haki ya kulindwa, yeye pamoja na mali yake. Wameenda kinyume na haki za binadamu za kutojali. Polisi hao hawaonekani wakifanya upelelezi wa kina kuwakamata wahalifu waliomuhangaisha Shukri. Ingawa Shukri alikuwa mfanyibiashara maarufu na mbabe katika sekta ya kibiashara. Jambo hili linashusha ubabe wake kama mwanamume. Wazo hili linaungwa mkono na wataalamu mbalimbali wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume akiwemo Connel, (1987). Anaeleza kuwa si kila mwanaume mbabe katika jamii anafaidika na ubabe huo.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi,* (Mbatiah: 2018), kuna maofisa wa polisi wa jinsia ya kiume wanaotumia madaraka yao kuwakandamiza wanaume wengine. Kiguto anakumbuka kisa ambapo alichukulia kwamba Mark Bagite ambaye ni ofisa wa polisi ameenda kuwakamata wahalifu waliomuua tajiri mwenye *rangerover.* Kumbe Mark Bagite alienda kuwinda ngawira! Hakushughulika hata kuripoti mauaji yaliyotokea. Alipomsimulia hadithi nzima siku chache baadaye, Kiguto alijicheka mwenyewe kwa ujinga wake. Kwa

ufupi, Mark Bagite aliwaua wezi waliomnyang'anya mwenzao ngawira, akajipatia milioni tatu kimuujiza. Haya yanabainika katika katika mfano ufuatao:

> Kiguto alikumbuka kile kisa cha majuzi ambapo alichukulia kwamba **Mark Bagite ameenda kuwakamata wahalifu waliomuua tajiri mwenye *rangerover*. Kumbe mzee huyo alienda kuwinda ngawira! Hakushughulika hata kuripoti mauaji yaliyotokea.** (Mbatiah 2018: 37)

Kutokana na nukuu katika Mbatiah (2018: 37), Mark Bagite anajikandamiza kwa kuongozwa na tamaa ya kupata utajiri haraka kwa njia haramu. Kiguto anashangazwa na jinsi Mark Bagite ambaye ni ofisa wa polisi mwandamizi anakuwa ni mhalifu na muuaji. Ukatili wake unamsawiri kama ofisa wa polisi aliyepuuza wajibu wake wa kumaliza uhalifu. Badala yake, anaendeleza uovu kwa kutumia madaraka yake vibaya. Tabia hii ya Meja Bagite kutumia mamlaka yake vibaya na kuficha uovu, inasadifiana na Uwezo-Mkuu wa Kiume. Kwa mujibu wa Bly, R. (1990), baadhi ya wanaume hutumia mamlaka yao kudhihirisha ubabe wao. Jambo hili linaonyesha kuwa Mark Bagite ni polisi mbinafsi anayesukumwa na tamaa ya kutajirika haraka.

### 2.1.2 Wezi

Mwizi ni mtu anayechukua kwa siri, kinyume cha sheria na kwa uhalifu mali ya mtu mwingine kwa faragha; dhuluma, kwa kudanganya na kulaghai kwa ujeuri au ukatili Bufacchi, V. (2005). Mara nyingi, wezi hao huchochewa kuiba na makundi ya wanarika, tamaa au uhusiano na wezi wengine. Tukiangalia takwimu katika, ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (L.H.R.C, 2019) kuhusu wanawake na mfumo wa haki ya jinai, ni wazi kwamba kati ya takribani idadi sawa ya wanaume na wanawake, 85% ya watu waliofanya uhalifu walikuwa wanaume na takriban 75% walikuwa wanawake. Takwimu hizi zinaonyesha wahalifu kuwa wanaume walifanya uhalifu zaidi kuliko wanawake. Haya yanaungwa mkono na Dabbs, J. na Morris, R. (1990), ambao walifanya utafiti mwaka wa 1990 kuhusu, uhusiano kati ya viwango vya *testosterone* na tabia zisizo za kijamii. Walifanya utafiti wa zaidi ya wanaume 4400 na kugundua kuwa, wanaume walio na viwango vya juu vya *testosterone* walikuwa na maswala ya matumizi mabaya ya uhalifu (Dabbs, J. na Morris, R. 1990).

Aidha, mwanasosholojia wa Marekani Sutherland, E. H. (1960), anaeleza kwamba tabia ya kuwafundisha wavulana kuwa 'wakali na wagumu' huwafanya wajihusishe na tabia potovu. Sutherland anadai kwamba, tangu majukumu na maadili ya kiume yalipoanza kukita mizizi kwa wavulana wakati wa ujana, walijihusisha na tabia ya uasi na ukaidi kuliko wasichana. Vilevile, wavulana wachanga katika magenge hujifunza sifa muhimu za utambulisho dhabiti wa kiume, kwa mfano utawala na ukakamavu**,** kutoka kwa washiriki wengine wa kiume wazima (Cloward na Ohlin, 1960).

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah, 2018), wavulana Kim na Dan wa shule ya upili ya wavulana ya Madaraka, walipomaliza masomo yao saa kumi walitakiwa kufika nyumbani lakini badala yake walielekea barararabara ya Mkomani kwenye kioski kilichomilikiwa na wezi sugu, Okuti na Nyangwe. Humo walitangamana na wezi hao na kujihusisha na vitu vya wizi kama vile simu ya Shukri waliyopewa na Okuti na Nyangwe wauze. Maelezo haya yanasadifiana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Jukumu la mwanaume katika jamii ni kuwa muamuzi anayefaa kufanya na kupata chochote anachotaka. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi katika mfano ufuatao:

> Simu nzuri zaidi, Kiguto alisema huku akimrudishia Kim simu. '**Ulitoa wapi hii simu? "Okuti na Nyangwe wa-li-ni-a-chi-a ni-wa-u-zi-e." Kim na Dan waligugumia**. (Mbatiah 2018:42)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 42), visa vya wezi wa jinsia ya kiume kuwahusisha wavulana wa shule kuendeleza wizi ili wakidhi mahitaji yao vimekithiri. Sifa hii inawafanya wezi sugu, wahusika Okuti na Nyangwe wawatumie wavulana wa shule ya kutwa ya Madaraka, Kim na Dan kama chombo cha kuimarisha mitandao yao ya wizi. Inabainika kuwa wavulana hawa badala ya kujihusisha na mambo yanayokinga usalama wao na elimu itakayokuwa nuru ya maisha yao, wamejishughulisha na wizi unaowanyima nafasi ya kuendelea na masomo yao. Hali hii inadhihirisha mwanamume hana mtu wa kumuongoza na kumwelekeza awe na mienendo mizuri. Baadhi ya wanasosholojia wanaotetea haki za wanawake wanadai kuwa, nafasi ya kando ya wanawake katika jamii za mfumo dume ndiyo sababu kuu ya wanaume kufanya uhalifu zaidi (Sutherland, E. H. 1990). Anaeleza kuwa wanawake wanadhibitiwa zaidi kuliko wanaume. Vilevile, anaeleza kuwa, majukumu na tabia za kijinsia za kawaida ziliwekwa alama wakati ujamaa uliwapa wanaume uhuru zaidi wa kibinafsi kuliko wanawake. Wanaume wanaweza kukaa nje kwa masaa ya baadaye wasiwe chini ya uangalizi mkali.

Vilevile, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi,* (Mbatiah 2018: 21), visa vya wezi kuwaibia wanaume wa jamii ya Wahindi vimezidi mno. Wezi sugu Okuti na Nyangwe wanasema kuwa "**umaskini ulikuwa sifa ya Kiafrika tangu uhuru. Ilikuwa Muhali kumpata Mhindi maskini".** Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, inaeleza kuwa wanaume wenye rangi nyeupe ya ngozi huwa na pesa, thamani kubwa na hushikilia nafasi chanya katika jamii kuliko wanaume wenye rangi nyeusi ya ngozi. Shukri ambaye alikuwa wa jamii ya Kihindi aliathirika zaidi na uhalifu. Wezi walimuandama kwa sababu ya imani iliyotawala kwamba Wahindi walikuwa na pesa nyingi. Imani hii ilitokana na ukweli kwamba walidhibiti pesa nyingi, biashara kubwakubwa. Vilevile, inaaminika aliendesha magari ya kifahari na kuishi katika mitaa ya matajiri. Muonekano wa kuwa yeye ni tajiri, kulimuweka Shukri katika hatari ya kunyanyaswa na wezi waliowania kuchuna pesa kutoka kwake.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi,* (Mbatiah 2018: 11), kuna wezi wa jinsia ya kiume wanapatwa na tamaa ya pesa kama vile Okuti baada ya kukamilisha kitendo cha wizi. Wezi hawa wanawauwa wezi wanaume wenzao ili wapate pesa nyingi. Mmoja wa wezi anasikika akisema: **"Wameniua! Mungu mmoja na pesa wamechukua. Zote milioni tatu hawakutaka tugawane".** Wezi hawa wanaonekana wakitorokea mahame ya jumba lililochomeka miezi kadha iliyopita wanaonekana vizuri. Ukandamizaji unaojitokeza hapa, unaafikiana na mhimili wa tatu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume unaosema wanaume ni wababe. Jambo hili linaonyesha wahalifu wengine ni wababe kuliko wahalifu wengine na wanawaua kwa kuongozwa na ubinafsi na kusombwa na tamaa ya pesa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, wanaume wanapaswa kuwa na pesa nyingi. Iwapo mwanamume atashindwa kudumisha nafasi yake ya kuwa na pesa nyingi huenda akaingilia wizi. Visa hivi, vinaonyesha wazi kuwa katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah: 2018), kuna baadhi ya wanaume wanakuwa wezi sugu ili wadumishe hadhi yao ya kuwa na fedha nyingi kulingana na matarajio ya jamii.

Vilevile, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 154), baadhi ya wezi wanaowakandamiza wanaume ni wanawake. Kwa maoni ya Parsons (1937), wanawake wa kijadi hutekeleza 'jukumu bayana' katika familia zao, ikiwa ni pamoja na kulea watoto na kutunza mahitaji ya kihisia ya waume zao. Kwa hivyo, wasichana wanakua wakizingatia maadili ambayo yanapunguza uwezekano wao wa kusababisha madhara kwa wengine au kufanya uhalifu. Hata hivyo, mawazo ya Parsons (1937), yanapingwa na Alder, F. (1975). Kulingana na Adler, F. (1975), kuongezeka kwa uhuru na fursa za kiuchumi kwa wanawake,

kumesababisha viwango vya juu vya uhalifu wa wanawake. Anasema kuwa wanawake wanapofikia viwango sawa vya kijamii na mifumo ya ajira sawa na wanaume, wanaanza kufanana na tabia za uhalifu za wanaume pia. Alder, F. (1975), anaendelea kueleza kuwa, kuna makahaba wanawake ambao humuwinda mwanamume na kunasa nafsi yake iliyo ya thamani. Jambo hili humfanya mwanaume kuingia katika dhambi, hatari na anaweza kupata mauko. Makahaba hawa huwa wana lengo la aidha: kujiburudisha, kuwaibia na kuharibu maisha ya wengine. Makahaba hao huwa hawatafutwi bali wao ndio hutafuta wanaume watimize maksudi yao ya kupata pesa. Jambo hili la makahaba hawa kuwachuna wanaume pesa linaafikana na mhimili wa tatu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume kuwa wanaume ni wenye pesa. Mwanamke aliyefungwa katika jela moja na Gasoya anaeleza alikuwa ameshagundua kwamba wizi ni nyenzo muhimu ya kuendesha biashara ya ukahaba. Usiku mmoja, aliangukia mzungu pa! Makahaba wote walipigania kupata mzungu kwa sababu wazungu walilipa vizuri. Mara nyingine kwa dola za Marekani. Mzungu alikuwa na kibeti cheusi cha ngozi ambacho kilifura kwa kujaa madola. Baada ya kitendo cha ngono, kahaba huyu alimuua mzungu na akaenda mafichoni. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Baada ya kupata alicholipia, alianza kukoroma, nikajua amelala. Niliinuka, nikavaa harakaharaka gizani, nikanyemelea nyatunyatu upande wa kitanda alipolala. Nikachukua suruali yake yake iliyokuwa juu ya stuli, nikatoa kibeti na kukificha katikati ya matiti. Mara aligutuka kama aliyejiwa na jinamizi. Nikachukua stuli ile na kuinyanyua kwa nguvu zangu zote, nikamgonga kichwani. “Sikusubiri matokeo. Nilinyaka ndara zangu nikafungua mlango na kutoka mbio. (Mbatiah 2018: 154)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 154), inabainika kuwa uamuzi wa mzungu mwanaume kupenda starehe na wanawake kunasadifiana na Nadharia ya Uwezo- Mkuu wa Kiume kuwa wao ni waamuzi, wanaotumia wanawake kama chombo cha starehe. Hata hivyo, mhimili wa tano wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume unaeleza kuwa jamii imebadilika kwa hivyo, wanawake ambao wangethibitiwa na wanaume kama duni na chombo cha kukidhia tamaa ya mwili wamebadilika. Kwa hivyo, wanawake wana nguvu na mamlaka ambayo wanawatumia wanaume kutajirika na kuwaua. Maelezo ya kahaba aliyemwibia mzungu na kumuua yanasadifiana na mawazo ya Bly, R. (1990) kuwa, katika historia ya Marekani, wavulana na wanaume wa rangi nyeupe hutazamwa kama wanaume wenye hadhi

ya juu, matajiri na wenye pesa nyingi. Sifa hii imewafanya wanaume watumiwe na makahaba kama chombo cha kuchuna pesa ili wakidhi tamaa yao ya kupata pesa na watajirike haraka.

### 2.1.3 Nafsi

Nafsi ya binadamu ni sehemu ya mtu ambayo sio kimwili, inaweza kuwa imara au dhabiti, inaweza kufurahia au iwe na huzuni na inaweza kufanya uamuzi unaofaa au usiofaa (Glenn, E. 2002). Hali kama hii hutokea akilini mwa mtu na mara nyingi inaweza kuzua mgogoro wa kimawazo mtu anapopatwa na changamoto nyingi maishani na hatimaye kujifikiria kuwa yeye ni dhaifu zaidi ya viumbe wengine wa jamii. Maoni ya Scott (2020) ni kuwa, mgogoro wa kimawazo ni hali ya hisia; uzoefu wa ndani wa kuchanganyikiwa na wasiwasi kwa kiwango ambacho mbinu za kukabiliana na hali iliyofanikiwa hapo awali humfanya mtu kuwa na maamuzi na tabia zisizofaa. Aidha, mtu anaweza kutamani jambo fulani lakini nafsi yake ikamsuta na akaamua kuacha jambo hilo.

Aidha, Scott (2020), anaeleza kuwa ukandamizaji wa nafsi una kigezo cha kiakili au kifikra. Anasema ukandamizaji huu hutokea mhusika anapopata changamoto nyingi maishani. Anajidhalilisha na kila anapotangamana na wanajamii wengine, anaanza kujikinga kutokana na matamshi au mienendo yao kwake, hata ikiwa matamshi na mienendo hiyo haimdhuru. Huwa amejitenga na wenzake bila kujua kuwa anafanya hivyo. Hii ni hali ya unyanyapaa, yaani mtu kuona maisha hayana maana kwake, hivyo kujitenga na wenzake. Hali hii mara nyingi hutokea iwapo mtu daima anakashifiwa au kudharauliwa. Ukandamizaji wa nafsi kulingana na Scott (2020), unatokea akilini mwa mhusika. Anaendelea kusema kuwa mara nyingi hutokana na hali za nje anazopitia muathiriwa: wanavyosema watu kumhusu, wanavyomtendea au hata matukio aliyoyapitia maishani mwake.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 21), mhusika Mrima anapata mgogoro wa nafsi kutokana na matusi anayopata kutoka kwa Chifu Mshabaha. Vilevile, jambo lingine linalomfanya Mrima apate mgogoro wa nafsi ni hofu ya mkewe kuchukuliwa na Sagilu. Chifu Mshabaha anamtusi Mrima kwa maneno yafuatayo: **"Mrima wewe ni kijana fukara, mwenye matongo. Ukiruhusu Sagilu amuowe mkeo Mangwasha, atamhakikishia maisha ya kifahari na staladhi za kila aina."** Kauli hii ya Chifu Mshabaha kwa Mrima kuwa yeye ni fukara asiyeweza kumpa mkewe maisha mazuri na ya kifahari, yanashusha thamani yake kama mume na kiongozi wa familia yake. Mrima anahisi amedunishwa na ndiyo sababu anaamua kuwa pombe ya bwerere hataiacha. Kwa mujibu wa Simon, J. na Pregger, S. M. (1991), matumaini ya wanaume walionyimwa nafasi ya kujitokeza vizuri

yamekuwa kikwazo cha haki, uhuru na maendeleo yao katika jamii. Uwezo wa Sagilu na Chifu Mshabaha kumuonyesha Mrima yeye sio mume kamili kwa mkewe Mangwasha, kunajengwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume inayoeleza kuwa, katika jamii kuna baadhi ya wanaume wababe na wengine sio wababe. Jambo linaloshusha uwezo wao wa kuwa jasiri na wakakamavu katika kukabiliana na changamoto anazokumbana nazo.

Kadhalika, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 43), mhusika Mrima hajitambui na hajielewi kabisa. Aidha, wanaomzunguka Mrima kama vile Mangwasha, wanamuona kama sanamu tu. Hii ni kwa sababu anajihusisha na ulevi ambao umemfanya asiwajibikie maisha yake, afya yake, mke na watoto wake. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Mhn, ati familia? Mangwasha na wanawe watajipanga. Pombe ya bwerere siiachi ng'o! Najua Sagilu alimpenda sana mke wangu Mangwasha. Aaah! Mrima! vunja mifupa ukiwa bado una meno bwana. (Momanyi 2019: 43)

Kutokana na nukuu katika Momanyi (2019: 43), uamuzi wa mhusika Mrima kwamba haachi pombe ni namna ya kuikandamiza nafsi na afya yake. Inabainika kuwa Mrima akiwa nyumbani, mkewe Mangwasha alimuona kama mfano wa mume asiyekimu familia yake. Hii ni kwa sababu mara nyingi alikesha katika vilabu vya pombe mtaani Taria. Watoto wake Sayore na Kajewa walishinda wakimsumbua mama yao. Walitaka kujua aliko baba yao. Tabia hii ya mrima kukwepa majukumu yake na kwenda kubombea pombe siku uchao, ilitokana na Sagilu na Mshabaha kumtisha kuwa Sagilu mwanasiasa maarufu mjini Taria, atamuoa Mangwasha mke wa Mrima.

Aidha, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah: 2018), kuna baadhi ya wavulana ambao hawapendi kujiendeleza katika njia yoyote ile kama vile kuendeleza elimu yao. Tabia kama hii inafanya Kiguto kuwa na mgogoro wa kimawazo na huku ni sawa na kujikandamiza nafsi. Rejwa na Mwongi hawakuwa na uwezo wa kiakili kama wa Kiguto wala hawakuyapenda masomo yao. Walipotoka darasani walicheza na rununu zao za bei ya juu ambazo zilikuwa na kila aina ya mchezo. Kutokana na maelezo haya mtu kukiuka sheria za shule na kuwa na maadili yasiyofaa ni kujikandamiza nafsi. Kadhalika, Mwongi na Rejwa ni wahusika ambao hawatambui umuhimu wa kuwa na maadili mema na nidhamu. Wanapoadhibiwa, wanakataa kurekebisha tabia zao mbaya. Hali kama hii ni kuiangamiza nafsi kuendelea kufanya maovu. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Kiguto aligundua kwamba binamu zake walioza kupita kiasi cha kuweza kusaidika. Walijifanya watiifu, lakini waliendelea kuvunja sheria za shule kisiri.

> Walichojifunza ni kuficha uovu na kuwahonga wanafunzi ambao wangeweza kuwasema. Hakuna aliyeweza kuwazuia. Walitoka shuleni kila walipotaka na kwenda kutia nyenzo zao za kufanyia maovu. Kiguto alisikitika sana alipowaona watu aliowapenda yaani Mwogi na Rejwa wakipotea njia. (Mbatiah 2018: 115)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 115), tabia ya Mwongi na Rejwa ya kutotaka kubadili maadili yao na kuendelea kuvunja sheria za shule hata bada ya kuonywa; kunasawiriwa na mwandishi kimaksudi kuwa, katika jamii kuna watu ambao matendo yao hukashifiwa lakini wao hujikandamiza kinafsi wanapoendelea kufanya maovu na kukosa kujirekebisha. Ukandamizaji huu umemfanya Kiguto azame katika mawazo changamano kuhusu nafsi yake mwenyewe na binamu wake Mwogi na Rejwa lakini hapati jawabu mwafaka. Kiguto anawaza kwa nini kila wakati hana furaha moyoni na binamu zake wenzake wanamchezea shere. Fikra hii inamfanya Kiguto awe na ukiwa. Huu ni ukandamizaji wa kisaikolojia unaoletwa na upotovu wa kimaadili kutoka kwa Mwongi na Rejwa. Mbatiah amebainisha waziwazi kuwa Kiguto anapitia mengi ambayo yamemlemaza katika kuhakikisha binamu wake wana nuru ya elimu na wameendeleza shughuli zao kwa njia ya kawaida: Kiguto amekandamizwa na mawazo ya jinsi anavyojifikiria. Anawaona Mwongi na Rejwa kama wavulana ambao bado hawajajitambua wao ni nani na hili limeshinikizwa zaidi na umri wao mdogo ambapo akili yao haijakua ili kuweza kung’amua haswa njia bora zaidi ya kukumbana na wanayosema wengine kuwahusu.

### 2.1.4 Mzazi wa Kiume

Mzazi wa kiume ni mwanamume anayechukua jukumu la: kuzaa, kulea, kuadilisha na kuwa na uhusiano mzuri na watoto wake unaoendana na matarajio ya jamii. (Tafsiri yetu). Hata hivyo, kuna wale ambao wanakwepa majukumu na hawapo katika kuwaongoza watoto wa kiume ili wawe na maadili yafaayo.

Kulingana na Baker, C. E. (2014: 19), wazazi wa kiume wanaweza kuwakandamiza vijana wa kiume kisaikolojia au kimwili. Anaeleza kuwa mara nyingi, mtoto wa kiume hunyimwa haki zake za kimsingi kama vile kutangamana na wenzake, kutopewa elimu na kutusiwa. Kwa hivyo, tunaweza tukasema amekandamizwa kisaikolojia. Vilevile, Baker, C. E. (2014) anasema kuwa, mzazi wa kiume anapokosa kumwadhibu mtoto wake wa kiume huwa amekandamiza ulezi mwema kwa mtoto huyo. Hata hivyo, mzazi anapomwadhibu mtoto wake na kumjeruhi, mara nyingi adhabu hii hailingani na kosa alilolitenda mvulana huyo.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 32, 148), tunapata wazazi wa kiume kama vile Mrima wakiwakandamiza wanao wa kiume kwa viwango tofautitofauti kama vile: kukosa kuwajibika na kukosa kuwapa malezi yafaayo. Wazazi wengi wa kiume huwa na mazoea ya kuondoka kila asubuhi kuelekea kutafuta riziki. Kwa upande mwingine, baadhi ya wazazi wa kiume hupotelea ulevini bila kujali watoto wao wa kiume wanalelewa vipi. Baadhi yao huwa hawana muda wa kuwa nyumbani. Hali hii huwakosesha wanao wa kiume kukosa baba mwelekezi wa kuwaadili na kuwapa mwelekeo mzuri wa maisha. Haya yanabainika katika nukuu zifuatazo:

> Mrima alianza kushiriki ulevi akawa anakesha katika vilabu vya pombe… Sayore alitaka kujua aliko baba yao. (Momanyi 2019: 32)
>
> Alipofika nyumbani, Sayore alibaki kumtazama baba yake kama mgeni aliyewasili kwao. Ilimchukua muda kumkubali mgeni huyo. (Momanyi 2019: 148)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 32, 148), ni wazi kuwa Mrima amejitenga na jukumu la malezi kwa kumdhulumu Sayore kisaikolojia. Sayore hakujua babake mzazi alikuwa amepotelea wapi. Jambo hili lilimpa msongo wa mawazo asijue la kufanya. Aidha, katika, Momanyi (2019: 148), tumepata kwamba Sayore anakosa kumtambua babake mzazi. Hili linamchukua muda kumkubali babake, kwa kumrejelea kama mgeni. Huu ni ukandamizaji wa kisaikolojia unaomwathiri Sayore kwa njia hasi. Hii ni kwa sababu Mrima alikuwa amepotelea ulevini, akakosa muda wa kutangamana na kumuadilisha mwanawe. Yaani alikosa ulezi wa baba yake. Wazazi wengi wa kiume huwa na mazoea ya kuenda kujistarehesha na vileo, suala linaloafikiana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kuwa mwanaume anapenda kustarehe jambo ambalo humfanya kusahau na jukumu lake kama mwanaume. Mawazo ya Bly, R. (1990) ni kuwa akina baba wa jamii zilizoendelea za viwandani wanashindwa kuwapa wanao wa kiume kile wanachohitaji kuwa wanaume. Anasema kuwa wavulana wanahitaji jando katika utu ili wakaribishwe katika baba za ulimwengu.

Vilevile, Bly, R. (1990), anaeleza kuwa mzazi wa kiume mara nyingi hayupo na hajali kwani mara nyingi linalomsukuma kutoka nyumbani ni kuelekea kazini kutafuta riziki na baadhi ya wanaume wengine wanaenda kujistarehesha aidha kwa vileo na kadhalika. Hali hii inamfanya Mrima akosekane katika malezi ya mwanawe wa kiume Sayore. Kwa maoni ya mtafiti, ni dhahiri kuwa wanaume katika karne ya ishirini na moja wamebadilika sana. Inashangaza kuona jinsi wanavyokata tamaa upesi eti kwa sababu ya kukumbwa na changamoto kama vile

kutusiwa, kutishiwa kuwa mke atachukuliwa na wanaume wababe kumshinda au kufutwa kazi. Hawadhihirishi kamwe ukakamavu na ujasiri unaohusishwa na wanaume katika jamii nyingi. Fauka ya hayo, wanaume wa karne hii wanapopata matatizo, wanashindwa kabisa kuchukua japo hatua moja ili kuyatatua. Hatuwaoni wakitafuta suluhisho. Wengi wao wanatorokea shida zao kwa kujiingiza katika ulevi kama Mrima. Tungetarajia kuwa, mwanamume anadhihirisha ujasiri wake wa kudhibiti na kukimu familia yake.

Kadhalika, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 180), kuna baadhi ya wazazi wa kiume kama vile Sagilu wanaonekana wakiwatumia wanao wa kiume kama vyombo vya kuendeleza uovu katika jamii. Wazazi hao wa kiume wameshiba taasubi ya kiume inayoongozwa na mfumodume. Hawaonekani wakiwaelekeza wavulana kwa njia inayofaa. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi katika nukuu ifuatayo:

> **Mashauri tokea mbali,** huku machozi yakimtiririka njia mbili, **aliwaambia Lonare jinsi Mzee Sagilu baba yake alivyoweza kumtumia mara kadha.** Alisimulia jinsi alivyoshauriwa na Mtemi kubomoa jengo la Lonare. **Alisimulia maovu mengi aliyotenda kwa niaba ya babake.** Mwishowe Sauni alitaka kumtimua kutoka pale. Alimwita kibaraka na jasusi aliyetumwa kumharibia Lonare kura. "Nani asiyemjua babako kwamba ni adui mkubwa wa Waketwa. Nani asiyejua yote aliyomtendea Mangwasha mumewe? Sasa amekutuma kuja kutuvunja kutoka ndani. **Wewe ni kibaraka wa babako." Sauni alifoka, akasimama kutaka kumtoa mle ndani**. (Momanyi 2019: 180)

Kutokana na nukuu katika Momanyi (2019: 180), mhusika Sagilu anadhihirisha yeye ni kiongozi mbaya wa mtoto wake wa kiume (Mashauri). Mzee Sagilu, babake Mashauri anamkandamiza kimaadili akiwa na ufahamu huo. Badala ya kumwelekeza kuwa mvulana anayewajibika katika ujenzi wa jamii yake, anamfundisha kuwa mkatili, asiyejali watu wengine na anayeongozwa na ubinafsi wa kujitajirisha kwa manufaa yake mwenyewe. Mashauri anaonekana akifuata ushauri wa babake Sagilu wa kuhujumu Lonare kwa kumharibia mali yake kama inavyodhihirika wakati alipobomoa jengo la Lonare. Katika Kiwango hiki tunakumbana na ukandamizaji wa mzazi wa kiume kwa mtoto wake mvulana ambaye anamfundisha kuwa mnafiki badala ya kuwa kijana aliyeadimika. Jambo hili linamfanya Mashauri kutukanwa na Sauni anayemwita kibaraka wa babake.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 199), kuna wazazi wa kiume waliokimbia majukumu yao ya kuwa baba, mzazi na mlezi. Kauli ya mhusika Mangwasha inapiga mwangwi hali halisi ya mtoto wa kiume anaposema:

> Mara nyingi Mangwasha alipotembea mjini, hakusahau kuwahutubia vijana wazururaji wa mji…Mangwasha aliwaona vijana hao kama kizazi kinachopotea. Kizazi kipya kinachoangamizwa taratibu na kizazi chenye mamlaka na mbinu zote za kukiauni**. Alijiuliza kama vijana hawa, hasa wale wa kiume watakuwa baba wa aina gani.** Je, wataweza kuzihimili familia zao iwapo hata wao wenyewe wanahitaji kuhimiliwa? "Ole wako ewe mwanamume uishiye leo...**Yu wapi baba aliyekutekeleza?** (Momanyi 2019: 199)

Kutokana na usimulizi katika nukuu, Momanyi (2019: 199), vijana wa kiume wanaozurura mjini hawaonekani wakiwa na mzazi wa kiume katika maisha yao ya kila siku. Mangwasha anasikitikia mwanamume anayeishi katika jamii ya leo. Kulingana naye, baba aliyemtekeleza mtoto wa kiume hajulikani aliko. Vijana wa kiume wazururaji mji wamekosa mzazi wa kiume wa kuwaongoza ili wapate mustakabali mzuri wa maisha. Hali hii inawafanya kutoweza kujitegemea na kuweza kuwa tegemeo katika jamii.

### 2. 1. 5 Makahaba

Makahaba ni la watu ambao hutumia miili yao kama biashara au kama bidhaa kwa kufanya ngono na wanaume au wanawake ili wapate pesa. (Tafsiri yetu). Makahaba huweza kuwa wanawake au wanaume. Makahaba hawa, mara nyingi huhadaa wanaume au wanawake kwa kutumia urembo wao na mapenzi yasiyo ya dhati ili watimize lengo lao la kupata pesa.

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah: 2018), kuna wanawake ambao wamejiingiza katika biashara ya umalaya na lengo lao ni kuwadhulumu wanaume. Kulingana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, wanaume ndio watawala na huwa na mamlaka makuu katika jamii. Kwa mujibu wa Izugbara (2005) wanaume hushikilia nafasi za raslimali katika jamii kama vile mashamba, kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini. Mtazamo kwamba wanaume ni wenye pesa umewafanya wanaume watumiwe na wanawake kama chombo cha kuchuna pesa. Tunaweza kuirejelea kama biashara ya "nipe nikupe." Hata hivyo, bidhaa inayotumiwa na wanawake ni miili yao ili wapate pesa kutoka kwa wanaume. Haya yanabainika kupitia mfano huu:

> Usiku mmoja, niliangukia Mzungu pa! Makahaba wote walipigania kupata Mzungu kwa sababu Wazungu walilipa vizuri. Mara nyingine kwa dola. Nani asiyejua uzito wa dola za Marekani. Tulilala, tukachapa maji na tukaenda kulala. Baada ya kupata alicholipia, alianza kukoroma, nikajua amelala. Nikachukua stuli ile na kuinyanyua kwa nguvu zangu zote, nikamgonga kichwani. "Sikusubiri matokeo. Nilinyaka ndara zangu nikafungua mlango na kutoka mbio. (Mbatiah 2018: 154)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018:154), kahaba aliyefungwa na Gasoya ameshauku katika kitendo cha kumuua Mzungu aliyempata usiku mmjoa katika biashara yake ya ukahaba. Tunaelezwa kwamba kahaba huyu anakiuka haki ya Mzungu ya kuishi. Alimuua Mzungu huyo ili apate nafasi ya kutoroka. Hii ni njia mojawapo ya jinsi makahaba wanavyowakandamiza wanaume kwa kuwatoa uhai.

Vilevile, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi: 2018), kuna wanawake ambao utashi wao wa maisha ya anasa na pesa unasababisha ukandamizaji wa jinsia ya kiume. Wanawake hao wanachojali ni pesa na sio mapenzi ya dhati. Haya yanabainika katika nukuu ifuatayo:

> *I say,* wajua nimewaona wapi leo? Katika hoteli ya *Saturn.* Cheiya na Sagilu Wameshikana "Sasa umeamini au sivyo? *Don't joke with some of these modern girls my friend. Their thirst for money is unquenchable."* Mashauri aliketi na kushusha pumzi. (Momanyi 2019: 178)

Kutokana na kauli ya Mashauri katika Momanyi (2019: 178), mhusika mwanamke amechorwa kama kiumbe asiye na mapenzi ya dhati na aliyebeba ushawishi na tamaa zote za ulimwengu. Haya yanaonyesha mwanamke ni mtegemezi wa wanaume. Utegemezi huu wa jinsia ya kike unajengwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, inayoeleza mwanamke huchorwa akiwa kiumbe duni, mdhaifu na mwenye kufanyiwa mambo kwa sababu mwanamume hutazamwa akiwa na mamlaka ya juu kumshinda. Kwa hivyo, wanaume wanapotumiwa kama chombo cha kukidhi mahitaji ya wanawake, wao huchukulia ni jukumu lao kama wanavyotarajiwa na jamii yao.

Vilevile, kutokana na nukuu katika Momanyi (2019: 178), Cheiya ametumika kusambaratisha uhusiano mwema kati ya baba mzazi na mwanawe, Sagilu na Mashauri, na kuzua uhasama baina yao. Kisa hiki kinasadifiana na kisa katika bibilia ambapo mwanamke aliyeumbiwa Adamu alishikwa na tamaa za ulimwengu zilizofifisha uhusiano mzuri kati ya Adamu na Mungu (Reynolds, W. T. (2020). Kwa hivyo, mwanamke amejengwa kama kiumbe binafsi

asiyejali athari hasi zinazowapata watu wengine kutokana na tamaa yake. Cheiya alienzi pesa kuliko heshima na mapenzi yake kwa Mashauri.

### 2.1.6 Jamii

Jamii ni mkusanyiko wa watu wanaoishi kwa pamoja katika eneo moja la kijiografia wakiunganishwa na historia yao na wakitambuliwa kwa utamaduni wao, lugha, mila na desturi (Stanley, 1967). Anasema kuwa, ili mkusanyiko fulani wa watu uweze kuitwa jamii, vigezo vifuatavyo lazima viwepo: watu wa jinsia na rika zote yaani wanawake kwa wanaume, wazee kwa vijana, wanaoishi pamoja, mfano wakazi wa kijiji fulani, ndani ya mipaka ya kieneo mfano wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro na kadhalika.

Kwa mujibu wa Connel, R. (1987), jamii humtarajia mwanamume ajihisi na aendeleze majukumu yote aliyotengewa na jamii yake kama mwanamume. Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, humtazama mwanamume akiwa mshindani na mwenye mamlaka makuu serikalini, katika siasa na kadhalika. Mathalani, jamii inapomgeuka na kumfanya awe na wasiwasi na mwenye shaka basi huwa imeshusha ujasiri wake. Mambo ya ubaguzi, chuki na ukabila siyo mageni katika jamii nyingi za Kiafrika. Kuna nchi ambazo tumeshuhudia jamii ambazo zimepigana vita kwa sababu ya kugombania madaraka. Kuna wale wanaopendelewa na kupewa nyadhifa mbalimbali za kiserikali.

Katika riwaya ya *Nguu za jadi*, (Momanyi 2019: 7), nchi ya Matuo imejaa ubaguzi wa kimbari ambapo jamii ya Wamunyu inawabagua watu wa jamii ya Waketwa. Jamii ya Wamunyu ndiyo inatawala nchi ya Matuo kwa kuwa Mtemi wa Matuo bwana Lesulia alikuwa wa mbari ya Wamunyu. Nyadhifa zote kubwakubwa serikalini walipewa watu wa mbari ya Wamunyu. Vilevile, watu wa jamii ya Wamunyu walipendelewa kwa kupewa fursa mbalimbali za kibiashara. Waliruhusiwa kuendesha biashara haramu kama dawa za kulevya. Wengine kama Sagilu na Mshabaha walifanya biashara hizo bila kulipa kodi. Wafanyabiashara wa jamii ya waketwa kama vile Lonare, walifanyiwa hujuma za kufilisi biashara zao. Lonare alipojitosa katika ulingo wa kisiasa maisha yake yalikuwa katika hali ya hatari. Dhuluma hii inaongozwa na chuki na ukabila kama ilivyo katika mfano ufuatao:

> Waliyemdhania ni kiongozi wao Lonare amekuwa akipitia kwenye mitego ya hatari aliyotegewa na Wamunyu. Mara kadha aliepuka kifo kutokana na mashambulizi ya watu waliotumwa na Sagilu, mfuasi wa Mtemi Lesulia kumwangamiza. (Momanyi 2019: 7)

Kutokana na maelezo katika Momanyi (2019: 7), Lonare ni mhusika wa kiume anayekandamizwa na jamii ya Wamunyu kwa misingi ya ukabila na ubaguzi. Wamunyu, wanamchukia Lonare na kumpangia njama ya kutoa uhai wake. Lonare anaishi maisha ya wasiwasi kwani anakosa uhuru wa kutekeleza nafasi ya kuwa huru. Inabainika uchaguzi mkuu unaendeshwa kwa misingi ya kikabila na ubaguzi, ambapo wananchi hupiga kura kwa kuzingatia mgombea anatoka kabila gani. Kwao haijalishi ana sera nzuri au mbovu kwani watu ya kabila la Wamunyu wanamchagua Mtemi Lesulia kwa misingi ya ukoo. Jambo hili linamfanya Lonare kukosa kuchaguliwa kama Mtemi. Kwa hivyo, anapoteza uteuzi aliowania katika nchi ya Matuo. Hii ni kwa sababu jamii ya Matuo imejigawa katika makundi mawili hasimu ya kisiasa.

Jambo hili linaafikiana na mawazo ya Connel, R. (1987) mwasisi wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Anasisitiza jamii huangalia nguvu za mwanamume kutokana na ushawishi na matendo yake. Anaendelea kueleza kuwa ushawishi huo wa wanaume wenye mamlaka, hufanya jamii fulani kufuata mwelekeo fulani katika asasi mbalimbali kama vile asasi za kisiasa, kielimu na kidini. Hali hii ndiyo huzua makundi mawili ya watu na jamii wanaopimana nguvu na mara nyingi huzua ukandamizaji wa jamii ambayo ni dhaifu. Kwa hivyo, katika nchi ya Matuo kuna kundi dhaifu (jamii ya Waketwa) lililomuunga mkono Lonare na lingine lenye nguvu na ushawishi mkubwa wa uongozi (jamii ya Wamunyu) lililompigia debe Mtemi Lesulia na kudinda kumpa Lonare kura.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, Momanyi (2019: 200), kupitia mhusika Mangwasha, nchi ya Matuo imejishughulisha na masuala mengi ya wanawake na machache yanayohusu wanaume. Mangwasha anadai kuwa masuala kuhusu msichana na wanawake yamepewa kipaombele na jamii ya Matuo. Kulingana naye, jamii yake inahamasisha wanajamii wengine wa nchi ya Matuo, kabila la Waketwa na kabila la Wamunyu kuhusu umuhimu wa kumkinga, kumuongoza na kumwelekeza msichana katika maisha yake. Anaeleza kuwa msichana anaelimishwa ili aweze kukubaliana na changamoto za maisha kwa ujasiri. Hali hii inadhihirisha ubaguzi wa jinsia unaoendelezwa na jamii ya Matuo. Kulingana na Mangwasha mtoto wa kike nchini Matuo, amewekewa wazi mikakati ya kumnasua kutoka minyororo ya dhuluma. Jambo hili limempa mwanamke mwelekeo wa jinsi anapaswa kujiendeleza kimaisha, mikakati inayokosekana kwa mtoto wa kiume anayeonekana anajiweza katika kila jambo. Maelezo haya yanaafikiana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kuwa mwanaume huchorwa akiwa na sifa angama za ukakamavu, ujasiri na aliye na

uwezo wa kutatua shida na migogoro anayokumbana nayo. Inabainika kuwa iwapo jamii haitatambua mwanaume pia ni binadamu aliye na udhaifu kama wanawake, basi atazama katika matatizo mengi maishani mwake.

### 2.1.7 Wanarika wa Kiume

Wanarika huwa ni jumla ya watu katika kundi moja lenye sifa zinazolingana na zaidi huwa wanakaribiana kiumri. (Fasiri yetu). Washiriki wa kikundi rika kimoja wana uwezo wa kutiwa moyo na kutaka kuwafuata wenzao kwa kubadilisha mtazamo, maadili au mienendo ili iendane na ile ya kikundi ya mtu binafsi.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi,* (Momanyi 2019: 199), kupitia mawazo ya Mangwasha ni wazi kuwa wavulana wengi katika nchi ya Matuo hawakuwa na kazi jambo lililowafanya wajihusishe na uovu. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Aliwaona vijana hasa wa kiume waliojikusanya kwenye viambaza vya maduka. Hawakuwa na shughuli maalum iliyowakutanisha pale ila kulisukuma gumzo tu. Kuna wale waliofuzu kujiunga na vyuo vikuu au hata katika shule za upili. Hawa walikongamana, wengine wakivuta bangi au kutumia dawa kali za kulevya kwa kujidunga sindano. Wengine walizurura tu katika barasate za mji wasijue wafanyalo. Vibaka nao walikuwa wakisubiri fujo au ghasia fulani zizuke ili wapate nafasi ya kunyang'anya watu mali zao au kupora maduka. (Momanyi 2019: 199)

Kulingana na usimulizi wa Mangwasha katika Momanyi (2019: 199), ni wazi kuwa wavulana wengi hawakuwa na kazi ya kufanya. Walijihusisha na uvutaji bangi, walijihusisha na wizi, wengine walitumia dawa za kulevya na walitumia sindano moja kujidunga kokeni. Iwapo mmoja wao ana ugonjwa hatari ambao hauna dawa kama vile UKIMWI, wavulana hawa wanajiweka katika hatari ya kuambukizana ugonjwa huo usio na tiba. Kutokana na mawazo ya Connel, R. (1987: 183), mahusiano ya wanaume hujengeka katika mazingira fulani ya kihistoria na kijamii. Kulingana naye mazingira haya uhalalisha uhusiano usio sawa wa kijinsia kati ya wanaume na wanawake. Anaeleza kuwa mwanamume katika harakati ya kufanikisha mahusiano yao na watu wengine, wanakubwa na ushawishi wa wanarika, wa kikabila na utamaduni katika kujenga ubabe unaotambulika katika jamii yake. Hali hii inawafanya baadhi ya wanaume kujipata katika makundi yanayofanya mambo yayoweza kuwaathiri kiafya, kimwili na kisaikolojia.

### 2.1.8 Wanasiasa

Mwanasiasa ni mtu mwenye uzoefu katika sanaa au sayansi ya serikali na anahusishwa kikamilifu katika kuendesha shughuli za serikali ya nchi fulani; na kwa kawaida huwa amejihusisha na siasa za chama kama taaluma ambacho kina imani sawa (Deutsch, K. W. 1970). Anaeleza kuwa wanasiasa wanaweza kuchaguliwa kwa njia ya kupiga kura, ambayo hufanyika katika demokrasia, au wanaweza kuteuliwa na kiongozi. Mfumo wa kisiasa wa nchi ni ishara muhimu ya jinsi kuishi huko. Baadhi ya mifumo inafanya vizuri na huduma za umma kama vile afya na elimu. Katika nchi zingine, rushwa au uzembe husababisha huduma duni. (Fasiri yetu). Wanasiasa hufanya maaamuzi katika ngazi mbalimbali za jamii kama vile mji na taifa husika. Kuna wanasiasa ambao hutekeleza mambo yote ya kiutawala kwa misingi ya katiba na demokrasia ambayo ndiyo serikali ya watu. Hata hivyo kuna wale ambao hufanya matendo mabaya kama vile kushiriki katika: ufisadi, fitina na ukatili kwa wapinzani wao. Hali kama hiyo, huzua ukandamizaji kwa wanaume wasio na ushawishi mkubwa wa kisiasa.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 64), wanasiasa Mtemi Lesulia na Sagilu wanamchukia mpinzani wao Lonare. Kutokana na chuki yao wanatuma magaidi kukatisha maisha ya Lonare. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi katika mfano ufuatao:

> Mtemi Lesulia na Sagilu walikuwa tutu kwa ufu. Wote walimchukia Lonare, wakamchukua kama hasimu wao mkuu. Walimpikia majungu, wakampangia njama ili awe muflisi. Walituma magaidi kumkatizia maisha. (Momanyi 2019: 64)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 64), Mtemi Lesulia na Sagilu wanamkandamiza Lonare kwa kumchukia, kufilisisha biashara zake na hata kumtumia magaidi kumuua. Maelezo kama haya yanasawiri Mtemi Lesulia na Sagilu kama wahusika waliokosa utu. Wameongozwa na tamaa ya uongozi na chuki. Nia yao kubwa ni kumnyamazisha na kumwondoa Lonare kwa sababu wanamwona kama kikwazo cha wao kuendelea kuwa wanasiasa maarufu. Tabia hii ya Mtemi Lesulia na Sagilu kutaka kumnyamazisha Lonare, inaafikiana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Nadharia hii inaeleza kuwa kuna wanamume ambao huwa na mamlaka na nguvu zaidi kuliko wanaume wengine katika jamii yake. Wanaume hao (Mtemi Lesulia na Sagilu) wanatumia madaraka yao vibaya na kuunda njama ya kumteka nyara Lonare ili watwae uongozi wa nchi ya Matuo kwa urahisi bila upinzani.

Kadhalika, katika Momanyi (2019: 201), kuna wanasiasa ambao wanaendeleza utumwa wa wavulana bila kujali maisha yao. Mtemi Lesulia anawatumikisha na kuwakandamiza wavulana wengi wa mji wa Taria kwa kuwalipa ada duni. Anawalipa shilingi ishirini kwa siku hata baada ya kufanya kazi kwa shamba lake kubwa la mikonge. Ni kinaya kwa Mtemi Lesulia kuwakandamiza wavulana kama vile Sailoki kwa kuwaajiri badala ya kuwasaidia kusaka elimu. Hii ni kwa sababu yeye kama Mtemi anapaswa kuakikisha kila mtoto amepata elimu lakini haonekani akifanya hivyo. Hali hii inawafanya wavulana wengi wa viungani vya mji wa Taria walio na ulitima mwingi kukataa shule ili waende wakaajiriwe waweze kukidhi mahitaji yao ya kimsingi kama chakula. Kuajiriwa kwa wavulana hawa kama vile Sailoki watafute riziki na kukidhi mahitaji yao, kunaafikiana na na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Nadharia hii humtazama mwanamume kama mtafuta riziki anayepaswa kukidhi mahitaji yake na jamii kulingana na matarajio ya jamii yake. Jukumu hili la wanaume la kukidhi mahitaji ya jamii yanapelekea wavulana hawa kukandamizwa na mabwenyenye kama Mtemi Lesulia wasiojali elimu ya wavulana hawa. Inabainika iwapo kizazi hiki hakitashughulikiwa kuendeleza elimu yao maendeleo na maisha bora ya kizazi kijacho yatakuwa chini.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 22), ni vigumu kujenga familia na jamii mpya iliyostawi iwapo kuna wanafiki na wasaliti. Amemtumia mhusika Mrima kama kielelezo cha watu katika jamii ambao wanaweza kununuliwa kwa fedha na kuisaliti ndoa na familia yake. Mrima anaisaliti familia yake kwa kupewa pesa nyingi na Sagilu ili aende kulewa na kuitekeleza familia yake pamoja na malezi ya wanawe Sayore na Kajewa. Sagilu alikuwa anafanya hivyo ili kumshinikiza Mangwasha akubali kuwa naye mapenzi lakini Mangwasha akadinda kuitikia tabia zinifu za Sagilu. Vilevile, Sagilu anaendelea na juhudi za kuwapokonya wanaume wengine wake zao. Anafanya hivi kwa sababu ya ukuruba wake na Mtemi. Tabia hii yake inamfanya aoe mara tatu. Haya yanabainika katika mfano:

> Sagilu alioa mara Tatu. Wanawake **wote hao aliwanyang'anya wanaume wengine**. Alinyemelea na mwishowe kuuvunja unyumba. Alijulikana sana Taria kwa sababu hii. (Momanyi 2019: 22)

Kulingana na mfano katika Momanyi (2019: 22), Sagilu amechorwa kama mwanamume mkware na mtajika katika mji wa Taria. Yeye alitaka kila mwanamke mzuri awe wake. Aliwanyang'anya baadhi ya wanaume wake wao. Jambo hili linakandamiza mapenzi na

unyumba wa wanaume wengine wanaoachwa katika lindi la upweke. Hali hii inawafanya wanaume hao wamchukie Sagilu. Wanaume hao wanapokuwa na chuki ni kuwakandamiza wasiwe na furaha ya kuwa na familia na mapenzi kutoka kwa wake wao. Tabia hii ya Sagilu kuwa na uwezo wa kuwanyang'anya wanaume wengine wake wao, linaafikiana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Nadharia hii huangangalia mwanamume kama mbabe. Hii inadhihirisha kuna baadhi ya wanaume waliona nguvu kushinda wanaume wengine. Kulingana na Connel, R. (1987) mwanaume hutazamwa kuwa 'kichwa' katika familia yake. Iwapo nafasi hii itachukuliwa mwanaume huyo huwa amekandamizwa na nafasi yake ya kuwa 'kichwa" katika familia yake hushushwa.

### 2.1.9 Hitimisho

Kupitia riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* na *Nguu za Jadi*, (Mbatia, 2018) na (Momanyi, 2019) mtawalia, makundi nane yanayowakandamiza wanaume yamechanganuliwa. Makundi hayo ni: polisi, wezi, nafsi, wanasiasa, wanarika, makahaba, jamii, na mzazi wa kiume. Kwa kurejelea malengo ya utafiti inabainika kuwa: tamaa ya uongozi, ya mwili na ya kutajirika haraka, ubinafsi, asasi za jamii kama vile: elimu na siasa ni baadhi ya vichocheo vinavyofanya makundi hayo kukandamiza wanaume na wavulana. Kuwepo kwa makundi yanayokandamiza jinsia ya kiume kunadhihirisha dhalimu wanazopitia.

# SURA YA TATU

## ATHARI ZA UKANDAMIZAJI WA JINSIA YA KIUME KATIKA RIWAYA YA *NJOZI YAPATA MTENZI* (2018) NA *NGUU ZA JADI* (2019)

### 3. 0 Utangulizi

Katika sura hii tunaangazia athari zinazowapata wanaume kutoka kwa makundi kandamizi kama inavyodhihirika katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah, 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019). Matendo mbalimbali ya makundi kandamizi yamedhihirisha athari anazopata mwanamume. Mifano mwafaka kutoka kwa riwaya teule zimetolewa kudhihirisha athari za ukandamizaji wa jinsia ya kiume ili kufanikisha malengo ya utafiti huu. Kulingana na Connel, R. (1987), jamii humtazama mwanaume kama mwenye hadhi ya juu kuliko mwanamke. Anaendelea kudai kuwa fikra hizi huongozwa na itikadi, mila na desturi ya jamii husika na hutambulika katika historia ya jamii yake.

Katika sura hii, baadhi ya athari ambazo tumechunguza hapa ni pamoja na: Mmomonyoko wa maadili, msongo wa mawazo, mauaji, kupata malezi yasiyofaa, kukosa kuendeleza

masomo, kukosa chakula, malazi, na mavazi, ugonjwa wa kiakili, kupoteza imani na polisi na kupoteza kazi.

### 3.1 Mmomonyoko wa Maadili

Maadili ni mienendo au tabia njema inayokubalika katika jamii mahususi kama sehemu ya maisha ya jamii husika (Watuha, 2011). Aidha, mmomonyoko wa maadili ni hali ya kukiuka maadili ya jamii fulani. (Tafsiri yetu). Kwa Mujibu wa Mowin (2018), maadili anayopata mtu kutoka kwa jamii yake huathiri mawazo yake yakawa hasi au chanya katika uzoefu wa matukio ya maisha yake.

Kutokana na mabadiliko ya kijamii hasa ujio wa utandawazi, tamaduni na maadili ya kigeni yameingizwa katika bara la Afrika. Maadili mema yaliyokuwa yakihimizwa katika jamii za Kiafrika tangu zama za kina babu zetu yametokomea na kutupwa katika kaburi la sahau. Aidha, Kgatia (2013) anasema kuwa, kupitia vyombo vya habari na burudani kwa mfano televisheni, simu ya mkononi, radio, mtandao, magazeti, filamu na video, utamaduni wa magharibi umesambazwa ulimwengu kote. Matokeo yake ni kuwa vijana wameshawishiwa kuuenzi na kuutekeleza utamaduni huo bila kuweka mipaka. Kadhalika, utamaduni wa magharibi ambao umeenezwa kote Afrika kupitia utandawazi umeathiri sana maadili na amali za Kiafrika (Oni, 2003). Elimu, asili ya maadili ya Kiafrika iliyokuwa ikihimiza heshima kwa watu wazima, utiifu, wema, upendo na umoja, imewekwa kando huku elimu ya kimagharibi ikihimizwa. Vijana wa Afrika wamefanywa kuamini kuwa utamaduni wowote wa Kiafrika unaohusiana na watu weusi haufai, hauna maana na umepitwa na wakati ilhali utamaduni wa Magharibi wa watu weupe ndio bora na ufaao kutekelezwa. Basi utamaduni huo wa wazungu uliojificha katika elimu tunayopata kwa sasa na pia vyombo vya habari na mawasiliano hasa simu za mkononi, unapitishwa pole pole kwa watoto na vijana na kudaiwa kuwa huo ndio usasa. Vijana Waafrika wamefanywa kuiga mitindo ya mavazi, tabia, nyimbo, mitindo ya nywele nakutumia muda mwingi wakitumia simu za mkononi, huku wakidharau masuala ya elimu na utamaduni wa Kiafrika.

Kutokana na utafiti uliofanywa na Keeley (2017), matumizi ya simu ya mkononi huwa na athari kubwa kwa maisha ya vijana. Ingawa matumizi ya rununu yanaweza kuwa makubwa, matumizi hayo pia yanaweza kuvuruga maisha ya vijana sio tu kiafya bali kisaikolojia. Ripoti hii inadhihirisha kuwa vijana wanapotumia simu ya mkononi isivyofaa, wanaweza kuwa na uraibu unaovuruga kabisa jinsi wanavyotangamana na wengine na mara nyingi inaweza kupoteza umakinifu. Hali hii inadhihirishwa na wahusika Mwogi na Rejwa katika riwaya ya

*Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 140). Inabainika kuwa wahusika Mwogi na Rejwa **wanakosa kutumia muda wao katika masomo kwani walicheza na rununu zao walipotoka darasani.** Hali ya kukosa kumakinikia masomo yao inawafanya **kupata matokeo duni** katika mtihani wa kidato cha nne kwani wote walipata alama ya D. Ndio waliovuta mkia katika shule ya upili ya Wateule.

Vilevile, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah, 2018: 69), kuna wavulana (Mwogi na Rejwa) ambao maadili yao yamedidimia. Wavulana hao wanajihusisha na matumizi ya dawa za kulevya kutokana na pesa nyingi wanazopewa na mzazi wao kiume Mark Bagite. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, wanaume huwa na pesa nyingi. Kutokana na nadharia hii, wanaume wenye pesa nyingi huwa na hadhi ya juu na huwa na matarajio makubwa kwa watoto wao. Jambo hili huwafanya wawadekeze watoto wao kwa kuwapa kila wanachohitaji kama vile pesa nyingi, kupelekwa katika shule za kibinafsi na kuishi maisha ya kifahari. Wazazi wanaotumia mbinu ya kuwapa watoto wao pesa nyingi huwapenda watoto wao kupita kiasi (Santrock 2007). Kulingana naye wazazi hao hawatungi sheria zozote za kuwaongoza watoto wao. Wao huwaacha huru wafanye watakalo bila kuangalia athari zinazoweza kuwapata. Maelezo haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> **Mwongi na rejwa ambao waliambulia alama za chini** walitafutiwa shule ya kibinafsi ambapo **badala ya kusoma walienda kufunzwa kuvuta bangi.** (Mbatiah 2018: 69)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 69), imebainika kuwa Mwongi na Rejwa hawakuthamini masomo yao, ila walikuwa watoro wa nidhamu. Walijisukuma katika matumizi ya bangi. Hii ilitokana na pesa nyingi Mark Bagite aliwapa wanawe. Jambo hili linawafanya Mwongi na Rejwa kufeli masomo yao kwa kuambulia alama za chini. Kufeli huku kunasababishwa na wao kutumia muda mwingi wakivuta bangi badala ya kutia juhudi masomoni. Aidha, imebainika kuwa matumizi ya dawa za kulevya yanafanyika kwa uficho mkubwa katika jamii. Hata hivyo, baadhi ya shughuli zinazohusu dawa za kulevya, zinafanywa kwa usiri katika jamii. Kadhalika, watu ambao wanaonekana kujijengea heshima katika jamii ndio wanahalalisha matumizi ya dawa za kulevya. Wanafanya hivi kwa kujificha kwenye kivuli cha tamaduni na asasi mbalimbali za jamii kama vile siasa, uchumi, dini na elimu. Hii ndiyo sababu, Mark Bagite badala ya kuwaonya Mwogi na Rejwa dhidi ya kutotumia bangi, anawatafutia shule ya kibinafsi ili waendeleze elimu yao.

### 3.2 Msongo wa Mawazo

Msongo wa mawazo ni hisia ya kutoweza kukabiliana na mahitaji yanayotokana na kazi, mahusiano, shinikizo za kifedha na hali zingine za maisha. (Tafsiri yetu). Ni kawaida kupata hisia za msongo wa mawazo, lakini zisiposhughulikiwa, zinaweza kuwa na madhara kama vile kusononeka moyo, kutojua la kufanya na kuiathiri afya ya akili.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 148), mhusika Mrima anadhihirisha kuwa majukumu ya mwanaume katika jamii za kiafrika hayajabadilika. Mwanamume ndiye anayestahili kutafutia familia yake riziki na kuboresha maisha ya wanawe na sio mke kushughulikia suala hiyo. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mwanaume ni mkimujamii anayepaswa kujiunga na wanaume wengine kukidhi hitaji la jamii la chakula, mavazi na malazi kulingana na matakwa ya jamii yake. Hali hii, inawafanya wanaume kuathirika kihisia na kuwa na msongo wa mawazo iwapo hawana uwezo wa kukimu mahitaji ya familia yao. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi katika mfano ufuatao:

> Ingawa Mangwasha alitamani mumewe kurejea nyumbani, Mrima alikuwa na tatizo. “Hamwoni **kwamba mila hairuhusu mie nikatunzwe na mke? Au mmesahau Mikatale ya utamaduni?** Mrima aliwauliza akina Lonare kumchukua kutoka hospitalini. “Siwezi Mrima, kuvunja mila kwenda kutunzwa kama mtoto, hamwoni sina kazi, sina chochote? Nitawapa nini watoto wangu? Mrima alijaribu kukaa karibu na wanawe. Wazo la kutoweza kuyaboresha maisha ya jamii yake lilimsababishia msongo wa mawazo. Aliyaona maisha kama kitabu cha matatizo. (Momanyi 2019: 148)

Kutokana na nukuu katika Momanyi (2019: 148), mhusika Mrima anaonekana kuwa katika njia panda ya ni vipi angeweza kuboresha maisha ya jamii yake. Madai haya yanabainisha kuwa **utamaduni, mila na desturi ni kizuizi kinachomnyima mwanaume kupata usaidizi wowote kutoka kwa mwanamke ili kukidhi mahitaji yake na familia**. Kwa mujibu wa Bly, R. (1990), kuwa mwanaume sio jambo rahisi hasa anapotakiwa kutekeleza majukumu ya kijamii mbele ya macho ya umma. Kulingana naye, wanaume hukaaa kimya na hukosa kuonyeshana dhalimu na matatizo wanayopitia. Hii ni kwa sababu katika jamii mwanaume hapaswi kuonyeshana unyonge wake kwani udhaifu huo huonyeshwa na wanawake. Wanaume hufanywa kama “wafungwa” yaani wanakuwa huru kimwili lakini wamefungwa na fikra zao, hali zao za kiuchumi, hisia zao na hata utamaduni wa jamii yake.

Hatua ya Mrima katika Momanyi (2019: 148), ya kukataa kusaidiwa na Mkewe Mangwasha kwa sababu ya mila na desturi ya jamii yake, inasadifiana na maelezo katika Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Nadharia hii husisitiza kwamba fikra za wanajamii humuona mwanamume akiwa na hadhi ya juu kuliko mwanamke. Kwa upande mwingine, kutokana na utaratibu wa mfumo wa kuumeni kuwa kutafuta riziki ni kazi ya mume pekee; mwanamume anaonekana kuathirika hasa kisaikolojia Hali hii ndiyo inamfanya Mrima kusongwa **na mawazo ya kutoweza kuyaboresha maisha ya jamii yake.** Haoni ni vipi mwanamke anaweza kutekeleza jukumu ambalo tangu zamani ni la mume. Mume ndiye anafaa kuajiriwa au kufanya biashara ili apate pesa za kununua chakula na mavazi, kulipa karo na kugharamia mahitaji yote ya mke wake na watoto.

Vilevile, kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 148), imebainika kuwa mila ya jamii ya Mrima ni kikwazo kikubwa cha yeye kukubali kutunzwa na Mangwasha mkewe. Anaonekana kusongwa na mawazo ya kutojua atawapa watoto wake nini kwa sababu hana kazi. Kulingana na utafiti uliofanywa na Matheka. B. (2021), anaeleza kuwa wanawake huwa na mtazamo chanya kuhusu wanaume. Katika utafiti wake, Matheka anamsawiri mwanamke kama kiumbe anayetarajia mwanaume adumishe hadhi yake ya juu kwa kukidhi mahitaji ya familia yake vizuri. Anaeleza haya kupitia mwanamke wa miaka 32 anayeitwa Mukami. Mwanadada huyu anadai kuwa mume sio suti, ni jasiri. Yaani, mume ni ngao ya mkewe, watoto wake na familia yake. Anaendelea kusema iwapo mwanaume atapungukiwa na ujasiri na uwezo wa kifedha basi, mwanaume huyo sio kigezo bora cha kukimu mahitaji ya familia yake. Kwa hivyo, tunaweza eleza kuwa ajira ni muhimu kwa binadamu yeyote. Mtu anapokuwa hana ajira anapata msongo wa mawazo. Hii ni kwa sababu hapati marupurupu ya kukidhi mahitaji ya familia yake. (Maelezo yetu).

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 179), inabainika kuwa usaliti wa kimapenzi unachangia kusononeka kwa moyo kwa baadhi ya wanaume. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mwanaume aliumbwa akiwa na uwezo wa kutunga sheria na kudhibiti, mwanamke na familia yake. Kulingana na Connel, R. (1987), wanawake wengi waliogopa hata kuchukua hatua muhimu kuhusu maisha yao. Kwa namna hiyo, walionekana kuwa tayari kuhatarisha maisha yao ilimradi wasitende kinyume na sheria za waume wao. Aidha, Bly, R. (1990), anasema kwamba misingi hiyo ya kijana wa kiume kuwa na mamlaka ya kumdhibiti mwanamke ampende imebadilika katika karne ya ishirini na moja. Mwanamke wa karne hii anauwezo wa kuamua atampenda nani, na atampenda kwa misingi ya hisia za mapenzi, uwezo wa kuwa na pesa au la. Mabadiliko hayo ya mwanamke yanashusha thamani

ya mwanaume na kumfanya awe na mgogoro wa kisaikolojia na msongo wa mawazo. Maelezo haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> "Ngoswe, mie ninahisi uchungu mno moyoni. Mambo ya Darwin sina time nayo wakati huu." "Pole my friend. Ulimrambisha Cheiya bungu la asali, sasa anachonga mzinga. Usikubali ujana wako ukafukuzwa na uzee haraka hivyo. Kwani wasichana wameisha duniani? Wako tele fungu shilingi. Bora uwe na senti tu," alitamka Ngoswe. "Najua huelewi ninavyohisi kwani hujui mapenzi n'nini. Hujawahi kufumwa na mshale wa mapenzi hata siku moja. Utakufuma vipi nawe unawabadilisha kila dakika hata usijue umpendaye? Usitamke lolote kuhusu mapenzi kwani hujui ni kitu gani," Mashauri alisema. (Momanyi 2019: 179)

Kutokana na nukuu katika Momanyi (2019: 179), inabainika kuwa usaliti na uchungu wa mapenzi unamzingua Mashauri kimawazo. Hali hii inatokana na kulaghaiwa kimapenzi na Cheiya aliyedhamini pesa kuliko mapenzi. Kauli ya Ngoswe kumuuliza Mashauri kuwa **"kwani wasichana wameisha duniani"** linazidi kumpa Mashauri lindi la mawazo. Kulingana na Mashauri, Ngoswe haelewi anavyohisi baada ya kusalitiwa na mtu aliyemdhamini. Mashauri anahisi hadhi yake kama mwanaume imeshushwa chini. Jambo linalomfanya kuapa hatawai penda tena. Kwa hivyo, usaliti wa mapenzi huacha maumivu makali kwa anayesalitiwa kiasi cha kufa moyo. Kusalitiwa kwa Mashauri na Cheiya kunajengeka katika misingi ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Kwa mujibu wa Wells na Holland (2001), jukumu la mwanamke katika familia na mapenzi ni kuwa mwenye huruma na aliye na usaidizi wa kihisia kwa familia yake. Vilevile, wanaeleza kuwa jukumu la mwanamume katika familia na hata katika mapenzi ni kuwa kiongozi mkakamavu, anayejua jinsi ya kupata chochote anachokitaka. Ikiwa mpangilio huu utapanguliwa au kubadilishwa kwa njia yoyote ile, basi familia, mapenzi ya dhati kama asasi haitatekeleza majukumu yake vizuri au pengine inaweza kuporomoka, hivyo kutisha hali imara ya jamii nzima.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 98), mzazi wa kiume anaonekana kusongwa na mawazo ya kutofaulu kwa wanawe wa kiume. Kulingana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, ubabe, ushindi na ukakamavu wa mwanaume hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hata hivyo, katika jamii kuna baadhi ya wanaume ambao hushindwa kudhihirisha ubabe na ushindi wao katika asasi zote za maisha ya binadamu (Bly, R. 1990). Jambo hili linawafanya waonekane kwa

mtazamo hasi na kuwafanya wawe na msongo wa kimawazo. Tunaweza kupata maelezo zaidi katika mfano ufuatao:

> Jambo moja tu ndilo lililotia doa kuridhishwa na maisha kwa Mark Bagite. Nalo lilikuwa wanawe pacha, yaani Mwongi na Rejwa. Licha ya pesa nyingi alizomwaga kuwapeleka shule bora za kibinafsi, hawakufanikiwa masomoni. (Mbatiah 2018: 98)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 98), mhusika Meja Bagite anasononeshwa na matokeo duni ya masomo ya wanawe Mwogi na Rejwa. Hali hii inampa mushkeli Meja Bagite katika mchakato wa kutamani wanawe wapite masomoni. Hata hivyo, Mwogi na Rejwa licha ya kupelekwa shule bora za kibinafsi zilizogharimu pesa nyingi, hawakufanikiwa masomoni. Kutofanikiwa kwa Mwongi na Rejwa katika masomo na maisha yao kunashusha ubabe ambao unahitajika kwa wanaume katika asasi mbalimbali za kijamii kama vile dini, elimu na kadhalika.

### 3.3 Mauaji

Mauaji kwa macho ya sheria ni matendo ya mtu mmoja au zaidi yanayosababisha kifo cha mtu mwingine. Uuaji kwa maana hiyo unahitaji tendo la mtu ambalo limelengwa, unaweza kutokana kwa bahati mbaya, kwa kutojali au kupuuza hata bila nia ya kusababisha hasara, au kwa kusudi la kuondoa uhai wa mtu (Card, 2006). Mauaji ni uhalifu unaofanywa dhidi ya ubinadamu wa kutamatisha maisha ya mtu au watu na unatambuliwa kama kosa chini ya sheria za taifa na kimataifa. (Tafsiri yetu)

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah: 2018) kuna wezi wa jinsia ya kiume kama vile, Nyangwe anauliwa na Okuti mwizi mwenzake wa kiume. Kulingana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, ili mwanaume adhihirishe uwezo wake wa kuwa na pesa nyingi, anaweza sombwa na tamaa ya pesa. Jambo hili linamfanya akatishe uhai wa watu wengine. Anafanya hivi kwa kusaliti makubaliano kati ya kundi la wezi ya kugawana pesa walizoiba. Madai haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> **Wameniua! Mungu mmoja. Wameniua na pesa wamechukua**. Mtu aliyefanya kazi ya polisi kwa robo karne hakuhitaji maelezo zaidi, wala hakuuliza maswali. Kiguto alielewa kwamba **msemaji alikuwa mmoja wa wezi ambao walikuwa njiani kwenda kugawana ngawira ya shilingi milioni tatu.** Huko mbele katika barabara ya lami iliyonyooka, taa za gari zilimulika migongo miwili ya wanaume

> waliokuwa wakikimbia kuelekea kwenye mahame ya jumba lililochomeka miezi kadha iliyopita. (Mbatiah 2018: 11)

Kutokana na nukuu katika, Mbatiah (2018: 11), sauti ya mwizi wa jinsia ya kiume ikilia, "**Wameniua! Wameniuwa!** Inadhihirisha kuwa kichocheo kikubwa cha mauaji ya wanaume ni tamaa ya pesa. Mhasiriwa wa wizi Nyangwe anadanganywa na wezi wenzake kuwa watagawana pesa walizoiba badala yake anauliwa na kumyima nafasi ya kupata pesa hizo na pia ananyimwa haki yake ya kuishi. Hali hii inaonyesha wezi hao wamekegeuka na wanapatwa na tamaa ya pesa. Hii ndiyo sababu kuu ya wao kuamua kutekeleza ukatili ule kwa mwenzao.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatia 2018: 12), babake mdogo Kiguto anakosa huruma kwa kutekeleza mauaji ya wezi wanaume. Tunaweza kupata maelezo zaidi katika mfano ufuatao:

> Babake mdogo Kiguto aliingia kwenye ganjo akanyatia, akatoa bastola yake na kuishika vizuri kwa mkono wa kulia na akawapiga risasi. Akachukua ngawira yake ya pesa milioni tatu akawa tajiri, akaficha wizi kwa kuwaua wezi na hakuripoti kesi hiyo kwa polisi. (Mbatiah 2018: 12)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 12), mhusika Kiguto anashangazwa na ukatili wa babake mdogo Kiguto. Anaonekana akiwapiga wezi hao risasi. Kitendo hiki kinamfanya awe muuaji. Anakiuka haki ya kuishi ya wezi hao wanaume. Zaidi ya hayo, anakosa kuripoti kesi hiyo kwa polisi. Jambo linalomchochea ageuke kuwa muuaji anayeongozwa na tamaa ya kupata utajiri haraka. Kulingana na kauli ya Kiguto babake mdogo anachukua ngawira yake ya pesa milioni tatu kisha kununua nyumba katika mtaa wa Igune na kuikodisha. Msowoya. T. (2021) anaeleza kisa ambacho mchungaji mmoja nchini Tanzania, wilaya ya kilolo mkoani Iringa, aliuliwa na shemeji yake. Kwa mujibu wa komanda wa polisi alisema, inadaiwa mchungaji huyo alikuwa ameuza baadhi ya mazao yake, hivyo alikuwa na fedha zaidi ya shilingi milioni mbili. Kwa hivyo chanzo kikubwa cha mauaji hayo ni tamaa ya mali. Hii ni kwa sababu huyu mchungaji alikuwa na fedha ambazo huyo mtuhumiwa alizipora kisha akamuua. Hii inadhihirisha kuwa mambo anayoandika mwandishi yanafanyika katika jamii ya Kiafrika.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 19), inabainika kwamba ushindani katika biashara na chuki ni vichocheo vingine wanaume wanatumia kusababisha mauti ya wanabiashara wa kiume wenzao. Kulingana na Nadharia ya Uwezo-

Mkuu wa Kiume, kuna baadhi ya wanaume ambao ni wababe kuliko wanaume wenzao. Ubabe huu wa wanaume unawaathiri wanaume wengine kwa njia hasi ya kutowajali. Jambo hili linasababisha ukiukaji wa haki ya kuishi ya wanaume wasio wababe. Maelezo haya yanabainika kwa kurejelea mfano ufuatao:

> **Kifaru alikuwa tisho kwa Sagilu kutokana na ufanisi wake katika biashara ya Saruji. Chuki ya Sagilu kwa Kifaru sasa ilipaliliwa makaa**, ikawaka mithili ya moto wa kichaka. **Hapo ndipo alipomtuma sihaba kumwangamiza Kifaru.** Kwa upande wake, **Kifaru hangekataa vishawishi vya Sihaba aliyekuwa mrembo ajabu**. Siku aliyotumwa kutekeleza wajibu huo alijopondoa akaondoka na tajiri huyo. Walienda kujivinjari katika hoteli moja kubwa iliyokuwa nje ya mji wa Taria. Siku **ya pili**, tajiri **alipatikana** katika chumba cha hoteli **akiwa mfu**. (Momanyi 2019: 19)

Kutokana na maelezo katika Momanyi (2019: 19), inabainika kuwa, Sagilu anafahamu Kifaru huwatazama wanawake warembo kama chombo cha kustarehe jambo linalosadifiana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Hivyo, Sagilu anamlipa Sihaba aanzishe uhusiano wa kimapenzi na Kifaru na kisha amuue. Sagilu alijua hii ilikuwa ni njia mwafaka ya kuondoa kizuizi cha ushindani katika biashara yake ya saruji.

### 3.4 Kupata Malezi Yasiyofaa

Malezi ya watoto ni njia ambayo huwawezesha wazazi na watoto kushirikiana katika hali zote za kiakili, kidini na kijamii Deater na Petrill (2006). Anaendelea kusema kwamba malezi hayo humwezesha mtoto kuishi katika mazingira bora na kujenga uhusiano mwema na wazazi na jamii yake. Katika hali nyingine, Malezi yasiyofaa ni mafundisho yasiyofaa yanayotolewa kwa watoto na wazazi au walezi wake au jamii inayomzunguka na kuwafanya kutopata maadili mema, kutokuwa na maisha mema na kukosa vitu vya msingi vinavyoweza kumsaidia katika maisha. (Tafsiri yetu).

Aidha, Getao (2016) anaeleza kuwa baadhi ya malezi yasiyofaa ni malezi ya kudekeza. Anasema kuwa katika aina hii ya malezi, wazazi huepuka migogoro na mapambano yoyote na watoto wao. Walezi wanaotumia mbinu hii huwapenda watoto wao kupita kiasi. Watoto hufanya mambo yanayowafurahisha bila wazazi wao kujali athari za mambo hayo. Mbinu hii hutumiwa sana na wazazi wenye ufanisi wa kifedha, ambao mara nyingi huwaona watoto wao kama warithi wa mali yao. Wazazi wanaotumia mbinu hii ya kupendelea huwapa watoto wao pesa nyingi. Jambo hili huwaharibu watoto kwa kuwapa vitu ambavyo hawavihitaji na

kukosa kuwapa mwelekeo mzuri wanaohitaji. Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 114), mhusika Meja Bagite anawapa pacha wake Mwongi na Rejwa malezi ya kudekeza. Tunapata hali hii katika mfano ufuatao:

> Malezi ambayo baba yao alijua ni kuwapa watoto pesa. Kila mwezi, aliwatumia kichele kilicholingana na mshahara wa tarishi wa shule. Mbali na kuwapa hela nyingi, aliwanunulia kila walichotaka. Kwa hali hii, hawakuthamini hela na walizitumia ovyoovyo. Ziliwatumbukiza katika maovu chungu zima. Hata baba yao alipowagombeza siku ile walipoadhibiwa kwa kutoroka shuleni, walijua kwamba hasira zake hazikuwa za kudumu. Hata tishio la kutowatumia kichele hakulitekeleza. (Mbatiah 2018: 114)

Kutokana na maelezo katika Mbatiah (2018: 114), mhusika Meja Bagite anawalea watoto wake (Mwongi na Rejwa) kwa kuwapa pesa nyingi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mwanaume huwa ni kiongozi ambaye ana pesa nyingi. Hata hivyo, uzoefu huu wa Mark Bagite kuwadekeza wanawe, unawafanya watumbukie katika maovu kama vile kutoroka shuleni. Tabia hizi zinatokana na baba yao kutowaadhibu na hawaelezi njia mwafaka wanazofaa kufuata ili wawe na nidhamu bora. Kwa mujibu wa Ngwiri (2008), kuna tofauti kati ya wazazi wanaotumia mbinu ya kudekeza na wanaotumia mbinu ya kupendelea. Anasema kuwa wazazi wanaotumia mbinu ya kudekeza hawaweki sheria zozote za kuwaongoza watoto wao. Watoto hufanya watakacho. Hii ndiyo sababu Mwongi na Rejwa wanajua kuwa hasira za baba yao hazitadumu hata baada ya wao kutoroka shuleni. Tabia hizi zinatokana na baba yao kutowaadhibu na hawaelezi njia mwafaka wanazofaa kufuata ili wawe na nidhamu bora.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 265), mzazi wa kiume anaonekana akimhusisha mwanawe wa kiume katika biashara haramu inayomfanya awe mhuni na mfisadi. Kulingana na Brooks (2012), anaeleza kuwa wazazi ndio huchangia pakubwa katika malezi ya mtoto. Anaeleza kuwa mzazi anaweza kuwalea watoto wake ili wakue katika maadili, nidhamu na hatimaye kuwa raia mwema kwa taifa lake au akose. Suala la wazazi wa kiume kuwashirikisha watoto wao wa kiume katika hulka mbaya kama vile, kuhusisha watoto wao wa kiume kufanya biashara haramu sio malezi mema. Suala hili ni kikwazo cha ustawi wa wavulana hao. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo- Mkuu wa Kiume, mwanaume ni mwenye mamlaka. Hata hivyo, kuna baadhi ya wazazi wa kiume wenye mamlaka wanatumia madaraka yao vibaya. Maelezo haya, yanabainika katika mfano ufuatao:

> Lonare alimtajia Ngoswe biashara haramu alizofanya pamoja na babake Mtemi Lesulia na watu watajika wanaoshirikiana nao. Isitoshe, alimtajia mitandao yote ulimwenguni na jinsi anavyonufaika huku akiwadhuru wavulana wa shule. (Momanyi 2019: 265)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 265), mhusika Mtemi Lesulia hakuweza kumpa mwanawe malezi yaliyostahili.  Kulingana na kauli ya Lonare, Ngoswe anashiriki katika biashara haramu ya dawa za kulevya ambazo zilisambazwa nchini kwa siri. Ijapokuwa sheria kali zilipitishwa nchini Matuo kuhusu dawa hizo, hazikuzingatiwa kutokana na ushawishi wa mabwenyenye waliohujumu sheria za nchi kwa manufaa yao.  Mathalani, Ngoswe ambaye ni mtoto wa Mtemi Lesulia ndiye anayejua njia zote za kupata na kusambaza dawa za kulevya. Ingawa aliweza kuagiza na kuuza dawa hizo, kamwe yeye hakuwa mraibu wa kubwia mihadarati. Badala yake, marafiki zake waliokataa shule ndio walikuwa wakitumia dawa hizo za kulevya. Ingawa kulikuwa na sheria kali zilizopitishwa na nchi kuzuia biashara hiyo ya mihadarati, Ngoswe aliweza kufanya biashara hii bila kubughudhiwa kwa kuwa alikuwa mtoto wa kigogo wa nchi ya Matuo. Tabia hii ya Mtemi Lesulia kumhusisha mwanawe katika biashara haramu, inasadifiana na Nadharia ya Uwezo- Mkuu wa Kiume, kuwa mwanamume ni mwenye mamlaka na nguvu nyingi katika jamii. Mtemi Lesulia anatumia madaraka yake ya Utemi vibaya. Vijana ambao wangekuwa wazalishaji mali kama vile Ngoswe na marafiki wake wanaishia kuwa waraibu wa dawa za kulevya na wanakosa kuenda shule. Wakati haya yanafanyika serikali ya Mtemi Lesulia inayafumbia macho tu.

Aidha, uozo wa namna hii umeangaziwa na mwandishi Momanyi, ili wananchi waamke kutoka usingizini na kupiga vita biashara hizi haramu na matendo mengine ya ovyo kama haya yanayojitokeza katika jamii zetu. Kulingana na uchunguzi uliofanywa na Wairimu. W. (2021) ulibaini kuwa, wavulana wengi katika kaunti za Nairobi, Lamu, Isiolo hawakuripoti shuleni kwa sababu ya kutekwa na uraibu wa dawa za kulevya. Kadhalika, uchunguzi huu unabainisha kuwa hata viongozi hawajafurahishwa na matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana. Hali hii inabainika kupitia Athman Sharif na mbunge Mwakilishi wa Wanawake eneo hilo, Bi Ruweida alisema hajafurahishwa na jinsi vijana wengi kote Lamu wanavyoendelea kutumia mihadarati. Bw Sharif alieleza haja ya idara ya usalama eneo hilo kuwasaka na kuwachukulia hatua kali za kisheria wasambazaji wa mihadarati ili wasiendelee kuharibu maisha ya vijana.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 148), mzazi wa kiume hajihusishi na malezi ya mwanawe wa kiume. Malezi ya kutojihusisha ni aina ya malezi ambapo wazazi hawashughulikii wanao, hawachangii katika malezi ya watoto wao (Ashworth, 2017). Anazidi kueleza kuwa wazazi wanaotumia mbinu hii ya malezi huwatelekeza watoto wao. Hawachangii kwa vyovyote vile katika malezi ya watoto wao. Anaeleza kuwa kuna sababu zinazowafanya wazazi kuwatelekeza watoto wao. Hizi ni pamoja na kukosa muda na watoto wao, kutumia muda mwingi kazi, matatizo ya nyumbani na matumizi pombe na ya dawa za kulevya. Katika aina hii ya malezi, mzazi hajihusishi na maendeleo ya mtoto wala hana malengo yoyote ya mtoto. Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 148), Mrima anakosa kujihusisha na malezi ya mwanawe Sayore. Anakosa baba wa kumwongoza kwani analelewa na mama yake Mangwasha. Maelezo haya yanabainika kwa kurejelea mfano ufuatao:

> Sayore alibaki kumtazama baba yake kama mgeni aliyewasili kwao. Hata baada ya mama yake kumweleza yule alikuwa baba yake ilimchukua muda mrefu kumkubali mgeni huyo. Mrima aliwazia maisha ya ulevi aliyopitia akatamani kuyarambukia tena hasa pale alipopita karibu na vibanda vya pombe. (Momanyi 2019: 148)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 148), mhusika Mrima hajihusishi na malezi ya mwanawe Sayore. Hii ni kwa sababu alikesha katika ulevi na kusababisha Sayore kumsahau na kumwona kama mgeni. Kukosekana kwa Mrima kama baba mzazi katika maisha ya Sayore kunamfanya Mangwasha kuchukua jukumu la kuwalea wanawe. Kulingana na Bly, R. (1990), anaeleza kwamba hali ilivyo sasa ni kwamba, wanawake wameingia ulimwengu wa kiuchumi ambapo wanaajiriwa kazi na kuweza kuchangia katika jukumu la kukidhia familia. Mwanamume si tegemeo la pekee katika kukidhi familia na jamii. Hadhi ya mwanamume inashushwa. Yeye sio 'kichwa" cha familia tena kama anavyojengwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Hali hii, imeleta malezi ya kutojihusisha ya Mrima kwa mwanawe Sayore. Jambo hili limekuwa tishio kwa hadhi na utukufu aliopewa mwanamume kwa misingi ya jukumu na nafasi aliyotengewa na jamii kudhihirisha ubabedume. Hii ndiyo sababu Sayore anamwona Mrima kama mgeni badala ya baba mzazi.

### 3.5 Kukosa Kuendelea na Masomo

Kukosa kuendelea na masomo ni kukosa kukamilisha kipindi cha masomo kutokana na aidha, ulitima miongoni mwa wazazi, utoro wa wanafunzi au sababu nyingine ile kama kufungwa jela. (Tafsiri yetu)**.** Kulingana na Bwaya (2017) vijana wanaomaliza masomo yao kwa ngazi mbalimbali za elimu, wengi wanakosa nafasi ya kuendelea na masomo yao kwa sababu ya

mfumo rasmi wa elimu. Anaeleza kuwa mfumo huu wa elimu huchuja wanafunzi kuwa kuangalia sifa ya ufaulu. Hata hivyo, anaeleza kuwa mara nyingi vijana hukosa kuendelea na masomo kwa sababu ya kukosa ufadhili wa masomo yao au uwezo wa chini wa mapato ya wazazi wao. Anaeleza kuwa hali hii huwafanya vijana wengi kukata kiu ya kuendelea na elimu yao jambo ambalo huwalazimisha baadhi ya vijana kurudi mitaani kutafuta namna ya kuendesha maisha yao.

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 217), kuna wavulana wanakosa nafasi ya kuendelea na masomo yao. Kulingana na Hong, Y. (2019), baadhi ya wavulana wanaoachwa mayatima au bila walezi hawaendelei na elimu yao. Anazidi kueleza kuwa wavulana hao hupata changamoto ya kifedha jambo ambao huwafanya watafute kazi ili wakidhi mahitaji yao. Haya tunapata katika mfano ufuatao:

> Sijawahi kuona kioja kama hiki, ni kama mtu kukamilisha safari ndefu na ngumu, halafu badala ya kutamatisha avunjike moyo na kuanza kurudi. Itakuwaje mtu aliyepata matokeo bora ya mtihani aanze kufikiria kozi ya polisi? "Sababu ya mtu kumpoteza babake na mamake kufungwa?" Mbona naziona kuwa sababu nzito za kukufanya uendelee na masomo yako?" Aroni aliuliza kwa hamasa. "Dharura ndugu yangu. Nitapataje kawi ya kuendelea na masomo wakati mamangu anaozea gerezani?" Kiguto alirusha swali la balagha ambalo lilisheheni hisia kali. (Mbatiah 2018: 217)

Kutokana na mfano katika, Mbatiah (2018: 217), mhusika Kiguto anakata kiu ya masomo kwa sababu mama yake alikuwa gerezani na babake alikuwa ameenda jongomeo. Ingawa rafiki yake Aroni anamshawishi kuendelea na masomo ili apate nuru katika maisha yake. Kiguto anamkumbusha kuwa hana wa kumlipia karo na ndio maana anajiunga na kikosi cha polisi ili aweze kupata riziki. Hatua ya Kiguto kutaka kujiunga na kikosi cha polisi ili aweze kujipatia riziki, inajengwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, inayoeleza mwanamume anapaswa kutafuta riziki ili apate marupurupu ya kukidhi mahitaji yake.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 207), wavulana wengi wanaonekana wakikosa kuendelea na masomo kwa sababu wanatoka katika familia maskini na wana matatizo ya karo. Kulingana na Hong, Y. (2019), wavulana wengi badala ya kujiunga au kuendelea na shule, wanaishia kwenye ajira za utotoni, mara nyingi ni za unyonyaji, unyanyasaji, au katika mazingira hatarishi. Anaeleza kuwa wanafunzi maskini huwa hawana uwezo wa kuenda shule. Hii ni kwa sababu ya gharama zingine kama vile

kulipa nauli ya kwenda shule, sare na mahitaji mengine kama vitabu. Tunapata haya katika mfano ufuatao:

> Wewe siye Sailoki, kijana wa mzee Letemere? Unafanya nini hapa? Nakumbuka ulifanya vizuri sana katika mtihani wako wa kidato cha nne. Hata baba yako alifurahi sana. Ni kitu gani gani kilikuleta hapa? Lonare alimuuliza. "Aah! Matatizo ya karo. Nikaamua kuja kuzumbua riziki hapa." (Momanyi 2019: 207)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 207), wavulana wengi wanaonekana wakikosa kuendelea na masomo kwa sababu ya matatizo ya karo. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mwanaume ameumbwa akiwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto anazopata kwa ujasiri na ukakamavu. Vilevile, kulingana na nadharia hii mwanaume amepewa sifa angama ya kuwa yeye ni mtafutaji riziki. Hii ndiyo sababu Sailoki anaacha shule. Tunaelezwa Anaeleza kuwa ingawa ada imetolewa mashuleni, wanafunzi maskini na mayatima bado hawana uwezo wa kuenda shule. Hii ni kwa sababu ya gharama zingine kama vile kulipa nauli ya kwenda shule, sare na mahitaji mengine kama vitabu. Tunaelezwa kuwa Sailoki na wavulana wengine kutoka viungani mwa mji wa Taria waliajiriwa na Mtemi Lesulia katika shamba lake la Mkonge. Walifanya ajira hii duni ili wakidhi mahitaji yao. Sailoki anamuarifu Lonare kuwa licha ya yeye kufanya vizuri katika kidato cha nne hakuweza kuendelea na masomo kwa sababu ya umaskini katika familia yao. Kinaya ni kwamba babake Sailoki alifurahia matokeo yake lakini hakuwa na uwezo wa kugharamikia elimu ya juu.

### 3.6 Kukosa Chakula, Mavazi Na Malazi

Binadamu yeyote anapokosa kupata chakula, malazi mazuri na mavazi huwa amekosa vitu vya msingi vya kumfanya binadamu kuishi maisha bora. (Tafsiri yetu). Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, humchora mwanamume kama mtafuta riziki. Kwa mujibu wa Connel (1987), mwanaume anapaswa kujiunga na wanaume wengine kukidhi hitaji lake na la jamii kama vile la chakula, mavazi na malazi. Hali hii inawasukuma baadhi ya wavulana na wanaume kufanywa kama watumwa na matajiri ambao huwafanyisha kazi sugu na malipo duni.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 203, 206), kuna wavulana kama vile Sailoki ambao wamekosa chakula, mavazi na malazi. Wavulana hao wametumikishwa na Mtemi Lesulia hadi miili yao ikadhoofika. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kuna baadhi ya wanaume wanatumia madaraka yao vibaya kwa manufaa yao binafsi.

Wanaume hawa kama vile Mtemi Lesulia, hawajali athari mbaya zinazowapata watu wengine. Tunaweza kupata maelezo zaidi kwa kurejelea mifano ifuatayo:

> "Ama kweli, miaka ya Seyyid Said imerudi. Tazama jinsi wavulana wanavyofungishwa mabunda ya makonge kubeba. **Hata migongo yao imepinda. Utumwa wa kizazi kipya**. (Momanyi 2019: 203)
>
> Nyuso zao zilisikitisha. Walivaa mararu huku wengine wakionekana kuadhibiwa na njaa. Mikono yao michanga iliota visuguru **kutokana na kazi ile ngumu.** Miili ya wengi wao ilikuwa imefisidiwa na funza usiseme chawa. Kutembea ikawa vigumu kwa baadhi yao. (Momanyi 2019: 206)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 203), inabainika kuwa wavulana walikosa chakula kwani nyuso zao zinaonyesha wamekosa lishe. Kadhalika, wavulana hawa wanavaa nguo zilizochakaa. Hali kama hii inadhihirisha matatizo wanayopata. Vilevile, migongo ya wavulana hawa imepinda na mikono yao michanga imeota visuguru kutokana na kazi ngumu wanayofanya. Hii inadhihirisha walikosa haki ya maisha mazuri kama watoto na ndio maana wakafanya kazi sugu ili kutafuta riziki wakidhi mahitaji yao.

Vilevile, katika Momanyi (2019: 206), inaonekana wavulana hao hawakupata mazingira masafi. Hali hii inadhihirishwa na miili yao iliyokuwa na chawa na funza. Jambo hili linafanya baadhi ya wavulana hao kuathirika kiasi cha haja kama vile kushindwa kutembea. Utafiti uliofanywa na Nyamemba (2012), kuhusu changamoto wanazopitia vijana unasadifiana na matatizo wanayopitia vijana wa kiume katika riwaya ya *Nguu za Jadi* (2019). Anaeleza kuwa jamii inapokosa kuwatosheleza vijana mahitaji muhimu kama vile chakula, mavazi na malazi huwafanya wakalemewa na hata wakaangamia kabisa.

### 3.7 Ugonjwa wa Afya ya Kiakili

Ugonjwa wa kiakili ni tatizo la kiakili ambalo husababishwa na mfadhaiko baada ya mtu kupata tukio ama matukio mabaya yanayomtia hofu kuu, kiwewe au wasiwasi. (Tafsiri yetu). Kadhalika, ugonjwa wa afya ya kiakili ni hali ya kutokuwa sawa kiakili na kisaikolojia. Hali hii humfanya mtu asiwe timamu na ashindwe kutatua matatizo mbalimbali yanayomkabili yahusishayo msongo wa mawazo katika maisha, shughuli za uzalishaji na mchango wa mtu husika katika jamii. (Fasiri yetu).

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 219), kuna wahusika wanaume wameathirika kutokana na ugonjwa wa kiakili. Tunaweza kupata maelezo zaidi katika mfano ufuatao:

> Walipofika, walipigwa na butwaa. Sagilu alikuwa akiongea peke yake. Mara ainame na kubong'oa, mara apige makofi na kucheka peke yake. Alipobong'oa, watoto walimcheka huku wakimfuata na kumtania. "Mama Yangu! zimemruka. Kichaa kimemvaa. Amekuwa majununi. Maskini mzee wa watu," alitamka Mbungulu kwa huzuni. "Ukifanyia watu maovu, haya ndiyo hukufika. Akili zitaenda likizo ndefu, nawe utabaki kucheka na kivuli chako. Msiba wa kujitakia huu. Hauna kilio." Mangwasha alitamka. "Ni ugonjwa gani huo?" Mashauri aliuliza. "Aaah, ni ugonjwa wa akili kuchanganyikiwa tu." (Momanyi 2019: 219)

Kutokana na maelezo katika, Momanyi (2019: 219), inabainika kuwa mabadiliko ya tabia ya Sagilu yanatokana na kufadhaika akili. Watu walio na tabia ya kiajabu ajabu, iitwayo *fronto-temporal dementia* huwa wanacheka ovyo hasa wanapotizama au kusikiliza taaarifa mbaya au wanapoangalia maisha yao ya kibinafsi, miaka tisa kabla ya kupatikana na maradhi hayo (Izugbara, C. 2005). Hali hii inadhihirika wakati Sagilu alipoonekana akipiga makofi na kucheka peke yake jambo lilowafanya watoto wamfuate wakimtania. Watafiti hao wanasema kuwa kuongezeka kwa vitendo viovu, kunaweza kuwa dalili za mwanzo za matatizo ya akili. Madai haya yanadhihirishwa kupitia kauli ya Mbungulu akisema mja akimtendea mja mwenzake matendo mabaya malipo yake ni kupata ugonjwa wa akili.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, Momanyi (2019: 146), kuna wanaume wanaougua ugonjwa wa akili kutokana na wao kutobugia pombe kwa muda. Anaendelea kudai kuwa matumizi ya pombe haramu ni kikwazo cha ustawi wa jamii. Pombe haramu huathiri afya ya watumiaji pamoja na kuzorotesha ustawi wa familia. Inabainika kwamba Mrima hana utulivu wa akili. Mrima ananusurika kifo kutokana na uraibu wa pombe. Hali hii inasababishwa na yeye kutokunywa pombe kwa kipindi kirefu jambo linalomfanya alazwe hospitali ili apate matibabu. Kuna watu wanaweza kuwa na hamu ya kunywa pombe kila wakati na kupata athari mbaya ya mwili wakati wa kuacha au kutokunywa kwa muda (Rehm, 2009). Anaendelea kusema kuwa dalili kama vile ukosefu wa amani, wasiwasi, kujeruhiwa na kuumiza wengine zinazoonyesha shida ya kunywa pombe sio ishara ya udhaifu bali zinaweza kutibiwa ili mtu awe katika hali ya kawaida ya binadamu. Kutokana na maelezo haya, Mrima alipelekwa hospitali kupata matibabu ili kupunguza athari za pombe.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 238), kuna wanaume ambao afya yao hudhoofika kutokana na kusalitiwa na wafanyikazi wao wasioaminika. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Samaki mmoja akioza, huoza wote. Hadhi ya shule hiyo ilishuka sana. Haikuwa katika orodha ya kitaifa ya shule kumi bora. Jambo kama hili lilikuwa halijatokea kwa zaidi ya miaka thelathhini. Mchungaji John aliathirika kiasi kwamba alipata ugonjwa wa afkani, akalazwa hospitalini. (Mbatiah 2018: 238)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 238), mchungaji John, anakuwa punguani hadi analazwa hospitali. Hali hii inasababishwa na hadhi ya shule kudidimia katika masomo kwani haikuwa katika orodha ya kitaifa ya shule kumi bora. Hii inatokea kwa sababu mwalimu mkuu alisajili Mwogi na Rejwa katika shule hiyo baada ya kufisidiwa na baba yao Mark Bagite. Watu ambao hufisidi jambo mbaya ili wao wafaidike huchangia athari mbaya kwa wasimamizi wa taasisi za kielimu, kidini na kisiasa Mwenda (2020: 34). Hali hiii ndiyo iliyofanya mchungaji John kuwa majununi kwani shule yake haijawahi kuwa na wanafunzi wanaoanguka mtihani na kudunisha hadhi ya shule yake.

### 3.8 Kupoteza Imani na Polisi

Kupoteza imani ni hali ya kuwa na hofu na shaka kuhusu uwezekano wa jambo fulani. (Maelezo yetu). Mtu yeyote anaponyimwa haki ya kuhudumiwa na kiongozi wake au vyombo vya dola, katika asasi mbalimbali za jamii, imani yake ya kupata huduma hiyo kama vile usalama na elimu huwa inafifia. Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 95), kuna wanaume ambao wamepoteza imani yao na polisi. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi katika ufuatao:

> “Hatuna haja na ulinzi wako. Tutalindwa na Mungu tokomea huko. Heri ya mrama kuliko ya kuzama.” Alinena Sagura aliyekuwa mtulivu wakati huu wote. (Momanyi 2019: 95)

Kutokana na nukuu katika Momanyi (2019: 95), mazungumzo kati ya Sagura na polisi yanaonyesha hana imani na ulinzi wa polisi. Kwa Mujibu wa Binyanya (2014), hisia za mtu aidha chanya au hasi haziwezi kufichika kwani hisia hizo huonyesha imani ya kibinafsi kwa mtu fulani. Anaendelea kusema kuwa mtu anapokuwa na hisia hasi huwa ana mbadala kidogo au hana njia yoyote ya kurekebisha hali mbaya. Kwa hivyo, Sagura amekata tamaa na imani yake kuhusu ulinzi wa polisi imedidimia. Kulingana naye, ana hofu na hawezi pata

usalama wa maisha na mali yake kutoka kwa polisi. Hali hii inamsukuma kuamini ni Mungu tu anayeweza kuwalinda.

**3. 9 Kupoteza Kazi**

Kulingana na Farber (2010), kupoteza kazi maana yake ni kumalizika kwa mahusiano ya kikazi baina ya mwajiri na mfanyakazi au mwajiriwa. Anaendelea kusema kuwa mwajiri anapositisha ajira ya mfanyikazi huwa amesukumwa na sababu fulani kama vile kustaafu, kugoma, mwenendo mbaya kazini, kumalizika kwa mkataba wa ajira, teknolojia mpya, kupunguzwa kazi na utovu wa nidhamu. Hali hii hufanya kusitishwa kwa huduma ambazo mtu alikuwa akitoa katika mahali pake pa kazi.

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 281), kuna wanaume kama vile Mark Bagite ambao hawawajibiki katika kazi zao. Wanume hao wana mwenendo mbaya unaofanya kazi zao zisitishwe. Kulingana na nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, wanaume hutakiwa wawajibikie kazi yao. Iwapo hawatawajibika, thamani yao katika jamii huenda chini. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Wakati huu, Mark Bagite hakuwa na madaraka ya kuweza kubadilisha mahali pa kufanya kazi ili pawe jijini karibu na nyumbani. Hawakumaliza hata mwaka mmoja kazini. Mwongi alipigwa kalamu kwa kupoteza silaha yake akiwa mlevi kazini. Naye Rejwa alimwaga unga kwa kumpiga bosi wake. (Mbatiah 2018: 281)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 281), inabainika kuwa ulegevu na utovu wa nidhamu unadhihirisha Mwogi na Rejwa kama wanaume ambao hawawajibikii kazi zao. Tabia ya Mwogi kubugia pombe akiwa kazini kunachangia yeye kukosa umakinifu wa kulinda silaha ya kazi, jambo linalofanya huduma zake kusitishwa na mwajiri wake. Vilevile, Rejwa anafutwa kazi kwa kumpa kichapo mkubwa wake kazini. Tabia hii ya Rejwa inadhihirisha amekosa heshima kwa mwajiri wake. Wazazi walio na hadhi ya juu hufanya juu chini kuakikisha kuwa watoto wao wamefanikiwa maishani (Miller, 2015). Kwa hivyo, tabia hii huwafanya kuhisi wamedekezwa na huwa huru kufanya watakacho na hawaweki sheria za kuwaongoza na kuna uwezekano wa watoto hao kuwa watovu wa nidhamu. Maelezo haya yanadhihirisha, awali Mark Bagite alikuwa na uwezo wa kuwabadilishia mahali pa kufanya kazi lakini madaraka hayo yalipokwisha, wanawe walikiuka sheria za ajira na wakapoteza kazi zao kwani hawakuzoea kufuata sheria zozote.

### 3. 10 Hitimisho

Katika sura hii, tumejikita katika kuchunguza namna wanaume wanavyoathirika kutokana na matendo ya ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* na *Nguu za Jadi* za Mbatiah (2018) na Momanyi (2019) mtawalia. Athari hizo ni pamoja na msongo wa mawazo, mmomnyoko wa maadili, mauaji, malezi yasiyofaa, kukosa kuendeleza masomo, kupoteza imani na polisi, ugonjwa wa kiakili, kupoteza kazi na kukosa chakula, mavazi na malazi.

Vivyo hivyo, imebainika kuwa matendo ya wahusika kama vile matumizi ya pombe, dawa za kulevya, kuvuta bangi, tamaa ya mali, na umaskini ni baadhi ya vichocheo vilivyochangia katika kukandamiza jinsia ya kiume kama ilivyo kati ya Ngoswe, Mtemi Lesulia na Sagilu katika riwaya ya *Nguu za Jadi* (2019) na Kim na Dan katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018).

Vilevile, inabainika kuwa mwanamume anaposhindwa kutekelezaa majukumu yake, anakuwa na wasiwasi ambao unashusha hadhi yake katika jamii. Hivyo, unyonge huu unafanya mwanamume kuathirika kihisia kama vile Kiguto katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) na Mrima katika riwaya ya *Nguu za Jadi* (2019).

## SURA YA NNE

## MIKAKATI AMBAYO WANAUME WANATUMIA KATIKA HARAKATI ZA KUPIGANIA UKOMBOZI WAO KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI: *NJOZI YAPATA MTENZI* (2018) NA *NGUU ZA JADI* (2019)

### 4. 0 Utangulizi

Katika sura hii tunatathmini mikakati ambayo wanaume wanatumia katika harakati za kupigania ukombozi wao kutokana na ukandamizaji katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah, 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019). Kwa mujibu wa Connel, R. (1987), mtazamo wa jamii kumhusu mwanamume hubadilika kwa sababu miili na akili ya wanaume pia hubadilika katika kipindi cha maisha. Maelezo haya yametusaidia kudhihirisha mabadiliko ya jamii hutokea katika asasi za kijamii kama vile elimu, siasa, na uchumi. Hali hii huzua mwamko mpya wa wanaume kutafakari upya hali yao katika jamii ambapo wamo mbioni kujikomboa kutokana na mifumo ya kitamaduni, makundi kandamizi na mahusiano yao na wanajamii wengine.

Katika sura hii, baadhi ya mikakati ambayo tumebainisha ni pamoja na mkakati wa kukimbilia dini, mkakati wa kukomesha utumwa wa kisasa, mkakati wa kutafutiwa makazi, mkakati wa kufuata sheria, mkakati wa kubadilika kutoka kuwa mui na kuwa mwema na mkakati wa wanaume kuamua kushirikiana na wanawake

### 4. 1 Mkakati wa Kuikimbilia Dini

Kulingana na Willmington (2008), katika kutimiza kusudi la dini hapa duniani, nyakati zote binadamu hukimbilia mwenyezi Mungu na maombi kama mkakati wa kutimiza kusudi la Mungu. Anaeleza kusudi la Mungu kwa binadamu anayeomba msamaha, huhusu kuungama dhambi zake, ili Mwenyezi Mungu amsamehe na amsafishe dhambi. Anaendelea kusema kuwa maombi kama mkakati hufungua mwelekeo wa wakristo kwa Mungu kujua nini, jinsi gani na nani wa kumwombea. Kwa hivyo, binadamu anapokimbilia maombi anafanya hivyo kuwasiliana na Mungu anapokuwa na hitaji fulani. Mara nyingi, binadamu huamini kuwa Mungu anamtazama na tayari anajua kile anachokwenda kumwomba. Hali hii hutokana na imani kuwa Mungu atajibu chochote amwambiacho.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 2), kuna wanawake kama vile Mangwasha ambao wanaamini kuwa maombi husaidia kumkomboa mwanaume. Kulingana na Mangwasha, mwanamume ni kiumbe muhimu katika ustawi wa jamii yake. Kwa mujibu wa

Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mwanamume huwa na thamani chanya na kubwa katika jamii. Tunaweza kupata maelezo zaidi kwa kurejelea mfano huu:

> Mangwasha alimwombea mumewe amwepushe mabaya kokote alikokuwa mumewe. Alimwomba asiruhusu mauti au hatari yoyote kumkaribia kwani wanawe walimhitaji, bora awe baba mtu, wamwite baba kwani Sayore alikuwa mvulana mkembe na alihitaji baba. (Momanyi 2019: 2)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 2), inabainika kuwa Mangwasha ana mapenzi ya dhati kwa mumewe Mrima. Pamoja na kwamba mume wake aliamua kumtekeleza akaenda kulewa na kuishi majalalani, Mangwasha anamwombea mumewe amwepushie mabaya kokote alikokuwa. Pia, anamwomba Maulana asiruhusu mauti au hatari yoyote kumkaribia Mrima kwa sababu wanawe Sayore na Kajewa walimhitaji baba atakayewaongoza na kuwalea. Hili linaonyesha Mangwasha na wanawe Kajewa na Sayore walimtarajia Mrima akabiliane na matatizo aliyokumbana nayo kwa ujasiri ili aweze kuhakikisha usalama na ubora wa familia.

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018:272), kuna wanaume ambao wanaamini kuwa, kumtegemea Mwenyezi Mungu kunawasaidia kupata haki. Wanaume hao wanaamini kuwa njia moja ya kuondokana na madhara, matatizo au ukandamizaji wa aina yoyote ni kumwamini Mungu. Kulingana na Kobia, J. M. na Mung'ahu, R. (2017), Mungu amejaa mamlaka na nguvu nyingi isiyo ya kifani katika ulimwengu mzima. Anaendelea kusema ikiwa Rabana ameumba mamilioni ya malaika wenye nguvu, mabilioni ya makundi ya nyota, dunia na viumbe wote waliomo duniani, ana hakika kuwa mtu yeyote anayemwamini Mungu atatumia nguvu zake kwa faida yake. Tunaweza kupata maelezo haya katika mfano ufuatao:

> Mimi ni Rashid mswalihina. Naamini kwamba Mwenyezi Mungu akikumulikia njia, hakuna lisilowezekana. Hakosi kuwamulikia njia wanaofuata maadili. (Mbatiah 2018:272)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 272), Rashid anaamini kuwa kumtegemea Mwenyezi Mungu humsaidia binadamu yeyote kupata haki anayostahiki. Anamweleza Kiguto kuwa mtu anayemwamini Mungu hufunguliwa njia na husaidiwa kukabiliana na changamoto zinazoweza kumkabili. Hali hii inatokana na Kiguto kufanya upelelezi wa kina na kupata wahalifu waliomwibia Rashid mali yake. Aidha, kutokana na kauli ya Rashid anadhihirisha kuwa kuna polisi ambao ni waaminifu na wenye maadili katika kazi

wanayofanya. Anampongeza Kiguto na kudai kungekuwa na polisi wengine kama yeye nchi ya Matuo ingekuwa na imani tele na utulivu kamili.

Vilevile, katika hali nyingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 128), kuna baadhi ya wanaume ambao wanampa Mola nafasi ya kuongoza maisha yao. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kuna baadhi ya wanaume ambao wamebadilika na hawaonyeshi ubabe na udikteta katika jamii inayowazunguka. Haya yanaungwa mkono na maneno yafuatayo:

> "Baba watoto, hamna haja ya kujiua na masikitiko. Sote tumejaribu kufanya kadiri ya uwezo wetu kuwasukuma Mwongi na Rejwa. Yaliyobaki tumwachie Mungu. Najua Mungu ni Mkubwa. *Aamen*. Mark aliitikia. (Mbatia 2018: 128)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 128), Mark Bagite amebadilika na kuwa mwanaume mpya. Hii ni kwa sababu alikuwa na sifa za udikteta, na mfisadi mkubwa aliyetumia madaraka yake kupata alichotaka kama vile, kuwatafutia wanawe Mwongi na Rejwa nafasi za shule na kazi. Mark Bagite anabadilika na kuamini kuwa ni Mwenyezi Mungu tu ambaye ana uwezo na mamlaka ya kuwapa watoto wao kazi ila sio madaraka yake ya kisiasa. Mabadiliko haya ya Mark Bagite, yanamfanya akimbilie maombi na yeye na mkewe wanaamini kuwa Mwenyezi Mungu atatimiza hitaji lao la kuwapa wanao kazi kulingana na matarajio yake.

### 4. 2 Mkakati wa Kuwajibika

Kuwajibika ni kitendo ambacho mtu hulazimika kutimiza jambo fulani aidha kwa mujibu wa sheria, matarajio ya jamii au kwa hiari yake mwenyewe (Bovens, 1998). Anaendelea kusema kuwa mtu anapowajibika huwa anaapa, anaahidi na kuchukua jukumu fulani na hufanya maamuzi kwa uangalifu, hufanya tabia zinazotaka kujiboresha na kuwasaidia wengine.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi, 2018: 148), mhusika Mrima anachukua wajibu wa jukumu lake kama baba na mtafutaji riziki ili kukidhi mahitaji ya watoto wake. Anaamua kuanzisha biashara ya kibanda cha kuchuuza mboga. Kutokana na bidii yake, kibanda hicho kilimsaidia kutimiza mahitaji ya nyumbani pamoja na kuwalipia wanawe Sayore na Kajewa karo. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, jukumu la mwanamume hujitokeza katika tamaduni, mila na desturi ya jamii yake kupitia kufanya kazi na kukidhia familia. Vilevile, nadharia hii inaeleza kuwa mapato huwa muhimu katika ndoa ili mwanamume aweze kutimiza jukumu lake kama mkimu familia. Hii ni kwa kwa sababu

uwajibikaji ni muhimu kwake, kuridhisha mke na watoto. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi kwa kurejelea mfano ufuatao:

> Mrima aliamua kukopa pesa kutoka kwa Lonare na kufungua kibanda cha kuuza mboga. Kibanda hicho kilisaidia kukimu masurufu yao nyumbani pamoja na kuwalipia watoto wake Sayore na Kejewa karo. Mrima hakukata tamaa alitia bidii duka likafunguliwa na kujazwa bidhaa tofauti. (Momanyi 2019: 148)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 148), mhusika Mrima yuko tayari kuchukua jukumu la kutafuta riziki ili kukidhi mahitaji ya watoto wake. Mwanaume anapaswa kuwa na sifa angama kama vile kukidhi familia, ushujaa, ushindani na kulinda usalama wa jamii Connel, R. (1987). Hali hii inamfanya Mrima adumishe nafasi yake kama mdhibiti familia yake, bwana, baba mzazi na mlezi anayewajibika. Lengo lake ni kuonyesha ulimwengu kuwa amebadilisha tabia zake za kilevi na ameacha hila za Sagilu na ameamua kuwajibika. Anamkopa Lonare pesa na kuanzisha biashara ya kuuza mboga. Mapato anayopata kutoka kwa biashara hiyo yanamsaidia kutimiza mahitaji ya nyumbani na kuwalipia watoto wake Sayore na Kejewa karo ya shule.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah, 2018: 210), kuna wavulana kama vile Kiguto wamepewa jukumu ya kuwa kiongozi wa familia yao na mzazi wa kiume. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, nafasi ya mwanamume kuwa kiongozi wa familia na jamii inapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Haya yanabainika katika mfano ufuato:

> Nimejeruhuiwa vibaya nikiwa kazini…nataka uyadhibiti maisha yako ipasavyo. Wewe sio mtoto tena. Kwa hivyo, lazima ukubali machungu ya maisha kama mwanamume. Nimeidhinisha ulipwe kiinuamgongo cha kazini kwangu kwa niaba yangu. Utaenda makao makuu ya jeshi usaidiwe ipasavyo. Babako akupendaye, Joe Bagite. (Mbatiah 2018: 210)

Kutokana na mfano katika Mbatiah (2018: 210), ni dhahiri kuwa jamii alimokulia Joe Bagite ni ya mfumo wa kuumeni unaomtwika mwanaume majukumu ya juu. Inabainika kuwa Joe Bagite anamtaka Kiguto awe mkakamavu. Mwanaume hutazamwa na jamii yake kama kiumbe anayemiliki nafasi kubwa katika kila jambo (Bly, R. 1990). Vilevile, ameeleza kuwa mwanaume hawezi na hapaswi kuonyesha hofu, wasiwasi au unyonge kwani udhaifu wowote uhusishwa na wanawake. Hadhi hii anayopewa Kiguto

kuhakikisha usalama wa mamake, wadogo wake Shaka na Koitalel, inadhihirisha jinsia ya kiume ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya familia na jamii yake.

### 4. 3 Mkakati wa Kukomesha Utumwa Wa Kisasa

Katika jarida la habari za Umoja wa Mataifa (UN), Garten, M. (2021), anaeleza kuwa ulimwengu huadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Utumwa (I. D. A. S) tarehe 2 Disemba kila mwaka. Anaendelea kusema kuwa mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN) kwa ajili ya kukomesha usafirishaji haramu wa binadamu na utumikishwaji ulioanza rasmi mwaka 1951 hutekelezwa siku hiyo. Garten anazidi kueleza kuwa itifaki ya kisheria iliyoundwa na muungano wa umoja wa mataifa ilidhamiria kuimarisha juhudi za kimataifa za kuondoa kazi ya kulazimishwa, ambayo ilianza kutumika mnamo Novemba 2016. Watumwa wanaojipata katika hali hizi hunyonywa wakiwa katika mazingira binafsi kama vile kazi za nyumbani, ujenzi au kilimo.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi, 2019: 229), kuna wanaume kama vile Lonare ambao ni wanamapinduzi wanaowania kukomesha utumwa wa kisasa. Mhusika Lonare alijitwika jukumu la kuwanusuru wavulana waliotumikishwa na Mtemi Lesulia na wadhalimu wengine kama Sagilu. Lonare anawahamasisha wavulana hawa kama vile Sailoki umuhimu wa kuendelea na masomo yao ili wanufaike katika maisha yao. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mwanaume huwa na mamlaka katika jamii yake. Mwanaume anapenda mafanikio ya mwanaume mwenzie tofauti na wanawake (Sherman na Wood, 1982). Hii ni kutokana na malezi walelewayo watoto wa kiume kwa kuwaandaa kuwa na roho ya kuwatakia wengine mazuri. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Wengine walijiunga na masomo kupitia kwa wahisani kama Lonare. Sailoki alikuwa mmoja wao. Shughuli ya kuwasaka watoto na vijana ili kuwarudisha shuleni ilifanywa kote mjini Raria. Lonare alitoa ahadi ya kuwajengea vituo vya mafunzo anuwai. Wengi wakaenda shule na wale waliokuwa wamehitimu awali wakajiunga na vyuo vikuu kupitia ufadhili wa watu binafsi na masharika ya kibinafsi. (Momanyi 2019: 229)

Kutokana na nukuu katika Momanyi (2019: 229), mhusika Lonare anaanzisha harakati za kukomesha makucha ya dhuluma, matumizi ya dawa za kulevya, ukandamizaji na utumikishwaji wa vijana wa kiume na mabwenyenye kama vile Mtemi Lesulia. Hali hii inamfanya Lonare kuwahakikishia vijana wa kiume kama vile Sailoki kwamba wataendelea na masomo yao. Jambo hili linawafanya wawe mbioni kuwakomboa kutoka minyororo ya

utumikishwaji. Lonare anadhihirisha mwamko mpya wa maisha kwa vijana wa kiume. Maelezo haya yanaafikiana na mawazo ya Connel, R. (1987), kwamba mwanaume ni mwenye mamlaka na uwezo mkubwa katika jamii yake. Hii ndiyo sababu Lonare anajitwika jukumu la kuwapa vijana matumaini na maendeleo ya maisha yao. Vilevile, uongozi wa Lonare unahakikisha kwamba vijana wa kiume waliofanya kazi katika shamba la Mtemi Lesulia, wameacha kazi hiyo sugu na kupata elimu inayowawezesha kujitegemea. Sailoki ni miongoni mwa vijana wa kiume waliopata nafasi ya kurudi chuo kikuu. Hali hii inadhihirisha elimu ni chombo cha kujenga mshikamano wa kijamii na uwapa raia ustadi na umilisi wa kukabiliana na changamoto za maisha. Lonare anafanikisha jukumu hili la kuonyesha umuhimu wa elimu kupitia ufadhili wa watu binafsi na mashirika yasiyo ya serikali.

### 4. 4 Mkakati wa Kutafutiwa Makazi

Makazi ni eneo au mazingira ambayo ni makao ya mnyama, binadamu au mmea fulani au aina nyingine ya viumbe hai (Nuissl, 2018). Nuissl anaendelea kusema kuwa ili mtu aweze kujitegemea katika mahali anapopaita nyumbani lazima awe na nguvu za kujitegemea kama vile afya nzuri, uhai na uwezo wa kiuchumi.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 207), kuna viongozi wanaume kama vile Lonare wanaowajali watu wengine. Kulingana na nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kuna baadhi ya viongozi wanaume wanatambua nafasi yao kama viongozi wanaowaonea binadamu wengine huruma. Viongozi hawa wanawanasua wanaume wengine katika hali ngumu inayowakabili. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi kwa kurejelea mfano ufuatao:

> Wale wasiokuwa na kwao Lonare alifanya mipango wakapelekwa kwa makao ya watoto mayatima. Wale waliokuwa na wazazi walipata ushauri nasaha kutoka kwa maafisa hao wa serikali.Kisha walisajiliwa ndipo wakaruhusiwa kwenda makwao. (Momanyi 2019: 207)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 207), ujenzi wa jamii mpya yenye ustawi unatakiwa kufanyika kwa hekima, utu na busara. Kwa mfano, mhusika Lonare ni kiongozi bora mwenye sifa hizi. Alitumia hekima na kujali wengine anatambua umuhimu wa kutafutia wavulana wasiokuwa na mahali pa kuishi makazi. Aidha, Lonare anaonekana akifanya mipango ya kuwapeleka wavulana waliozurura mitaani katika makao ya watoto mayatima. Anafanya hivi ili wapate mahali wanapoweza kuita nyumbani. Vilevile, maafisa wa serikali wanawasaidia kuwapa vijana hao ushauri nasaha na kuwasajili na kisha kuwaruhusu kwenda makwao na kuungana na wazazi wao. Kadhalika, Sailoki anaokolewa kutoka mtaani Taria na

vijana wengine wa kiume na kupelekwa kwa wazazi wao. Hali hii inaunda jinsia ya kiume mpya inayojitegemea na haina udhaifu wa kukosa mahali wanapoweza kuita nyumbani.

### 4. 5 Mkakati wa Kufuata Sheria

Mtu yeyote anapofuata sheria huwa anafahamu kuwa kanuni au taratibu zinazoongoza jamii fulani huratibu mahusiano baina ya watu na jamii. Yaani huwa ni njia mbadala ya kujaribu kupata wokovu kwa njia ya utii wa sheria au kutenda mema. (Tafsiri yetu).

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 116), mhusika Lonare na wenzake kama vile mwanasheria Mwamba kama wahusika ambao wamezinduka, wamepevuka kwa kutambua kuwa ushahidi wa ukweli mahakamani ndio njia mwafaka ya kutenda mema katika jamii na kurekebisha wale wanafunika maovu kwa ushahidi wa uongo. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, ni dhahiri kwamba kuna baadhi ya wanaume wababe ambao wanafuata ukweli, ambao ndio msingi wa jamii yenye umoja na ushirikano mzuri. Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Lonare na wenzake walienda mbio kuharakisha kesi ya ardhi ya Matango. Mwanasheria bwana Mwamba sasa alikuwa na ushahidi wa kutosha kuwasilisha mahakamani. Upande wa serikali uliwasilishwa na bwana Mafamba. Huyu naye alikuwa mfisidi mkubwa aliyejulikana ndani na nje ya nchi. Ndiye aliyekuwa akifunika maovu yote yaliyofanywa na viongozi mbalimbali kama vile Sagilu na Mtemi Lesulia. Mwanasheria Mwamba alikuwa mwambao ambao bwana Mwamba angeweza kuupasua hata kwa baruti za maneno. Hakimu alikata kesi kutokana na ushahidi uliowasilishwa. Waketwa kama vile Lonare, Sagura na Mrima waliochomewa maskani yao wakashinda kesi. (Momanyi 2019: 116)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 116), kuna baadhi ya wanaume ambao wanaamini kwamba kufuata sheria na kuwa wakweli ni njia mwafaka ya kukabiliana na ukiukaji wa haki za kibinadamu, ubaguzi, ukabila na unyakuzi wa ardhi ya wanyonge. Utambuzi huu unawafanya wahusika Lonare, Sagura na Mrima kumuhusisha Mwanasheria bwana Mwamba katika kesi ya kudhihirisha kuwa walichomewa maskani yao ya Matango na Wamunyu. Lonare na wenzake kama vile mwanasheria Mwamba ni wahusika wa kiume ambao wamezinduka. Lengo lao ni kuwarekebisha wafisadi kama vile Sagilu na Mwanasheria Mafamba. Wanafanya hivi ili waache kufunika maovu kwa ushahidi wa uongo.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah 2018: 277), kuna polisi wa kiume kama vile mhusika Kiguto wanapofanya upelelezi wa uhalifu wowote

ule, huwa wanafuata sheria. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kuna baadhi ya viongozi wanaume wenye mamlaka ya kukomesha uovu ili walioathirika na uhalifu wapate haki. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi kwa kurejelea mfano ufuatao:

> Mpango wa Kiguto wa kuwashirikisha chokora katika kumtafuta Onemi ulifanikiwa sana. Alijaribu kila mbinu kukwepa, lakini baada ya majuma mawili, alipatikana. Mbinu ya kubadilishabadilisha magari aliyotumia kwa muda mrefu haukumsaidia. Akakabiliana na Kiguto uso kwa uso. Mwanzoni alikana kuwepo kwa Kibweta cha almasi, lakini Kiguto akamtolea ushahidi wa ule mkataba ambao ulikuwa umetiwa saini na wakili. Onemi hakuwa na njia ya kukwepa tena. Hofu ilimsukuma zaidi kumpa Kiguto hela zake. Isitoshe, Kiguto alikuwa Inspekta wa polisi wa upelelezi aliyeogopwa sana na wahalifu. Tena alikuwa na ushahidi kamili na aliweza kumshtaki Onemi na kukubali kumgawia Kiguto shilingi milioni mia moja. (Mbatiah 2018: 277)

Kulingana na nukuu katika Mbatiah (2018: 277), mhusika Kiguto anatambua kuwa ili amnase Onemi, aliyekuwa anajificha asimpe pesa zake, alihitaji upelelezi wa hali ya juu. Anashirikisha chokora kumtafuta Onemi. Hatua hii inamfanya Onemi kusalimu amri kwani Kiguto alikuwa Inspekta wa polisi aliyeogopwa na wahalifu. Hali hii inasababishwa na ukweli aliotolewa Onemi kuhusu mkataba uliokuwa umetiwa saini na wakili. Zaidi ya hayo, Onemi alihitajika kumpa Kiguto shilingi milioni moja. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mtoto wa kiume ni mrithi anayetenda majukumu yake kulingana na matarajo ya jamii husika. Kwa hivyo, Kiguto anatekeleza jukumu lake la kuwa kiongozi wa familia yao na mrithi wa pesa alizoachiwa na babake Joe Bagite ambazo zingemsaidia kuafikia matarajio ya babake.

### 4.6 Mkakati wa Kuamua kubadilika kutoka Mui na Kuwa Mwema.

Mtu anapofanya mambo mazuri kwa jamii yake humfanya aweze kuaminika na kupewa heshima. Hii humfanya mtu kuchagua jambo linalofaa kwa sababu anaamini ni sawa kufanya hivyo. (Tafsiri yetu). Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, baadhi ya wanaume wanatakiwa kubadilika na kuacha tabia mbaya ambazo zinawafanya waonekane dhaifu, wahalifu na wenye kutojali hisia na uhusiano wao na watu wengine katika jamii. Badala yake, nadharia hii inamtaka mwanaume anayejali maadili yake, anayeshauriana kufanya maamuzi mazuri na wanajamii wengine, na anayedumisha uhusiano mzuri kati yake na watu wengine katika familia na jamii. Mabadiliko ya riwaya katika karne ya ishirini na

moja ambapo anafafanua kuwa riwaya ya kiswahili huwa na mabadiliko ya kidhamira ambayo yanalingana na matukio yanayoibuka kutokana na binadamu kupitia changamoto katika nyanja mbalimbali za maisha (Chaterji, 2004). Mabadiliko hayo huwa ni dhamira zinazowahusu wahusika ili kuweza kubadilika kwa kutenda matendo mazuri na kuacha mabaya yanayowakwamisha kimaendeleo. Hii inazungumziwa na Chaterji, (2004) katika utafiti wake anapochunguza mabadiliko katika mfumo wa kuumeni kwa kuzingatia jamii ya Wahindi kule Uhindi. Anaeleza kuwa wanaume wenye matendo mabaya wana uwezekano mkubwa wa kubadilika na kuwa wazuri katika jamii yao.

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2018: 265), kuna wavulana kama vile Ngoswe na Mashauri ambao wanaamua kuwa watu wema. Hali hii inasababishwa na wao kuamua kuwa wavulana wenye tabia nzuri na kubadili tabia na mienendo yao ya kuwa wafisidi, na kuacha biashara ya dawa za kulevya. Kulingana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, wanaume ni wenye kufanya maamuzi yanayokubalika katika jamii. Mawazo haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Lonare alianza kumpa ushauri kuhusu namna ya kujiepusha na marafiki wabaya. Alimsihi kusahau yaliyopita, awajibikie maisha yake. Baada ya kitambo kidogo, Ngoswe alimhakikishia Lonare mbele ya wenziwe kuwa tokea wakati ule angebadili mwenendo wake. Angeishi kama rafiki zake, Mashauri na Lombo. Alihisi Lonare alimfahamu kuliko alivyodhania. Wakiwa njiani kutoka hospitali, Ngoswe aliungama vitendo vyake viouvu mbele za rafikize, Mashauri na Lombo. (Momanyi 2019: 265)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 265), wahusika Mashauri na Ngoswe wanaamua kubadilika na kuwa wavulana wenye hulka nzuri. Mabadiliko hayo yanachochewa na Lonare ambaye anawapa ushauri wa namna ya kujiepusha na marafiki wanaowafanya wawe wafanyibiashara wa dawa za kulevya na wafisidi. Ngoswe na Mashauri wanaungana na kuamua kuwa miongoni mwa vijana wa kiume ambao wanachangia mabadiliko chanya katika jamii. Wanafanya hivyo kukomesha ufisadi na matumizi ya dawa za kulevya viungani mwa mji wa Taria.

Katika hali nyingine, katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi*, (Mbatiah, 2018: 277), kuna wezi wa jinsia ya kiume kama vile Kibetu wanauasi wizi na wanaamua kuacha uhalifu. Wanadhihirisha wao ni wanaume wanaojali maisha yao. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mwanaume ni kiongozi anayeheshimiwa. Inabainika kuwa mwanaume anapaswa kuwa mtu mzuri asiyejihusisha na wizi au uhalifu. Vilevile, mahusiano

ya binadamu hujengwa kwa misingi ya kukomesha uhalifu katika jamii. (Fasiri yetu). Haya yanabainika katika mfano ufuatao:

> Kibetu alipotoka hospitalini baada ya kulazwa kwa juma moja, alianza kumsaidia Kiguto katika upelelezi. Ndipo inspekta huyo alipogundua kwamba mui huwa mwema. Kibetu aliamua kuachana na uhalifu. Akajaribu kulipia kwa mema yote ambayo Kiguto alikuwa amemtendea kwa kumsaidia katika upelelezi. Kiguto alifurahishwa sana na mabadiliko yake. Akamwajiri kama wakala wake katika usimamizi wa yale majumba ya Ngomeni. (Mbatiah 2018: 277)

Kutokana na nukuu katika Mbatiah (2018: 277), Kibetu anaamua kuacha uhalifu. Anaungana na Kiguto polisi wa upelelezi kukomesha uhalifu. Mabadiliko haya ya Kibetu yanamfurahisha Kiguto kwa sababu Kibetu anajihusisha na mambo mema. Tabia hii ya Kibetu inamfanya Kiguto kumwajiri kama wakala wake katika usimamizi wa majumba yake yaliyo Ngomeni. Kuajiriwa kwa Kibetu kunadhihirisha anaweza kuaminika katika jamii. Hali hii inasababisha inspekta wa polisi kuamini kuwa mui anaweza kuwa mwema. Kulingana na Hill, (1977) anaeleza kuwa watu huweza kubadilika na kueleza hali halisi iliyomo katika jamii. Walio wazuri huweza kuwa wabaya na wabaya huweza kuwa wazuri. Hali hii, husisitiza kubadilika kwa wahusika kulingana na nyakati pamoja na mahitaji ya jamii.

### 4.7 Mkakati wa Wanaume Kuamua Kushirikiana na Wanawake.

Ushirikiano ni hali au tendo la watu wawili au zaidi kuungana na kusaidiana katika shughuli fulani au kufanya kazi pamoja kwa manufaa fulani, kinyume na kufanya kazi kwa ushindani kwa manufaa ya ubinafsi Kethers (2020). Anaendelea kusema kuwa watu wanaposhirikiana, huwa wanalenga kutimiza lengo fulani la pamoja linalotokana na makubaliano ya maandishi au ya mdomo. Katika ushirikiano, wanaume na wanawake wanaungana kufanya kazi au mwanaume anamhusisha mkewe katika utendaji kazi ambazo kitamaduni zilikuwa za mwanaume. Wanaume hao wamedhihirisha ushirikiano baina yao na wenzao wa kike hasa katika masuala ya kifamilia, kidini, kisiasa na kiuchumi ni njia ya kuwasaidia kuwakomboa na kuwawezesha kufikia malengo yao ya maisha.

Aidha, hoja hii ya wanaume kuamua kushirikiana na wanawake, imeelezwa na Frimpong (2012), aliyefanya utafiti kuhusu wanawake katika karne ya ishirini na moja. Kwanza anarejelea nafasi yao hapo awali. Anabaini kuwa, katika bara la Afrika wanawake walionekana kama viumbe vya kuhifadhi boma na pia kuzaa. Huko Uropa, wanawake walidhaminiwa kutegemea nafasi za wazazi wao katika jamii. Kule Uchina, walipatikana

katika fikira tu. Pia, hawakuruhusiwa kufanya kazi katika viwanda au hata kurithi mali. Hata hivyo, karne ya ishirini na moja imekuja na mabadiliko mengi. Chaterji (2004), amejadili mabadiliko katika mfumo wa kuumeni akizingatia jamii ya Wahindi kule Uhindi. Anadhihirisha kuwa nafasi na majukumu ya wanawake katika jamii hiyo yamebadilika kimfululizo katika kipindi cha miaka kumi na tisa iliyopita ikilinganishwa na sasa. Chaterji (2004), ameeleza huko Uchina, Chama cha Ujamaa kiliinua na kuboresha maisha ya wanawake. Kiliwakomboa kutoka kazi za nyumbani na kuwapa kazi viwandani. Huku Afrika, imani kuwa kumwelimisha mtoto wa kike ni kupoteza pesa ilianza kubadilika hasa mwisho wa karne ya ishirini. Huko Uropa, wanawake walianza kupigania usawa wa jinsia zote za wanawake na wanaume.

Vivyo vivyo, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi, 2019: 229), kutokana na mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume, nafasi mpya ya mwanamke imejitokeza. Mwanamke ni mkakamavu, mwenye bidii na mwanaume anaweza kushirikiana naye katika masuala ambayo yanamfaidi kama vile kushirikiana kuanzisha biashara ili wasaidine kukimu mahitaji yake, kisiasa na kielimu. Kwa mujibu wa Connel, R. (1987), jamii huwa na ushirikiano wa watu wote katika jamii hiyo. Maelezo haya yanabainika katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi, 2019: 229), kuwa kijana wa kiume Sailoki ameamua kushirikiana na Mangwasha kuwanusuru wavulana wengine.Mhusika Sailoki anafanya hivi ili awatoe katika mikono ya wadhalimu kama vile Mtemi Lesulia na Sagilu. Tunaweza kupata maelezo haya katika mfano ufuatao:

> Mangwasha alishirikiana na kijana Sailoki kuwasaka vijana wengine na kuwarudisha shueni. Sailoki alishauriwa na Mangwasha pia kuunda chama cha vijana mjini Taria. Sailoki alikusanya vijana wachache waliookolewa kutoka katika shamba la Mtemi Lesulia wakaunda chama kilichoitwa *Youth for Change Movement.* Mangwasha alifanya bidii kuwahamasisha vijana hawa dhidi ya wajibu wa kuanzisha biashara ndogondogo. (Momanyi 2019: 229)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 229), mhusika Sailoki anashirikiana na mhusika wa kike Mangwasha ili yeye na wavulana wengine waweze kuanzisha biashara ndogondogo. Inabainika kuwa Sailoki alikubali usaidizi wa Mangwasha ili aweze kukimu mahitaji yake kwa sababu alitoka familia maskini. Vilevile, Sailoki alianzisha chama kilichoitwa *Youth for Movement*. Hatua hii ya Sailoki kushirikiana na Mangwasha ilimfanya Mashauri na Ngoswe kuungana na wao. Mashauri anatafuta ufadhili wa mashirika yanayosaidia wavulana kupata haki zao katika elimu. Ufadhili huu ndio uliomfaidi Sailoki aliyebahatika kujiunga na chuo

kikuu mjini Taria. Jambo hili lililofurahisha wazazi wake ambao waliamua kujiunga na wavulana hawa kuzindua vijana wengine wa kiume ili wajiunge na shule. Kadhalika, mwamko huu mpya wa Sailoki, Ngoswe na Mashauri unaafikiana na mawazo ya Wells & Holland (2001). Wanaeleza kuwa mwamko wa wanaume ni ishara kwamba wanaume wameitafakari upya hali yao katika jamii ya sasa ambapo wamo mbioni kujikomboa kutokana na umaskini, ukandamizaji na mifumo ya kitamaduni ya jamii ya kiasili.

Kadhalika, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi, 2019: 186), kuna wanaume kama Mrima ambao baada ya kuacha pombe wanakuwa wanaume wapya ambao wanawapenda wake zao kwa dhati na kushirikiana na wake zao kujenga ndoa yao, kuendelea na masomo na kuanzisha biashara ya kuwakimu pamoja. Wazo hili linaungwa mkono na wataalamu mbalimbali akiwemo Connell, (2005), anayeeleza kuwa si kila mwanaume mbabe katika jamii anafaidika na ubabe huo bali husukumwa na mifumo ya jamii zao hivyo inapobidi wabadilike ili kuleta furaha katika familia badala ya kuendeleza kutoelewana miongoni mwao na kuleta maumivu. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi kupitia mfano ufuatao:

> Kwa Mangwasha na Mumewe, maisha yaliwaendea vyema. Kutokana na moyo wao wa kujituma, Lonare aliwapa Mangwasha na Mrima mtaji wa kuimarisha biashara yao. Duka likajazwa bidhaa nyingi zaidi na wateja wakawa wengi katika duka lao kila dakika. Walitegemea duka hilo kufawafadhili kwa kila kitu. (Momanyi 2018: 186)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2018: 186), mhusika Mrima anashirikiana na mkewe kuanzisha biashara ya duka, kutokana na ufadhili waliopewa na Lonare. Inabainika kuwa Mrima na Mangwasha wanasikilizana na wanafanya biashara pamoja ili wakidhi mahitaji yao na ya wanao Sayore na Kajewa. Kwa mujibu wa Parson (2004), hakuna mhusika katika familia anayepewa kipaumbele kutoa suluhisho na maamuzi katika familia za kisasa. Wanaume na wanawake wanashirikiana katika kutoa suluhisho kuhusu jambo lolote linaloleta utata katika familia na maisha kwa jumla. Kauli hii ya Parson (2004), inabainisha kuwa katika familia za kisasa, badala ya mwanaume kutegemewa katika utoaji suluhu, huwa anamshirikisha mwanamke katika jukumu hilo. Kwa hivyo, kila mmoja wao anajihisi kuwa wa maana katika familia huku uhusiano wao ukiwa bora zaidi. Kupitia haya yote inabainika kuwa katika familia ya Mrima kuna umoja na mshikamano kama ndugu na kwa sasa wanatenga muda wa kujadiliana kama bwana na mke wanaopendana na waojali maendeleo na ufanisi wa maisha yao.

Kadhalika, katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, (Momanyi 2019: 186), kuna wanaume kama vile Lonare na Mrima wanaoshirikiana na wanawake kama vile Mangwasha katika masuala ya kisiasa. Kupitia mabadiliko haya yote, ni wazi kuwa mwanamke katika karne ya ishirini na moja yu huru na anafanya kazi nzuri za kupata faida au kulipwa mshahara. Aidha, kiwango chake cha elimu kimeongezeka na anajihusisha na wanasiasa wa kiume. Tunaweza kupata ufafanuzi zaidi kutoka mfano ufuatao:

> Kitimutimu cha siasa sasa kilipamba moto, ikawa kila siku baada ya kazi, Mangwasha alijiunga na mumewe kwenda kushawishi watu kumuunga mkono Lonare.Walijiunga na wafuasi wengine kama vile Sauni na Sagura, wakabisha mlango baada ya mlango. Mangwasha akaunda vikundi vya wanawake na wasichana wa Matango ili kumpigia debe Lonare. (Momanyi 2019: 186)

Kutokana na mfano katika Momanyi (2019: 186), inabainika kuwa mhusika Lonare alikuwa ametambua kuwa, ili apate ushindi wa kura na kuwa mtemi wa Matango, alihitaji kushirikiana na wanawake na sio wanaume peke yao. Jambo hili linaonyesha ushirikiano mwema uliopo kati ya wahusika wa kiume (Lonare, Sagura na Mrima) na wahusika wa kike (Mangwasha na Sauni). Wahusika hawa wote wanashirikiana kushawishi watu wamuunge mkono Lonare katika kampeni za kuwa mtemi wa Matango. Hali hii inadhihirisha wanaume wametambua wanahitaji kujielewa kwanza, wanapaswa kushirikiana na wanawake na wanaume wengine na wajithamini katika juhudi za kutafuta ukombozi wao.

**4.8 Hitimisho**

Katika sura hii, tumechunguza mikakati ambayo wanaume wametumia katika harakati za kupigania ukombozi wao katika riwaya teule za Kiswahili: *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah: 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi: 2019). Mifano mwafaka na maelezo ya kina yametolewa katika riwaya mbili teule. Mikakati hiyo imechunguzwa kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume.

Tumebainisha kwamba jinsia ya kiume imebaini mikakati ya kujikomboa kutokana na ukandamizaji. Mikakati hiyo ni kama vile mkakati wa kukimbilia dini, kuwajibika, kutafuta na kupata makazi, kubadilika kutoka kuwa mui na kuwa mwema na mkakati wa wanaume kuamua kushirikiana na wanawake.

Kwa hivyo, wanaume wamepiga hatua ya kubadili mtazamo wa jadi na kuwa na mtazamo wa kisasa. Mabadiliko hayo ndiyo yamechangia utambuzi wa umuhimu wa kuwa na usawa wa

kijinsia bila kuegemea jinsia yoyote. Utambuzi huu, umemwezesha mwanamume kupata kujielewa mwenyewe, kujitathmini, kujitambua, kujikomboa na kushirikiana na wanajamii wengine ili kujiweka katika nafasi ambayo haimkandamizi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, MCHANGO WA UTAFITI NA MAPENDEKEZO

## 5. 0 Utangulizi

Katika sura hii, tunajumuisha muhtasari wa tasnifu kuanzia sura ya kwanza hadi ya nne. Katika kuchunguza ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili, tumechunguza makundi ya watu wanaohusika na ukandamizaji wa jinsia ya kiume. Pia, tumeangazia athari zinazowapata wanaume kutoka kwa makundi kandamizi na mikakati ambayo wanaume wanatumia katika harakati za kupigania ukombozi wao.

## 5. 1 Muhtasari wa Matokeo Ya Utafiti

Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa kuna baadhi ya wahusika wa jinsia ya kiume ambao wanatumia ubabe wao kwa njia hasi. Wanaume hao ni wezi, wauaji, wana malezi yasiyofaa na wanaongozwa na tamaa za uongozi zinazopelekea ukandamizaji wao na wa wanaume wengine. Aidha, kuna wale wanatumia ubabe wao kwa njia chanya kama vile kuonyesha matendo mema wanayotenda na kutendea wanaume wengine ili yaweze kuboresha maisha yao na ya wanaume wengine.

Katika riwaya teule, wako wahusika wa jinsia ya kiume wanaofuata maadili ya kazi zao na wengine hawafuati maadili ya kazi zao. Hali hii imewapelekea kuwa wakandamizaji na wahalifu wasiojali. Kutofuata maadili ya kazi ndiko kunawapelekea kutotenda haki. Aidha, katika riwaya teule, kuna baadhi ya wahusika wa jinsia ya kiume wanaonyimwa haki zao na makundi ya watu wanaowakandamiza kwa malengo yao binafsi. Hali hii inawafanya wanaonyimwa haki kuwa na maumivu makali katika mioyo yao na msongo wa mawazo. Jambo hili linawafanya wakate tamaa ya kuendelea kutafuta ustawi wao.

Vilevile, kuna viongozi wa jinsia ya kiume ambao wanapata ukinzani mkubwa katika asasi za kisiasa na kiuchumi. Viongozi wa jinsia ya kiume walio na ubabe wa kisiasa na kiuchumi wanawanyanyasa wapinzani wao wasio wababe. Jambo kama hili linapelekea wahusika hao wa kiume kuumia nafsini mwao bila kujua nini cha kufanya kwa sababu maisha yao yanakuwa katika hatari ya kuangamia.

Kadhalika, kuna wazazi wa jinsia ya kiume ambao aidha wanakwepa majukumu yao na wengine wana malezi yasiyofaa. Jambo hili linapelekea watoto wao wa kiume kuwa na tabia zisizofaa kama vile kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya. Jambo hili linawafanya wahusika hao wa kiume kukataliwa katika jamii na kupelekea ukandamizaji wao.

Zaidi ya hayo, kuna baadhi ya wahusika wa jinsia ya kiume katika riwaya teule ambao wana kipato cha chini. Hili linawafanya wakubali kupewa rushwa na wanaume matajiri. Hali hii inawapelekea wajihusishe na ulevi na kutekeleza majukumu yao kama wakimufamilia. Jambo hili linashusha thamani yao kama wanaume wanaotarajiwa kuongoza familia yao vyema.

Kwa upande mwingine, wako wahusika wa jinsia ya kiume katika riwaya teule, ambao wanatumia ubabe kuonyesha matendo mazuri yanayotendewa wahusika wa jinsia ya kiume. Wanaume tulioangazia katika utafiti huu, ndio wanaweka bayana kuwa jinsia ya kiume inapaswa kubadilika na kuwa na matendo mema. Baadhi ya wanaume hao, wanajali wanaume wengine, wanaupendo na ushirikiano wakweli. Mambo haya ndiyo yanasaidia jinsia ya kiume ijikomboe kutoka makundi ya watu wanaowakandamiza na athari zake. Hatua hii ni muhimu katika ukombozi wao kwa sababu wamedhihirisha wanajijali, wanajali wengine, ni wenye bidii, ni wachapakazi na wana mshikamano kwa kujitoa kwa ajili ya wengine ili waendeleze ukombozi, mahusiano mazuri na ustawi wao na wa wengine.

### 5.2 Mchango wa Utafiti

Kutokana na utafiti huu, kuna masuala yanayohusu changamoto wanazopitia baadhi ya wanaume na vyanzo vya ukandamizaji wao. Taswira za ubabe ambazo jinsia ya kiume inadhihirisha katika kutangamana na wanaume na wanajamii wengine kunaibua sababu zinazopelekea ukandamizaji wao.

Aidha, kutokana na utafiti huu tumeona kuwa jinsia ya kiume inakandamizwa na makundi ya watu kama vile, polisi, wezi, makahaba, wanarika wa kiume miongoni mwa wengine. Aidha, utafiti huu utakuwa muhimu ili kuelewa vile jinsia ya kiume invyoathiriwa katika mahusiano yao, kutekeleza majukumu yao na mabadiliko ya kijamii, ya kisiasa na ya kiuchumi.

Kadhalika, utafiti huu umeonyesha taswira hasi za jinsia ya kiume zinazotokana na ukandamizaji. Mambo hayo ni kama mmomonyoko wa maadili, ulevi, matumizi ya dawa za kulevya, mauaji, kukosa chakula, mavazi, malazi na kukosa kuendelea na masomo, kupata malezi yasiyofaa na msongo wa mawazo. Kuonyesha kuwa mambo haya hayafai, yameibua

dhamira chanya ya baadhi ya jinsia ya kiume kama vile kuamua kuwajibika, kushirikiana, kukimbilia dini na kumwamini Mwenyezi Mungu, kufuata sheria na kubadilika kutoka kuwa mui na kuwa mwema. Hivyo, kupitia mikakati hii, tunapata kutatua matatizo ambayo jinsia ya kiume inapata kutokana na ukandamizaji.

Zaidi ya hayo, utafiti huu umeonyesha mambo mbalimbali yanayoathiri jinsia ya kiume katika riwaya teule. Haya mambo yamo katika jamii halisi na yamedadavuliwa kwa kutumia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume ili kuyaweka bayana. Hivyo, ili kuwakomboa wanaume kutokana na mila zilizopitwa na wakati na njia zingine zinazowadhalilisha, wanahitaji wabadilike ili ukandamizaji wao upunguzwe. Kwa hivyo, ikiwa mabadiliko yana manufaa hayafai kukataliwa. Pia, wanaume watafaidika kwani wataanza kutathmini na kupima mambo mageni kabla ya kuyakubali au kuyakataa. Watafiti wa fasihi hasa wa riwaya nao watafaidi maarifa mapya kutokana na utafiti huu.

**5.3 Mapendekezo**

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza suala la ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya *Njozi Yapata Mtenzi* (Mbatiah, 2018) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2019). Utafiti wa baadaye unaweza kufanywa ili kuchunguza kama suala hili la ukandamizaji linajitokeza katika tanzu zingine za fasihi andishi kama vile tamthilia na hadithi fupi.

Kadhalika, utafiti wa baadaye unaweza kutalii iwapo jamii za Afrika zimeasi matendo yanayowakandamiza wanaume. Tanzu za fasihi simulizi kama vile hadithi na ushairi ni sehemu zinazoweza kuchunguzwa kwa upana.

Vilevile, watafiti wa kibayolojia wanaweza kufanya utafiti kubainisha ni misingi ipi inayopelekea wanaume wakandamizwe. Aidha, watafiti na waandishi wa fasihi hasa riwaya wanaweza kutafiti suala la mabadiliko ya jinsia ya kiume katika karne ya ishirini na moja na karne zijazo.

Katika hali nyingine, watafiti wa isimu saikolojia wanaweza kufanya utafiti kubainisha ni kwa nini jamii huwa na upendeleo na tayari huwa imemuhukumu mwanamume vibaya na kwa ukali kuliko mwanamke na kumsawiri kama zimwi au mnyama anayefaa kuogopwa. Aidha, watafiti hawa wanaweza kufanya utafiti kubaini iwapo jamii itapata elimu kuhusu masuala ya jinsia ya kiume.

## MAREJELEO

### A: MAREJELEO YALIYOTOLEWA VITABUNI

Adler, F. (1975). *The Difference of Man and The Diffencence it Make.* New York: Fordham University Press.

Bly, R. (1990). *Iron John: A Book about Men*. New York: Minesota Publishers Limited.

Bovens, M. (1998). *The Quest for Responsibility: Accountability and Citizenship in Complex Organisations*. Cambridge: Cambridge University Press.

Brooks, J. (2012). *The Process of Parenting*. New York: McGraw-Hill Publishers Limited

Bufacchi V. (2005). *Violence, Acts and Omissions*. London: Pluto Publishing Limited.

Burke, K. (1966). *Definition of Man.* Berkeley: University of California Press.

Chachage, S. L.C (2002). *Makuadi wa Soko Huria.* Dar es Salaam: E & D Publishers limited.

Connell, R. W. (1987). *Gender and Power*. Cambridge: Stanford University Press.

____________ (2005). *Masculinities*. Berkeley: University of California Press.

Deutsch, K. W. (1970). *Politics and Government: How People Decide Their Fate*. New York: Houghton Mifflin Press.

Farber, H.S. (2010). *Job Loss and the Decline of Job Security in the United States*. Chicago: University of Chicago Press.

Glenn, E. N. (2002). *Unequal Freedom: How Race and Gender Shaped American Citizenship and Labor*. Cambridge: Harvard University Press.

Hill, J. S. (1977). *The Romantic Imagination*. London: Macmillan Press Limited.

Mbatiah, M. (2018). *Njozi Yapata Mtenzi*. Nairobi: Moran Publishers Limited.

Momanyi, C. (2019). *Nguu za Jadi*. Nairobi: Queenex Publishers Limited.

Msanjila, Y. P. na wenzake (2011). *Isimu Jamii Misingi na Nadhari*a. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Ngwiri, L. (2008). *Powerful Parenting. What Every Parent Should Know*. Nairobi: Queenex Holding Limited.

Parsons, T. (1937). *The structure of social action*. New York: McGrawHill Publishers Limited.

Santrock, J. (2007). *As Topical Approach to Life Span Development*. New York: Mc Graw-Hill Publishers Limited.

Sherman, H. J. & Wood, J. L (1982). *Sociology, Traditional and Radical Perspectives*. London: Harper & Row Publishers Limited.

Sue, D. W. (2010). *Microaggressions and Marginality: Manifestations, Dynamics, and Impact*. Hoboken: John Wiley and Sons Publishers Limited.

Stanley, B. (1967). The Concept of Society. NewYork: MacMillan Publishing and the Free Press.

Sutherland, E. H. (1973). *Analyzing Crime*. Chicago: University of Chicago Press.

Willmington, H. L. (2008). *Choice of God/Higher Power, Perceptions of God/Higher Power, Religious Beliefs and Behaviours*. Cambridge: Stanford University Press.

**B: MAREJELEO YALIYOTOLEWA KUTOKA KWA TASNIFU MBALIMBALI**

Badru, Z. (2020). Mfumo Dume-Chanzo cha Ufungwa wa Wanaume-Uhakiki wa Semi Kutoka Jamii za Kiafrika. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Bayyo, F. B. (2020). "Usawiri wa Jinsia ya Kiume katika Riwaya za Shafi Adam." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).

Binyanya, R. M. (2014). "Sajili ya maafisa wa polisi: Tathmini ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kituo cha polisi cha Central, Nairobi." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Gwachi, M. (2012). "Ukengeushi wa Wasomi katika Riwaya ya Euphrase Kezilahabi." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Katola, E. (2006). "Usawiri wa Mhusika Wa Kike Katika Tamthilia za Kiswahili." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kibigo, M. L. (2019). "Tamathali za Semi Zinazosawiri Ubabedume Katika Majigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo ya Waisukha, Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Semantiki." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro. (Imechapishwa).

Kones, N. C. (2021). "Jinsia Inavyowakilishwa katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa katika Kaunti ya Bomet Nchini Kenya." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Lugano, R. (1989). "Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Masibo, B. (2009). "Gendered Perspectives in Novels of Ngugi wa Thiong'o and Alice Walker." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mavisi, R. (2007). "Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Kazi za Zainabu Burhani", Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mnenuka, A. (2011). "Taswira ya Mwanamke Katika Muziki wa Bongo Fleva." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).

Mwenda, A. K. (2020). "Taswira ya Malezi ya Watoto katika riwaya za Tumaini na Dunia Mashaka Makuu." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mulila, J. L. (2009). "Usawiri Chanya wa Wahusika Wanawake katika Tamthilia za Zilizala na Chamchela." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mutungi, B. (2008). "Usawiri wa Wahusika wa Kiume Kama Kielelezo cha Udume katika Tamthilia za Chacha Nyaigotti: *Mke Mwenza* (1982), *Wingu Jeusi* (1987), *Marejeo* (1986) na *Hukumu* (1992). Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Makerere. (Haijachapishwa).

Nyamemba, R. (2012). "Uchanganuzi Linganishi wa Maswala ya Vijana na Jinsi Yanavyoshughulikiwa na Waaandishi katika Diwani ya Tunu ya Ushairi." Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Opunde, S. (2018). "Uchunguzi wa Masuala ya Kijinsia katika Nyimbo za Daudi Kabaka na John Amutabi." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Masinde. (Haijachapishwa).

Osore, M. K. (2008). "Kinaya katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Raymond, N. M. (2016). "Usawiri wa Mwanamume katika Methali za Kimeru Nchini Kenya." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Pwani. (Haijachapishwa).

Rwegira, T. F. (2017). "Kuchunguza Ujinsia katika Methali za Wakurya". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Scott, G. O. (2020). "Mgogoro wa Kisaikolojia katika Riwaya ya Mkamadume na Unaitwa Nani." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Suzana, S. (2015). "Usawiri wa Mwanamke katika Muziki wa Dansi: Mifano Kutoka Nyimbo za Mbaraka Mwinsheshe." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Wasike, M. W. (2020). "Mwanamke wa Kisasa katika Insha za Kifasihi Magazetini." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kibabii. (Haijachapishwa)

Watuha, A. (2011). "Maudhui ya Waadhi Katika Utenzi wa Adili." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

## C: MAREJELEO YALIYOPAKULIWA MTANDAONI

Aluanga, L. (2013). "The Changing Face of Women Leadership Over the Decades." www.stardardmedia.co.ke.

Ashworth, D. (2017). "Uninvolved Parenting Style. Traits and Effect on Children." www.momjuction.com/articles/how-does-uninvolved-parentingaffect-your-child.

Baker, C.E. (2014). "African American fathers' contributions to children's early academic achievement. https://www.researchgate.net/publication/271929966_African_American_Fathers'_Contributions_to_Children's.

Bufacchi, V. (2005). "Violence, Acts and Omissions: Publication Two Concepts Violence" https://www.researchgate.net/publication_Two_Concepts_of_Violence.

Bwaya, C. (2017). "Kukosa Nafasi Ajira Kusikufanye Ukose Kazi: Wasomaji Waliojiandikisha Kukosa Nafasi. http://bwaya.blogspot.com/2017/07/kukosa-ajira-kusikufanye-ukose-kazi.html

Chaterji, S. A. (2004). Signs of Change in Patriarchal Ideas about Men and Women"s Status and Role in Indian Society. https://www.irenees.net/bdf_dossier-441_en.html.

Cloward na Ohlin (1960). Delinquency and Opportunity." https://study.com/academy/lesson.

Dabbs, J. na Morris, R. (1990). "Uhalifu na Tabia Mbaya kati ya Wafungwa wa Kiume." https://doi.org/10.1016/0191-8869 (94)00177-T.

Deater, K. na Petrill, S. (2006). "Maternal Warmth Moderates the Link Between Physical Punishment and Child External Problems." Https://psycnet.apa.org/record/2006-02145-003.

Galla, S. (2020). Men's Rights Groups. https://mensgroup.com/mens-rights-groups.

Garten, M. (2021). "Utumwa wa Kisasa." Https://news.un.org/sw/story.

Getao, K. (2016). "Parenting the Kenyan Way. Https://www.nation. Lifestyle/saturday/flakes-parenting-the-kenyan-way.

Frimpong, Y. (2012). "The Woman in the 21st Century and Her Effect on the Society." https://m.modernghana.com

Izugbara, C. (2005). "Local erotic songs and chants among rural Nigerian adolescent males. Sex Cult." Https://doi.org/10.1007/s12119-005-1014-9.

____________ (2019). "Young Men, Poverty and Aspirational Masculinities in Contemprary Nairobi, Kenya. https://www.tandfonline.com/doi/abs/10.1080/0966369X.2019.1693347.

Hong, Y. (2019). "Alone and 'left behind': a case study of 'left-behind children' in rural China. https://doi.org/10.1080/2331186X.2019.1654236.

Kabir, S. M. S. (2016). "Methods of Data Collection Basic Guidelines for Research." https://www.scribd.com/document/447337319/Basic-Guidelines-for-Research. (Accessed on 16th March, 2023)

Keeley, B. (2017). "Children in a digital word Newyork. Nations Children Fund." Https://www.unicef.org/media/48601/file.

Kethers, S. (2020). "Cooperation in Work." https://Conference.eresearch.edu.au/the-journey-to-the-research-data-alliance-cooperation-16.

Kgatia, S. T (2013). "Globalization: Facts and Fictions. Asian Journal of Social Sciences, Arts and Humanities." Https://www.multidisciplinaryjournals.com.

Kibet, J. O. & Mavisi, R. (2021). "Taswira ya Mwanamke katika Kipindi cha Bi. Msafwari Runinga ya Citizen Nchini Kenya." Http://doi.org/10.37284/eajss.3.1.430.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. (2020). "Wanawake na Mfumo wa Haki ya Jinai." Http://doi.org/10.37284/eajss.3.1.430.

Kobia, J. M. & Mung'ahu, R. (2017). "Ubabedume katika Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Utenzi wa Fumo Liyongo." https://journals.udsm.ac.tz.index.

Matheka, B. (2021). "Chocheo: Mume si Suti, Ni Jasiri." Http://taifaleo.nation.co.ke/12/1/2021/makala-mume-si-Suti.

Miller, C. (2015). "Class Differences in Child Rearing are those on the Rise." Https://cepa.stanford.edu>news>class-differences-in-child-rearing-are-on-the-rise.

Mowin, A. (2018). "Parenting Styles from Around the World." Http://www.verywellfamily.com.

Msowaya, T. (2021). "Shemeji Mbaroni: Mauaji ya Mchungaji." Http://www.mwananchi.co.ke.tz/22/12/2021/habari/kitaifa/shemeji.mbaroni- mauaji-ya mchungaji-Iringa.

Nuissl, H. (2018). "Settlement/settlement Structure." https://nbn-resolving.org/urn:nbn:de:0156.

Oni, A. (2003). Globalisation, Its Implications and Consequences for Africa. International Journal of African and American Studies. Https://www.researchgate.net/publication/32

Rehm, J. (2009). "Alcohol, Social Development and Infectious Disease." Imepakuliwa: Https://www.researchgate.net/publication/266499471.

Reynolds, W. T. (2020). "The Genealogical Adam and Eve: The Surprising Science of Universal Ancestry. https://source.wustl.edu/2020/06/can-science-prove-adam-eve-really-existed.

Rimando, M. (2015). "Data Collection Challenges and Recommendations for Early Career Researchers." https://www.coursehero.com/file/101246369/Data-Collection-Challenges-and-Recommendations-for-Early-Career.

Scanzoni, J. (1979). "Mikakati ya kubadilisha majukumu ya Wanaume: Uhusiano wa Wanaume na Familia. https://journals.sagepub.com/doi/10.1177/237802311668451.

Simon J. na Preger S. M. (1991). "Male Oppression and Relationships with Women." https://doi.org/10.1080/00377319109517371.

Wairimu, W. (2021). "Kiini cha Wavulana Kutorejea Shuleni." Imepakuliwa: Http://taifaleo.nation.co.ke/18/1/2021/habari-mseto/kiini-cha-wavulana.

Wells, R. na Holland, S. (2001). "Social Learning Theory and the Influence of Male Role Models on African American Children. The Qualitative Report." Imepakuliwa: https://doi.org/10.46743/2160-3715/2001.1994 .